# Nipashe

Jumanne Oktoba 1, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580037

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

m/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Maombi 10,450 ya mikopo elimu yabainika na kasoro

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mabilioni uhujumu yanaweza kujenga

UKURASA 2



HOSPITALI ZA WILAYA 56



Bilioni 107.8/-



VITUO VYA AFYA 215



BARABARA KM 107

**TOLEO MAALUM LA KANDA YA KASKAZINI**

Katika kuwaongezea wigo wa habari wasomaji wetu, kuanzia kesho tutakuwa na toleo maalum la kila siku kwa mikoa ya Kanda ya Kaskazini (Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga)- Mhariri

## Muswada Makonda wamtisha waziri

UKURASA 3



## Mbowe abadili mada kuwakwepa polisi

UKURASA 2

MICHEZO AUSSEMS: SASA NI WAKATI WA SAMBA UK.32 MAONI, KATUNI UK.6

# Mabilioni fedha uhujumu uchumi kufanya makubwa

**Na Romana Mallya**

KIASI cha Sh. bilioni 107.8 kilichotangazwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, kinachotarajiwa kurudishwa na watuhumiwa wa makosa ya uhujumu uchumi, kinaweza kuwezesha serikali kujenga vituo vya afya 215 na hospitali 56 za wilaya.

Kwa mujibu wa Mganga kiasi hicho kingetokana na watuhumiwa wa uhujumu uchumi 467 ambao wamejitokeza kuandika barua za kuomba msamaha.

Tathmini iliyofanywa na Nipashe imebaini kuwa kama kiasi hicho kingepatikana kingeleta mabadiliko makubwa katika sekta za afya na miundombinu.



Rais John Magufuli akipokea toka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, taarifa ya utekelezaji wa ushauri alioutoa kuwasamehe watuhumiwa wa uhujumu uchumi kurejesha fedha Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

Jana, Rais John Magufuli akizungumza baada ya kupokea taarifa ya DPP, alisema fedha zinaweza kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo kama afya, barabara na kulipa mishahara ya watumishi.

Nipashe imebaini kuwa makadirio ya ujenzi wa kituo kimoja cha afya ni sawa na Sh. milioni 500 ambazo zikigawanywa zinaweza kujenga vituo vya afya 215 na kila kata kupata kituo kimoja.

Pia kiasi hicho cha fedha kikiingizwa kwenye ujenzi wa hospitali za wilaya, kitawezesha wilaya 56 kuwa na hospitali.

Kadhalika, Nipashe imebaini kuwa iwapo fedha hizo zitaelekezwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami, zitawezesha kujenga barabara yenye urefu wa kilomita 103 (kwa mfano, kutoka Dar es Salaam - Chalinze). Kilomita moja ya barabara ya kiwango cha lami inagharimu Sh. bilioni moja.

Akizungumza Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Magufuli alimpongeza DPP pamoja na watendaji wake kwa kazi wanayoifanya na kwamba idadi hiyo ya watuhumiwa 467 iliyojitokeza kuitikia ushauri alioutoa, hakuitegemea.

"Sikutegemea kama watu wengi wangejikotekeza, watuhumiwa 467 wa kesi za uhujumu uchumi wameandika barua wakiomba wasamehewe na kulipa fedha wanazodaiwa kwa awamu, kadiri watakavyokuwa wamekubaliana nyinyi na serikali, kwa kweli sikutegemea.

"Jumla Sh. 107,842,112,744.4 zitapatikana, nikupongeze DPP pamoja na watendaji wenzako wanaokusaidia kwenye ofisi yako, ninawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya nasema kwa dhati ofisi yako inafanya kazi kubwa," alisema na kuongeza:

"Kwanza nikiri sikutegemea kama wangejitokeza watu 467 mpaka sasa na umeeleza wengine wameshindwa kwa sababu mchakato wa kuandika barua kwenye magereza wengine wamecheleweshwa na kuna barua ambazo hazijafika, ambazo zimekwama magerezani. "Kwa hiyo kuna barua za watu wanaoomba msamaha zimekwama kwenye ofisi zako za mkoa na nyingine zimekwama magerezani, na umechomekea hapa nikuongezee siku tatu."

"Kwanza, huu mwitikio ni mkubwa sana wa watu 467 na kama kweli wapo waliokwamishwa na wamekwama kutokana na umbali kutoka mikoani kuja hapa na wengine kwenye mchakato ndani ya magereza na umeniomba siku tatu, hakuna tatizo, mimi naomba nikupe siku saba, ili usiniombe siku nyingine."

Rais Magufuli alisema alitoa siku siba za awali ili watuhumiwa wote wanaotaka kupata msamaha kwa kupitia mchakato wa kisheria, wafanye hivyo na wameitikia na fedha Sh. bilioni 107.8 zitaokolewa.

"Nina uhakika hawatarudia makosa yao, ninafikiri niwaongezee siku saba zaidi, lakini nitoe tahadhari, baada ya siku hizi kuisha wale wote watakaohusika kwenye masuala ya uhujumu uchumi, sheria ichukue mkondo wake.

"Isije ikawa imejengeka mazoea, kwamba kesi ya uhujumu uchumi haipo, watakaoshikwa baada ya siku hizi saba nilizoongeza na wale ambao wana kesi mpya, kwa sababu leo mtu akihujumu apelekwe kwenye kesi hausiki na huu msamaha."

**SIKU SABA BASI**

Alisisitiza kuwa katika kesi za uhujumu uchumi watu watakaoshikwa kuanzia jana na kuendelea waendelee nazo.

"Siku saba ambazo nimeongeza kwa wale ambao wamekwama, wameandika barua lakini bado zipo magerezani hazijakufikia (DPP), lakini zimeandikwa na wale ambao wameandika lakini barua zipo kwenye ofisi zako za mikoani.

"Inawezekana mwingine akawa amejifikiria zaidi katika siku ya leo (jana) hadi siku ya saba akatoa maamuzi yake."

**WANAODANGANYWA**

Rais Magufuli alisema anafahamu wapo wanaodanganywa, wanaambiwa msamaha ni wa uongo.

"Hakuna msamaha wa uongo, ukishatoa msamaha ni msamaha, huwezi ukatoa msamaha wa majaribio, huwezi ukatoa msamaha wa kumtega mtu, msamaha ukishatoa ni msamaha, kinyume na hapo labda wewe unayeutoa utabeba hiyo dhambi kwa Mungu," alisema.

Alisema anafahamu wapo wengine wanadanganywa na mawakili wao ili waendelee kuwachomoa fedha watu hao.

"Wanawaambia ukiomba msamaha maana yake umejishtaki mwenyewe, hao shauri yao wachague kusikiliza mawakili wao au wachague kukusikiliza DPP na ushauri wangu nilioutoa, ndio maana ninasema nimetoa siku saba nyingine, sitatoa tena," alisisitiza.

Kuhusu waliojitokeza kuomba msamaha, Rais Magufuli aliwapongeza kwa kuandika barua na kuiomba ofisi ya DPP iharakishe ili watu waanze kuwa huru, watoke wakajumuike na familia zao.

"Mtu akishalipa fedha na mkishafanya michakato yote ya kimahakama, kwa sababu waliingia kwa njia ya mahakama watatoka kwa njia ya mahakama, muwahishe haraka kwenye vyombo vya sheria ili waachiwe, wakajumuike na familia zao, isije hawa 467 mtakapochambua labda mkajikuta wamebaki 400 au 300 wakakaa tena wanasubiri, ilikuwa wiki, ikawa wiki mbili, mwishoe mwezi, hadi mwaka, dhana ya msamaha haitakuwa na maana," alisema.

Alimweleza DPP kuwa anaamini ofisi yake imejipanga vizuri na hatua itakuwa ni kutoa msamaha.

"Wapo walioshikiliwa na maofisa wa magereza kwamba sipeleki ombi lako lazima na sisi unatuachaje tunaokushikilia..., Kamishna wa Magereza upo hapa? Fuatiliane wote waliopo magereza ambao wameomba msamaha huu kwa DPP ili msiwakwamishe," alisisitiza.

"Ili watu kwa dhamira yao wala msiwalazimishe, pasitokee mtu wa kulazimishwa kuomba msamaha kwa hiari yao katika siku hizi, nafikiri ni kitu kizuri hizi Sh. bilioni 107 zitatumika kujenga hospitali, barabara na kulipa mishahara ya wafanyakazi.

Alisema watuhumiwa hao, walikuwa na shughuli na biashara zao zilikuwa zimekwama, waje washiriki pamoja na serikali katika kuziendeleza na serikali ikusanye kodi.

"Lengo letu kubwa ni kujenga nchi yetu, nilifikiri DPP mkashirikiane na ofisi nyingine, kama kesi ilikuwa ikisimamiwa na ofisi ya Takukuru mkashirikiane vizuri kwa vile DPP ameshaiidhia kwamba anataka kuwasamehe kwa mujibu wa sheria na taratibu basi mkashirikiane nao, kama ni suala la upelelezi Jeshi la Polisi au Magereza mkashirikiane," alisema.

**AWAONDOA WASIWASI**

Aliwahakikishia wanaotubu makosa yao na kurudisha walichokiri waasiwe na wasiwasi. Alisema hawezi kufanya kazi ya kitoto, siyo kwa wakati huo na kwamba akishasema ametoa msamaha maana yake ni msamaha kweli.

"Msidanganywe, hao wanaowadanganya wanataka mwendelee kukaa gerezani, na kadiri mtakavyokaa msimlaumu mtu yeyote, DPP amesharidhia ameguswa na Watanzania wengi wangependa kuwaona hao watu wakirudisha na kutubu dhambi zao, lakini hatuwalazimishi."

"Nitoe angalizo kwa DPP kwa wale wanaoshikwa na kesi za uhujumu uchumi, wasifikiri wanahusika na msamaha huu, kashughulike nao kisawasawa, siyo kwamba kesi za uhujumu uchumi zimefutwa."

"Ziliundwa kwa mujibu wa sheria, ila kwenye hili nilitoa ombi na ombi limekubalika kwako na wasaidizi wako, na

INAENDELEA UK 8

## Mbowe abadili mada kuwakwepa polisi

**Na Godfrey Mushi, HAI**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, jana alilazimika kuendesha mkutano wa ndani huku kamanda wa polisi wa wilaya akiwa ndani na polisi wengine wakiwa wamezingira nje ya jengo.

Kikao hicho ambacho ni cha ndani, kiliongozwa na Mbowe ambaye ni Mbunge wa Hai. Kutokana na polisi kuingilia mkutano huo, alijikuta akibadilisha mwelekeo wa mazungumzo yake huku akiwasifia polisi kwa kuhudhuria mkutano huo pia akiwapiga vijembe kiaina.

Katika video iliyosambaa mitandaoni, Mbowe alisema anashangazwa na woga uliopo licha ya vyama vya upinzani kutoruhusiwa kufanya mikutano.

"Mnaogopa nini? Ushindani? Mmefunga wenzenu mikono miaka minne, mmewafunga miguu miaka minne, ngoma (uchaguzi) unanyanyuka keshokutwa bado mnataka kuwafunga mikono. Hofu ya nini kama unajiamini? Tuingie 'field' (eneo la kazi) tunaone shughuli inavyokuwa pevu," alisema Mbowe.

Aidha, aliwataka viongozi kutambua kuwa uchaguzi huo si lelemama na kwamba Chadema inajiandaa pasipo kupigana na mtu bali kutafuta haki.

"Vikao vya kupeleka rufani ni utaratibu lakini kuna maelekezo maalum yametolewa ya kuwaengua wagombea wetu. Kumwona kamanda wa polisi amekuja kwenye kikao cha ndani cha chama unafikiri ni bahati mbaya? Eti anatupenda sana?" Alihoji huku wanachama wakicheka na kumkaribisha kwa kusema: "Mgeni wetu karibu sana".

"Kuna vihunzi vingi tulivijua mapema kama vya kadi, watu wakose kadi ili watu wapite bila kupingwa, wakijua hakuna chama cha upinzani chenye uwezo wa kutoa kadi kutoka Mtwara mpaka Kigoma mpaka Tanga. Chadema tuko vizuri," alisema.

Mwenyekiti huyo baada ya kuzungumza hayo, alisema ameyazungumza hayo kama tahadhari ili wanachama na viongozi wa Chadema wajipange mapema, ili wagombea wa chama hicho wasije wakaenguliwa pasipo sababu za msingi.

Jana, mkutano huo uliendeshwa kwa saa kadhaa chini ya ulinzi mkali wa askari wa Jeshi la Polisi wakiwamo askari kanzu.

Askari kanzu pamoja na askari waliokuwa na silaha walivamia mkutano huo saa 5:00 asubuhi na kuingia ndani ya ukumbi na kuhojiana na baadhi ya viongozi na baadaye kuimarisha ulinzi kila kona ya eneo hilo hadi saa 10 jioni.

Wakati Polisi wanazingira ofisi za Chadema zilizoko mtaa wa Gezaulole, Mbowe alikuwa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai, Helga Mchomvu, madiwani na makatibu wa Chadema.

Polisi waliovamia mkutano huo na kuweka ulinzi mkali mwanzo hadi mwisho wa mkutano huo, walikuwa wakiongozwa na Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Hai, Lwelwe Mpina.

Nipashe ilipofika eneo hilo, ilishuhudia polisi wakiwa wameweka ulinzi zilipo ofisi hizo ambako Mbowe alikuwa ameegesha gari lake lililokuwa na utambulisho wa Kiongozi wa Upinzani Bungeni (KUB).

Alipotafutwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kuzungumzia hatua hiyo ya polisi alisema: "Polisi wana kazi ya kumlinda kila mtu na kuhakikisha usalama wa

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA

# Lugola: askari wote wahamishwe kituoni

**Na Felix Mwagara, KATAVI**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani Katavi, kuwahamisha askari wote wa Kituo cha Polisi Majimoto kutokana na tuhuma mbalimbali zinazowakabili askari hao.

Waziri Lugola alitoa agizo hilo jana kwenye mkutano wa hadhara uliohudhuriwa na mamia ya wananchi wa Mji wa Majimoto, Wilaya ya Mlele wakati akijibu kero mbalimbali za wananchi.

Waziri Lugola alisema kero zilizowasilishwa na wananchi hao, zinaonyesha askari wa kituo hicho wanajihusisha na vitendo mbalimbali vya rushwa, kupiga wananchi ovyo, kushindwa kudhibiti ulinzi na usalama pamoja na kushughulikia malalamiko ya wananchi.

"Natoa agizo hili liwe fundisho kwa askari wote wasiowaaminifu kote nchini, Kamanda wa Polisi wa Mkoa huu natoa siku saba askari wote wa kituo hiki wahamishwe na waletwe wengine ili wajifunze," alisema Lugola.

Baada ya agizo hilo, waendesha bodaboda na wananchi wengineo, walishangilia na kusema kuwa mji huo sasa utatulia kutokana na uwepo wa amani bila kuwa na manyanyaso.

Mmoja wa wananchi aliyetoa malalamiko dhidi ya polisi katika kituo hicho, Malewe Maswe, alilalamikia kuwa baadhi ya askari hao walimpiga na kumsababishia maumivu makali ya miguu kutokana na kuhoji kosa lake la kuletwa kituoni hapo baada ya kugombana na mwalimu mmoja katika mji huo.

"Tulikuwapo na mwalimu niliyegombana naye kituoni hapo, askari wakaniambia nendeni mkaelewane na mwalimu huyo, nikawaambia hatuwezi elewana maana zoezi hilo lilishindikana, askari wakasema unatufundisha kazi, yule pale dogo (askari ambaye alikuwa katika mkutano huo) simjui jina lake alinipiga kipigo sana, na askari mwingine bonge anachochea hii ndiyo Serikali ya Magufuli," alisema Maswe.

Waziri Lugola alijibu kero mbalimbali, ikiwamo ya mkazi wa Mji huo, Malugu Mayombi, ambaye ni mkulima maarufu wa mpunga wa eneo hilo, ambaye aliangua kilio kwa waziri akidai polisi wameshindwa kushughulikia kesi yake ya madai ya Sh. milioni sitini anazomdai mfanyabiashara Sali Kulwa maarufu TBS aliyemuuzia gunia 623 za mpunga.

"Waziri wangu, naomba unisaidie mimi maskini, ujio wako utaniokoa na kuomba Waziri unisaidie nadai shilingi milioni 33 na laki 5 (33,500,000) kati ya Sh. milioni 60, nimelipwa Sh. milioni 26 na laki 5 (26,500,000) pekee, nimeshindwa kuendeleza kilimo naishi kwa shida, nilikuwa nalima ekari 100, kwa sasa nalima ekari 30 tu, nisaidie jamani, nateseka mimi," alisema Mayombi.

Waziri Lugola alimwagiza Kamanda wa Polisi kushirikiana na Mkuu wa Polisi Wilaya kulitatua suala hilo kwa wiki moja wamkamate mtuhumiwa na aweze kulipa fedha za Mayombi.

# Waombaji 10,450 elimu ya juu wakutwa na kasoro

**Na Salome Kitomari**

WAOMBAJI 10,452 kati ya 81,992 wa mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2019/20, wamekutwa na dosari kwenye maombi yao zinazoweza kuwanyima sifa ya kupata mikopo hiyo.

Kwa mujibu wa tangazo lilitolewa juzi kwenye tovuti ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu nchini (HESLB), waombaji hao wamepewa muda wa siku nne kurekebisha kasoro hizo.

Kwa mujibu wa nyaraka hiyo wengi wa waombaji wana makosa kwenye eneo la vyeti vya kuzaliwa vinavyotolewa na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita).

Nyaraka hiyo imeonyesha zaidi ya waombaji 10,000 wana kasoro kwenye vyeti vya kuzaliwa na wametakiwa kurekebisha kuanzia jana hadi Oktoba 3.

"Hatua ya HESLB inafuatia kukamilika kwa uhakiki wa maombi ya mikopo na kubainika baadhi ya fomu za maombi ya mikopo zina upungufu unaozuia kuendelea na hatua ya kupangiwa mikopo," alisema.

Pia tangazo hilo lilibainisha kuwa upungufu huo ni pamoja na kukosa nyaraka ama viambatanisho vilivyothibitishwa na mamlaka husika na saini za waombaji na wadhamini wao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mawasiliano Mwandamizi wa HESLB, Veneranda Malima, alisema mwongozo unasema mwanafunzi ataweka viambatanisho ambavyo vimethibitishwa na mamlaka husika.

"Baadhi yao wameweka vyeti, lakini hakikuthibitishwa na hizo mamlaka na kukifanya kisiwe halali, tumetoa siku nne kuthibitisha nyaraka hizo wakishindwa hawataingia kwenye hatua inayofuata ya kugawiwa mikopo," alisema.

Veneranda alisema majina hayo yamebainika wakati wa kupitia orodha ya waombaji na baada ya siku hizo kupita wanaanza kugawa mikopo kwa waombaji wenye sifa.

Aprili mwaka huu, Rita ilitangaza kuanza uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa na vifo kwa wanafunzi wanaotaka kuomba mikopo kupitia mfumo wa kielektroniki.

Wanafunzi hao walitakiwa kujaza fomu maalum kwenye mtandao na kuambatanisha vyeti vyao ili kuhakikiwa kama walivyonavyo ni sahihi.

Rita ilieleza kuwa baada ya uhakiki, majina ya wahusika yatapelekwa Bodi ya Mikopo kwa njia ya mtandao kwa ajili ya kupatiwa mikopo kwa mujibu wa sifa zilizoainishwa na bodi hiyo.

Mwaka jana Rita ilifanya uhakiki wa vyeti 108,000 kati yake 2,000 vilibainika kuwa na kasoro mbalimbali ikiwamo kughushi na wapo waliofikishwa mbele ya vyombo vya sheria.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Ocean Business Partners, Abdulsamad Abdulrahman, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kongamano la mafuta na gesi. Kulia ni Makamu wa Rais wa CWC Group, Tiago Marques. **PICHA: JOHN BADI**

# Muswada wa Makonda wamtisha waziri

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Agustino Mahiga, amesema baadhi ya wabunge wamemtisha kuwa Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Mirathi uliowasilishwa kwake na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda ni kaa la moto.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akifungua mjadala kuhusu kuelekea mabadiliko katika Sheria ya Kimila na Mirathi ulioandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF).

Dk. Mahiga alisema kunahitajika elimu ya kutosha kwa wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini na kimila kwa kuwa sehemu kubwa ya muswada huo inagusa imani za watu, hivyo haitakuwa rahisi kufanya mabadiliko bila kuwapa elimu.

"Ninyi WiLDAF na wadau wengine mnapaswa kufanya kazi kubwa sana ya kuelimisha watu kwa sababu kuna wabunge wameshaniita na kuniambia huo muswada uliopewa ni kaa la moto. Sasa hii ni dalili kwamba kuna kazi kubwa ya kufanya, hivyo kaeni na wadau muwaelimishe umuhimu wa mabadiliko," alisema Dk. Mahiga.

Pamoja na hayo, Dk. Mahiga alisema serikali itaendelea kutatua changamoto za kimila wanazokutana nazo wajane, wanawake na watoto katika masuala ya mirathi ili kuhakikisha wanapata haki.

Waziri Mahiga alisema kama tatizo ni sheria, serikali iko tayari kupokea maoni ya wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na WiLDAF ili kuwa na sheria itakayotoa haki sawa kwa wote, yaani wanawake, wanaume na watoto.

"Sote tunafahamu kuwa Sheria ya Kimila Na. 4 inatokana na mila na desturi zetu. Ombi langu kwenu mwendelee kuhamasisha jamii kujali familia, wanawake na watoto kwani mabadiliko makubwa yanayotakiwa ni ya kifikra na jamii kuacha kudhulumu mali za marehemu kwani watoto wataathirika," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa WiLDAF, Anne Kulaya, alipongeza serikali kwa kupokea rasimu ya mabadiliko ya sheria ya mirathi waliyoiwasilisha serikalini na kwamba anaamini serikali itaifanyia kazi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

23 -09-2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe **29-09-2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Dar -Es-Salaam kuelekea Geita, gari hizo zenye namba za usajili:

   **T660 BZU/T 310 DDH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 20**
   **Upana - mita 4.2**
   **Kimo - mita 4 .6**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Geita Kupitia Dodoma,** gari zitasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215437302

## TOLEO MAALUMU

# TOLEO MAALUM LA MAADHIMISHO YA MIAKA 70 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA

1949 — 2019

# CHINA NA TANZANIA BEGA KWA BEGA KUJENGA JUMUIYA YA MUSTKABALI WA PAMOJA YENYE UKARIBU ZAIDI



*Bi. Wang Ke, Mh. Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China nchini Tanzania*

JAMHURi ya Watu wa China ilianzishwa Oktoba 1, 1949. Katika kipindi cha miaka 70, China imepita safari ndefu ya kujiendeleza kutoka nchi maskini na dhaifu na kuwa nchi yenye neema na yenye nguvu. China sasa ni nchi ya pili kwa nguvu ya uchumi duniani, nchi kubwa zaidi ya kiviwanda, nchi kubwa zaidi kwa biashara ya bidhaa na ni nchi yenye akiba kubwa zaidi ya fedha za kigeni.

Katika muda wa zaidi ya miaka 70 iliyopita, uchumi wa China umekuwa na ongezeko la kasi na endelevu. Tangu ilipoanza kutekeleza sera ya mageuzi na kufungua mlango mwaka 1978, wastani wa ongezeko la pato la ndani la taifa GDP kwa mwaka lilikuwa karibu 9.5%. Wakati huo huo, wastani wa pato la taifa kwa kila mtu umeongezeka kutoka dola za kimarekani 240 na kufikia takribani dola za kimarekani 10,000, na mwaka 2018 pato la ndani la China GDP lilifikia dola za kimarekani trilioni 13.

Katika muda wa zaidi ya miaka 70 iliyopita, sayansi na teknolojia nchini China imepiga hatua mara kwa mara. Chombo cha safari kwenye anga ya juu chenye binadamu, utafiti wa sayari ya mwezi, sayansi ya Quantum, utafiti wa bahari yenye kina kirefu, kompyuta zenye kasi kubwa na satelaiti za uongozaji zimerushwa moja baada ya nyingine, huku mafanikio kadhaa ya kisayansi na kiteknolojia yamefikia viwango vya kuongoza duniani.

Katika muda wa zaidi ya miaka 70 iliyopita, kiwango cha maisha na ustawi wa jamii ya watu wa China vimekuwa vikiongezeka bila kukoma. Wastani wa pato linaloweza kutumiwa na mtu kwa mwaka umeongezeka kutoka chini ya dola za kimarekani 27 za mwaka 1978 na kuwa dola za kimarekani zaidi ya 4,000 za leo, zikiwa zimeongezeka mara 160. Katika muda wa zaidi ya miaka 40 ya utekelezaji wa sera ya mageuzi na kufungua mlango, China imewaondoa watu milioni 740 kutoka kwenye umaskini, na wastani wa muda wa kuishi wa wachina umeongezeka na kufikia miaka 77.

China imekuwa inahimiza kujenga jamii yenye mustakabali wa pamoja kwa binadamu. Wazo la kimsingi la jamii hii, ni kuwa wakati tunakabiliana na masuala na changamoto za dunia, tudumishe amani badala ya vita, maendeleo badala ya umaskini, ushirikiano badala ya migongano na kunufaishana badala ya kujinufaisha.

Uzoefu wa miaka 70 wa China unaonyesha kuwa, ni pale tu usiposahau ulipoanzia, ndio unaweza kufanikisha lengo lako. Kutafuta furaha kwa watu wa China na ustawishaji mkubwa wa taifa la China ni nia yetu thabiti na lengo letu lisiloyumba. Mwaka kesho, China inatarajia kutimiza lengo la kwanza la karne la kujenga jamii yenye maisha bora kwa pande zote, na watu milioni 16 waliobaki kwenye umaskini wataondolewa kwenye umaskini.

Uzoefu wa miaka 70 wa China unaonyesha kuwa mwelekeo unadhamiria siku za baadaye huku njia ikidhihirisha mustakabali. Tumepita kwa mafanikio kwenye njia ya ujamaa wenye umaalum wa China, wachina sasa wameinuka na kuweza kujitetea, na kujitajirisha na kuwa na nguvu. Dunia ina rangi mbalimbali, na hakuna njia moja ya maendeleo. Njia inayofuatwa na nchi inatakiwa kuwa ile inayoendana na mazingira ya taifa, inayohimiza maendeleo na inayoleta manufaa endelevu kwa watu wake.

Miaka 70 ya uzoefu wa China inaonyesha kuwa kufungua mlango kunaleta maendeleo na kujitenga kunarudisha nyuma. Sera ya mageuzi na kufungua mlango ni ufunguo muhimu kwa China kupata maendeleo makubwa ya kiuchumi na kijamii. Katika siku za baadaye, China itafungua mlango zaidi na kushirikiana kwa karibu zaidi na nchi nyingine duniani, na kuleta maendeleo na neema zaidi kwake yenyewe na kwa dunia kwa ujumla.

Mwaka huu pia ni mwaka wa maadhimisho ya miaka 55 tangu kuanzishwa kwa uhusiano wa kibalozi kati ya China na Tanzania. Nikiwa balozi wa China nchini Tanzania, ninafurahi kuona kuwa katika miaka 55 iliyopita, urafiki wa jadi kati ya China na Tanzania ulioanzishwa na viongozi waanzilishi wa nchi mbili umevuka majaribio ya kimataifa, na ushirikiano wa pande mbili wa kuheshimiana na kunufaishana umeleta mafanikio makubwa na kuleta mambo "makubwa zaidi" na "ya kwanza" nchini Tanzania na hata Afrika.

Kwa mfano, reli ya TAZARA bado ni mradi mkubwa zaidi uliojengwa kwa msaada wa China; daraja la Nyerere lililojengwa na kampuni ya China ni daraja la kwanza la kamba linalovuka bahari kwenye eneo la Afrika Mashariki; na maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam iliyojengwa kwa msaada wa China, ni maktaba ya kisasa barani Afrika; mradi wa mkonga wa mawasiliano ya habari wa Taifa uliogharamiwa na Benki ya Exim ya China ni "njia kuu ya mawasiliano ya taifa" nchini Tanzania; Daraja la juu la Ubungo linaloendelea kujengwa na kampuni ya China litakuwa ni daraja la kwanza lenye ngazi nyingi na njia nyingi nchini Tanzania. Wakati huo huo, China ni chanzo kikubwa cha uwekezaji kwa Tanzania, mshirika mkubwa wa biashara na mkandarasi mkubwa wa ujenzi. China pia ni nchi inayotumia idadi kubwa zaidi ya watumishi watoa msaada wa matibabu nchini Tanzania na pia ni nchi inayotoa udhamini mkubwa zaidi wa masomo wa kiserikali kwa Tanzania. Kwa ufupi ni kuwa, ushirikiano kati ya China na Tanzania umeleta manufaa halisi kwa watu wa nchi mbili.

Wiki mbili zilizopita Rais Xi Jinping wa China alitoa amri ya kutoa nishani ya urafiki kwa mheshimiwa Dk. Salim Ahmed Salim, aliyekuwa waziri mkuu wa Tanzania, nishani hii ya urafiki ni tuzo ya heshima kubwa ya China kwa wageni. Dk. Salim ni mmoja wa marafiki wa watu wa China, aliteuliwa kuwa balozi wa Tanzania nchini China akiwa na umri wa miaka 27. Mwaka 1971, akiwa mwakilishi wa kudumu wa Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa, aliongoza kampeni ya kuunga mkono Jamhuri ya Watu wa China irudishe kiti chake halali kwenye Umoja wa Mataifa. Na baada ya kustaafu, amekuwa mwenyekiti wa Chama cha urafiki kati ya China na Tanzania. Dk. Salim, ambaye ni mwafrika pekee kupewa tuzo hiyo, anastahili kabisa nishani hiyo. Sio tu ni utambuzi mkubwa kwa mchango wake kwenye uhusiano kati ya China na Tanzania, bali pia ni heshima kubwa kwa urafiki wa jadi kati ya China na Tanzania.

China na Afrika zimefurahia ushirikiano wa jadi. Kwa zaidi ya nusu karne iliyopita, China na Afrika zimeshirikiana kwa shida na raha, na kuunda jumuiya yenye mustakbali wa pamoja.

Kwa watanzania na marafiki wote wa Afrika, China itaendelea kufuata kanuni zake tano za kutoingilia njia za maendeleo za Afrika zinazoendana na mazingira ya taifa, kutoingilia mambo ya ndani ya Afrika, kutozifanya nchi za Afrika zifuate maoni yetu, kutoweka masharti ya kisiasa kwenye misaada kwa Afrika, na kutotafuta maslahi binafsi ya kisiasa kwenye uwekezaji au kugharamia ushirikiano na Afrika.

Tukiangalia siku za baadaye, tuko tayari kufanya kazi pamoja na Tanzania na nchi nyingine za Afrika kutekeleza mapendekezo manane makuu ya mkutano wa kilele wa baraza la ushirikiano kati ya China na Afrika uliofanyika Beijing mwaka 2018 na kuiunganisha kwa karibu utekelezaji wa pendekezo la Ukanda Mmoja, Njia Moja na ajenda ya maendeleo ya mwaka 2063 ya Umoja wa Afrika na mikakati ya maendeleo ya Tanzania na nchi nyingine za Afrika, ili kuweka nguvu mpya kwenye ushirikiano wa kunufaishana kati ya China na Tanzania na kati ya China na Afrika, na kujenga jumuiya ya mustkabali wa pamoja yenye ukaribu ya China na Afrika.

Ningependa kutumia fursa hii kuonyesha shukrani zangu za dhati kwa marafiki zetu wa Tanzania na wa kimataifa wanaounga mkono China kwenye mageuzi na kufungua mlango na kazi ya kuunganisha taifa letu. Wakati huo huo, naitakia Tanzania ipate maendeleo makubwa kwenye nia yake ya kuleta maendeleo ya viwanda chini ya uongozi wa Rais Magufuli. Tanzania ina uwezekano mkubwa wa kuwa na maendeleo, hii ni nchi nzuri iliyojaa matumaini.




*Jukwaa la Ushirikiano wa Cbhina na Afrika (FOCAC) lililoanzishwa mwaka 2000, limekuwa taasisi muhimu ya ushirikiano kati ya China na nchi za Afrika.*

TOLEO MAALUMU

## TOLEO MAALUM LA MAADHIMISHO YA MIAKA 70 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA

1949 – 2019



# MIONGO SABA YA MAENDELEO KWA WATU: MFANO WA CHINA

***Salaam za Mbelwa Kairuki, Balozi wa Tanzania nchini China***

OKTOBA 1, 2019 ni kumbukumbu ya miaka 70 ya kuundwa kwa Jamhuri ya Jamhuri ya Watu wa China. Umri huu hauifanyi nchi ya China kuwa ya pekee, isipokuwa ni namna China ya kisasa ilivyoweza kufikia maendeleo makubwa katika kipindi kifupi.

Lakini pia nchi ya China kufikia hadhi ya kuwa Taifa kubwa na lenye nguvu dunia ni ni moja ya jambo linaloishangaza dunia mpaka leo.

Katika kipindi hicho chote, China ilijipambanua kwa namna mbalimbali ili kufikia maendeleo yakeHata hivyo maendeleo ya nchi ya China yameelekezwa kwa watu na yanalenga kukidhi matakwa ya watu kwa maisha bora.

Aidha, wakati wa kujenga uchumi dhabiti kipindi hicho , nchi ya China pia imezingatia maendeleo ya usawa katika nyanja zote.

Katika safari yake ya miongo saba, nchi ya China imejikita katika kujifunza kubadilishana na kuheshimiana na nchi zingine.

Kupitia mifumo mbali mbali ya kikanda na kimataifa, pamoja na Utaratibu wa Ukanda wa Barabara(the Belt and Road Initiative),Jukwaa la pamoja kuhusu mahusiano ya China na nchi za afrika (Forum on China-Africa Cooperation).

Aidha uzoefu kipindi chote hicho, nchi ya China imekuwa mstari wa mbele kuzishirikisha, kujifunza na kupata uzoefu kutoka kwa nchi mbalimbali duniani.

Sera yake ya kuunda ushirikiano wa kiuchumi ulio sawa (win-win) bila ubaguzi kwa nchi nyingine ni moja nguzo kuu zilioifanya nhci hiyo kufikia hatua kubwa waliyo nayo sasa.



**Mageuzi na sera ya uwazi**

Miaka 41 iliyopita, nchi ya China ilijikita kubeba sera yake ya mageuzi ya kiuchumi na kufungua ambayo imeleta sifa kubwa ya kuleta muujiza kwenye uchumi ya taifa hilo iliyoifanya Taifa hilo kuwa la pili Dunia.

Kasi na kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi ya China tangu kupitishwa kwa mkakati huo wa mageuzi na kufungua milango ya kiuchumi ya mifano na historia ya maedneleo katika karne iliyopita.

Wakati Deng Xiaoping, baba wa sera ya mageuzi na ufunguzi wa China, alipoanza harakati za kukuza uchumi, kiwango cha umaskini nchini China kilikuwa kikubwa kuliko nchi nyingi kwenye bara la Afrika.

Wakati pato la nchi ya china likiwa dola 156 mwaka 1978, miaka arobaini iliyofuata, na kwa ushawishi wa sera ya mageuzi, pato lake lilikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia 9.5 kwa mwaka kufikia dola 8,827 za kimarekani sawa na asilimia 86 ya wastani wa pato la ulimwengu mnamo 2017.

Kimsingi, kiasi kikubwa, ukuaji huu wa haraka uliinua zaidi ya watu milioni 700 kutoka nchi ya china pekee na kupunguza viwango vya umaskini kutoka asilimia 90 mnamo 1981 hadi chini ya asilimia 2 chini ya miongo minne.

Tangu 1978, sera ya mageuzi na ufunguzi wa China iliporuhusiwa imeongeza uwekezaji wa wa moja kwa moja wa nje katika sekta zenye tija na viwandani ambazo zimeonekana kuwa njia muhimu ya kuharakisha maendeleo kwa miundo miundo mbalimbali ikiwemo ya afya kote nchini

Ni ukweli usiopingika kwamba maendeleo ya nchi ya china iliyokuwa na idadi ya moja ya tano ya watu dunia yalikuwa na madhara chanya kwa nchi nyingine duniani.

Mageuzi katika sera yake yalilenga kurahisisha chakato wa uetkelezaji wa sera hiyo ha hivyo kuboresha mahusiano wenye nguvu kati ya nchi ya china na nyingine duniani.

Uwezo wa nchi ya China uliisaidia nchi hiyo kuwa na uwezo mkubwa wa ushawishi kiuchumi uliopelekea ukuaji wa uchumi wa ulimwengu ikiwemo ongezeko la uagizaji wa bidhaa na vifaa vya kusindika na visivyosindikwa.

Uwezo huu haukuwa tu na athari katika kuongeza uwezo wa usafirishaji wa washirika wake wa kimataifa, haswa nchi tajiri za Kiafrika, mahitaji yaliyoongezeka ambayo yaliongeza bei ya bidhaa hizi na kuongeza pato kwa nchi wasafirishaji.

Zaidi ya hayo, usafirishaji wa vifaa vya gharama nafuu ulitoa fursa mpya za matumizi kwa watumiaji ulimwenguni, haswa katika nchi za Afrika, ambapo utumiaji wa bidhaa za bei nafuu bila shaka umebadilisha maisha kuwa bora.

**Ushirikiano wa China na Afrika**

Tangu kuanzishwa kwa Mkutano wa Ushirikiano wa Uchina na Afrika, Afrika imefaidika na 'China Flying geese'.China imekuwa mshirika mkubwa zaidi wa biashara kwa Bara hilo kwa miaka 9 mfululizo.

Mpaka leo, theluthi mbili ya uwekezaji wa China katika bara hilo uko katika miundombinu kama ya barabara. Uwekezaji na misaada ya Wachina katika bara hilo sio tu kubadilisha uso wake na maboresho yanayoonekana katika miundombinu, pia inaangazia na kuboresha umoja na maendeleo ya bara hilo.

Miongo ishirini iliyopita, njia za kawaida za kusafiri kati ya miji barani Afrika zilikuwa ndefu na barabara mbovu ambazo ziliathiriwa kwa urahisi na mvua na mafuriko.

Hata hivyo, kwa sasa barabara kuu zilizotengenezwa mpya na treni zenye kasi kubwa zinaunganisha miji na nchi kote barani afrika, huku zikipunguza muda wa kusafiri, gharama na kuunganisha biashara.

Wakati huo huo, uwekezaji katika uzalishaji wa nishati jadidifu bei nafuu na endelevu za nishati kwa ueendelevu wa mazingira. sambamba na usalama na utulivu wa kisiasa,bara la afrika lineguzwa mojawapo ya sehemu katika ulimwengu inayovutia kwa uwekezaji.

Wakati nchi nyingi zinazoendelea barani Afrika zinaangalia China kwa mshangao juu ya maendeleo yaliyofikiwa kwa muda mfupi,swali na msingi linalojitokeza mara kwa mara ni jinsi gani nchi hiyo iliamua hatima yake.

Ingawa maendeleo ya Uchina yanaweza kuhusishwa na sababu nyingi zinazoingiliana ikiwemo uwekezaji muhimu katika huduma za afya na elimu tangu mwanzo wa ajenda yake ya mageuzi ni moja maoni yangu yaliyopelekea matokeo makubwa yaliyoshuhudiwa leo.

Wakati China ilipokuwa na uwezo wa kutoa mapato makubwa kupitia kuvutia na kushiriki katika biashara ulimwengu, kuboreka kwa maisha ya watu wake na ongezekeo ya idadi ya watu wake

Uwekezaji wa elimu kwa watu wa Taifa hilo nayo ilikuwa muhimu sana katika kufanikiwa kwa sera ya mageuzi ambayo ilisababisha ukuaji w auchumi lenye kubwa idadi ya watu inayokaribia mataifa 54 barani afrika.

**Urafiki wa China na Tanzania**

Mwaka huu ni muhimu kwa China na Tanzania. Tunaposherehekea miaka 70 ya kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa Uchina, tunasherehekea pia miaka 55 ya uhusiano wa kidiplomasia wa nchi hizi mbili .

Kuna mengi ya kujivunia kuhusu uhusiano huu wa kipekee, shukrani kwa Mwenyekiti na baba mwanzilishi Comrade Mao Tsetung na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kizazi kilichofuata cha viongozi kimeendelea kukuza mahusiano haya hadi leo tunaposhuhudia uhusiano wetu unakua siku hadi siku ya Uongozi wa Rais Xi Jinping na Rais Dkt John Joseph Pombe Magufuli.

Kwa upande wa kiuchumi na kijamii. China imekuwa mshirika mkubwa zaidi wa biashara kwa Tanzania kwa miaka 3 mfululizo. Mnamo mwaka wa 2018, biashara yetu ya pande mbili ilifikia bilioni 4

Uhusiano wetu umeendelea kukua siku kwa siku. Tanzania inajivunia kuungana na Uchina kurejeshwa katika kiti chake halali katika Umoja wa Mataifa na Mkutano Mkuu wa 26 wa Umoja wa Mataifa mnamo 1971.

Haikushangaza, kwamba kama sehemu ya kusherehekea miaka 70 ya kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa Uchina, heshima yake Rais Xi Jinping alitoa Amri ya Rais ya kukabidhi medali ya Urafiki kwa mtoto wa mchanga wa Tanzania, waziri mstaafu , Dk. Salim Ahmed Salim.

Wakati huohuo, watanzania hawatasahau jinsi China ilivyosaidia nchi yetu kutoa mafunzo kwa wapigania uhuru na jinsi ilivyotoa msaada mkubwa wa kifedha na kiteknolojia kwa harakati za ukombozi wa kitaifa katika nchi za Kusini mwa Afrika.

Reli ya Tanzania-Zambia (TAZARA) bado ni moja wapo ya miradi mikubwa ya misaada ya nje kutoka nchi ya Kichina barani Afrika na ishara ya ushirikiano wa China na Afrika.

Ndio sababu mnamo 1965, licha ya shinikizo kubwa la nje, Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza katika Afrika Mashariki na Kusini, kusaini Mkataba wa Urafiki na Uchina.

Aidha, msimamo wa sera ya nje ya Tanzania dhidi ya uchina ilidhihirishwa wazi mwaka 2013, wakati Rais wa China Xi Jinping alipofanya safari ziara yake ya kikazi barani afrika na kuichagua Tanzania kama nchi yake. Mahusiano yetu sio dola za kisiasa za Amerika tu. Kwa kuongezea, nchi ya nchina ndiye mwekezaji mkubwa zaidi wa nje nchini Tanzania na uwekezaji wake unafikia jumla ya za kamrekani dola bilioni 7 na miradi zaidi ya 700 ya uwekezaji, ambayo imeunda ajira za moja kwa moja zipatazo 150,000.

Kupitia sera ya kubadilisha watu katika nyanja kumeimarisha maisha nchi mbili.Ziadi ya watanzania 5,000 hivi sasa wanasoma nchini China na zaidi ya watalii 30,000 wa China walitembelea Tanzania mwaka jana. Huu ndio mfano bora wa ushirikiano wa kushinda kwa usawa (win-win).

Liliko kubwa zaidi ni kwa Rais Dkt John Pombe Magufuli kukuza na kuongeza uhusiano huu kwa urefu zaidi. Chini ya uongozi wake, takwimu juu ya biashara ya China, uwekezaji na utalii nchini Tanzania zimeongezeka sana.

Ni imani yake kwamba China inayoendelea kukua italeta matarajio pana kwa nchi zetu mbili kushirikiana katika kuzaa matunda na kutoa faida zaidi kwa watu wa nchi zetu mbili na zaidi.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ipokeeni tena fursa hii ya kusamehewa

TUNAMPONGEZA Rais John Magufuli, kwa kupendekeza utaratibu wa washtakiwa wa makosa ya uhujumu uchumi kukiri makosa, kuomba msamaha na kurudisha fedha na mali wanazomiliki, wakiamini kuwa zina walakini.

Tunaipongeza hatua ya Rais ya kuwa kiongozi pekee aliyeibua utaratibu huo, hapa nchini na kuanza kutekeleza jukumu hilo ambalo tunaona kuwa lina tija kwa nchi na wahusika.

Kadhalika, tunawapongeza wahusika takribani 460 walioitikia wito wa kuomba msamaha na kuahidi kurudisha fedha hizo na kukubali kusamehewa na Rais.

Aidha, tunaungana na maelezo ya Rais kuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), imefanya kazi kubwa ya kuwapokea, kuwasikiliana na wahusika kuwasikiliza na kupitia nyaraka zao na kwa moyo wameamua kuomba msamaha na kurejesha kile walichoamini kuwa kilistahili kuwa mikononi mwa serikali.

Tumpongeze Rais kuonyesha moyo wa upendo, huruma na kuthamini utu wa watu hao, ambao hata kama pengine walikuwa na hofu kuwa wametegwa amewaahidi kuwa amewasamehe na hiyo ni kweli na ni haki yao.

Ikumbukwe kuwa kuwasamehe wahusika kunamaanisha mambo mengi si kwa mshtakiwa mwenyewe lakini pia, familia yake na taifa ambalo lilikuwa linawahudumia wakiwa mahabusu magerezani.

Wale ambao bado wanatafakari wakumbuke kuwa msamaha huo ni dawa kwao hasa kwa kuwa wamekaa muda mwingi gerezani na baada ya kuendelea kujichunguza na kuona kuwa wana stahili kungama wafanye hivyo.

Tunaomba umma ufahamu kuwa kuingia gerezani ama kufikishwa mahakamani si jambo la mtu mmoja kila binadamu ana hatia ambayo inaweza kumfikisha mahakamani pamoja na jela.

Ni vizuri familia na jamaa za wahusika zikawashauri kwa weledi kama kuna uwezekano wa kunufaika na msamaha huo wafanye hivyo wasipoteze wakati.

Tunasema hivi hakuna cha kuhofia kwa sababu kila mtu ni mfungwa au mshtakiwa mtarajiwa.

Tena tukumbuke kuwa kinachowatofautisha walio uraiani na magerezani ni kwamba ambao hawajashtakiwa ni kwa sababu hawajakamatwa kutokana na hatia zao, lakini nao pia wana sababu na sifa zote za kuwafanya kufikishwa mahakamani na magerezani.

Wahusika wakumbuke kuwa kupata msamaha baada ya kuomba radhi na kurejesha mali pamoja na kuondoka gerezani ni jambo la kuwafariji na kuwapa ushujaa wa kukiri kuwa walikosea na wakaomba msamaha ili wakaanze upya maisha yao.

Tunawashauri wahusika wajitie moyo wa ushujaa na kuachana na mambo ya zamani wakumbuke kuwa kupata msamaha nako ni fursa ya kujenga upya kuleta mabadiliko katika maisha yao.

Wafahamu kuwa kila binadamu anapitia kwenye mambo mengi ambayo yanamkuza kutoka hatua moja kwenda jingine na hilo wanalolipitia ni kama darasa.

Waombe radhi na waichukulie hali hiyo kuwa ni nafasi nyingine ya kujifunza kuhusu harakati za maisha, kujikwaa, kuanguka lakini pia kusimama tena.

Wahusika wafahamu kuwa nia ya serikali ni njema na imelenga pia watu wengine wajifunze na wawe tayari kubadilisha mienendo yao hasa katika uadilifu na ulinzi wa mali za umma.

Tunaamini kuwa msamaha wa Rais hautapita na kusahaulika bali utaacha alama za kujitizama upya kama taifa, kubadilika na kutumia fursa hiyo kama njia ya kutafakari njia na mienendo yetu.


Tafakari hiyo si kwa wahusika peke yao ambao wanaweza kuomba msamaha na kurudisha mali za Watanzania bali ni kwa kila mmoja.

Wengi watakubaliana nasi kuwa kukamatwa, kufikishwa mahakamani na hata kufungwa gerezani ni mambo yanayotokea katika maisha ya binadamu wote.

Tunawahimiza tena kujichunguza na kutumia fursa hiyo kuomba radhi ili kunufaika na msamaha wa Rais.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Siku ya Wazee, halmashauri ziige mfano wa Ubungo

Na Raphael Kibiriti

OKTOBA Mosi ya kila mwaka, dunia huadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wazee katika dhima nzima ya kuangalia ustawi katika umri wao wa uzee, unaombatana kwa sehemu kubwa na changamoto mbalimbali za kimaisha.

Pamoja na zingine kwa ujumla wake, changamoto zinazowakabili wazee ni pamoja na kutolipwa kwa wakati mafao yao pindi wanapostaafu.

Vilevile zipo changamoto za ukosefu wa lishe bora na kubwa zaidi kwa minajili ya safu hii leo, suala la kukosa huduma bora za afya na hivyo kuathiri ustawi wao.

Hili si kwa Tanzania tu, bali ni changamoto inayowakumba takribani wazee wote katika maeneo tofauti ya dunia.

Na ndiyo sababu ambayo kimsingi imechangia Umoja wa Mataifa (UN) kupitia majukwaa yake mbalimbali likiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO), kuja na siku hii ya kimataifa ya wazee.

Kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya wazee nchini kwa maana ya watu wenye umri wa miaka 60 na zaidi ni milioni 2.5, sawa na asilimia 5.6 ya Watanzania wote takribani milioni 55 kwa hivi sasa.

Kwa mwaka huu, maadhimisho ya siku hii yanafanyika Manispaa ya Mtwara katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara, ambapo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Kauli mbiu ya mwaka huu kwa maadhimisho haya ni 'Tuimarishe Usawa Kuelekea Maisha ya Uzeeni' ikikusudia kuihimiza serikali na kwa maana hiyo nchi wanachama wa UN, kuweka mipango na mikakati ya kupunguza tofauti za watu katika jamii.

Si hilo tu, pia kutoa fursa kwa makundi maalumu likiwamo la wazee kufaidika na fursa zilizopo na maendeleo yaliyofikiwa katika nchi husika.

Kimsingi Muungwana anakiri kwamba serikali inaendelea na jitihada za kujenga uelewa kwa jamii juu ya changamoto zinazolikabili kundi hili na husussani katika eneo la kuhakikisha wazee wanapata huduma bora za afya.

Inachukua hatua za kuwabaini wazee wote kuanzia ngazi ya kitongoji, kijiji, mtaa, kata, wilaya, mkoa hadi ngazi ya taifa.

Aidha, inachukua hatua za kuhamasisha kuundwa kwa mabaraza ya wazee kuanzia ngazi ya kijiji au mtaa, hadi ya taifa, kuwapatia vitambulisho vitakavyowawezesha kupata huduma za matibabu bila ya kulazimika kuzilipia.

Serikali iko pia katika mpango wa kuhakikisha wanapata Bima ya Afya ili waondokane na kero wanazokumbana nazo wanapohitaji huduma za afya.

> **Serikali iko pia katika mpango wa kuhakikisha wanapata Bima ya Afya ili waondokane na kero wanazokumbana nazo wanapohitaji huduma za afya.**

Pamoja na kwamba hatua hizi chanya bado hazijaenea katika maeneo yote nchini, Muungwana ana ushuhuda wa baadhi ya halmashauri ambazo zimeweza kimsingi kutimiza wajibu wa kuliangalia kundi hili katika eneo la afya.

Mojawapo ya halmashauri hizo ni ya Manispaa ya Ubungo, Wilaya ya Ubungo jijini Dar es Salaam.

Wazee katika manispaa hii walau wanatibiwa bure katika ngazi ya zahanati na vituo vya afya ambako Muungwana amefanya utafiti wake mdogo.

Kwamba halmashauri hii imeweza kutoa huduma kwa wazee bila ya kuwatoza fedha katika zahanati na vituo vyake vya afya, hatua ambayo ni ya kupigiwa mfano.

Sasa wakati leo dunia inaadhimisha Siku ya Wazee Kimataifa, Muungwana anaona wakati umefika kwa halmashauri zote nchini kuwezesha hili la kutoa huduma bora za afya kwa wazee walio katika maeneo yao bila malipo.

Ninasema hivyo kwa sababu kuna halmashauri ambazo zimeweza kufanya hili kwa ufanisi, kama hiyo ya Ubungo inayotolewa mfano.

Msingi wa msisitizo huo umejikita vilevile katika ukweli kwamba UN imepitisha Azimio la kisiasa kuwahi kufikiwa linalochochea afya kwa wote ifikapo mwaka 2030.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Dk. Tedros Ghebreyesus, azimio hilo linahimiza dunia ambamo kwao afya si gharama bali ni uwekezaji.

Dunia ambamo afya inachagiza maendeleo endelevu, ambayo kila mtu wakiwamo wazee atafurahia apaswavyo kuwa nayo.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, akikabidhi zawadi kwa mshindi wa shindano la michoro ya alama za usalama barabarani kutoka Shule ya Msingi Kibamba, Emmanuel Massawe, linaloendeshwa na Taasisi ya Amend kwa udhamini wa kampuni ya Puma Energy Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi kigogo Nida yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imepiga kalenda kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi Mkuu wa zamani wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), Dickson Maimu na wenzake baada ya upande wa Jamhuri kudai upelelezi haujakamilika.

Maimu na wenzake wanakabiliwa na mashtaka 100 ya uhujumu uchumi ikiwamo kusababisha hasara ya Sh. bilioni 1.16 kwa serikali. Kesi hiyo ilitajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai, alidai upelelezi haujakamilika, hivyo aliomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Pamoja na maombi hayo, upande wa utetezi ulidai kuwa unaomba ruhusa kwa mshtakiwa Sabina Raymond ya kusafiri kwenda mkoani Morogoro kwa masuala ya kifamilia.

Hakimu Ally alisema kesi hiyo itatajwa Oktoba 15, mwaka huu, pia mahakama yake ilikubali maombi ya mshtakiwa Raymond kusafiri kwenda Morogoro.

Kesi hiyo ilifikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza Agosti 18, 2017. Mbali ya Maimu, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Meneja Biashara wa Nida, Avelin Momburi na Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama), Joseph Makani. Wengine ni Kaimu Mhasibu Mkuu wa Nida, Benjamin Mwakatumbula; Mkurugenzi wa Kampuni ya Aste Insurance Brokers, Astery Ndege; Ofisa Usafirishaji, George Ntalima, Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond na Xavery Kayombo.

Katika kesi hiyo, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya kutumia madaraka vibaya, kula njama, kutumia nyaraka za uongo kumdanganya mwajiri na kuisababishia serikali hasara ya Sh. 1,169,352,931.

Inadaiwa kwenye shtaka la kwanza, Maimu na Mwakatumbula kati ya Januari 15 hadi 19, 2010 katika makao makuu ya Nida, Kinondoni jijini Dar es Salaam, wakiwa watumishi wa umma kwa nafasi walizokuwa nazo, walitumia madaraka vibaya.

Wanadaiwa kuwa waliidhinisha malipo kwa Gotham International Limited (GIL) ya Dola za Marekani 2,700,00 bila kutumia viwango vya kubadilisha fedha za kigeni vilivyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania, kinyume na kifungu 19.3 cha mkataba kati ya Nida na GIL, hivyo kuifanya GIL kupata faida ya Sh. 3,969,000.

Maimu na Mwakatumbula katika shtaka lingine, wanadaiwa kati ya Juni 3 na 5, 2013 katika makao makuu hayo walitumia madaraka vibaya kwa kuidhinisha malipo kwa GIL ya Dola za Marekani milioni 1.8 bila kuzingatia viwango vya kubadilisha fedha, hivyo kuifanya GIL kupata faida ya Sh. 106,346,000.

Washtakiwa hao wawili wanadaiwa Juni 20, 2014 katika makao makuu hayo, waliidhinisha tena malipo ya Dola za Marekani 675,000 kwa GIL bila kuzingatia viwango vya kubadilisha fedha, hivyo kuifanya kampuni hiyo kupata faida ya Sh. 42,471,000.

Maimu na Mwakatumbula wanadaiwa kutumia madaraka yao vibaya kwa kupitisha malipo mengine ya Sh. milioni sita kwa GIL bila ya kupiga hesabu kwa kutumia viwango vya kubadilishia fedha hivyo kuifanya kampuni hiyo kupata faida ya Sh. 14, 661,676.76.

Wawili hao pia wanadaiwa kati ya Januari 15, 2010 na Mei 16, 2015 katika makao makuu ya Nida, kwa kuidhinisha malipo kwa GIL ya Dola za Marekani bila kuzingatia viwango vya kubadilisha fedha za kigeni, waliisababishia Nida hasara ya Sh. 167,445,676.76.

# Polisi wapigwa mkwara kamata wachimbaji wadogo

**Na Alphonce Kabilondo, GEITA**

NAIBU Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo, amewaonya askari polisi nchini kuwakamata wachimbaji wadogo na wanaopeleka madini yao kuuza kwenye masoko ya madini.

Kadhalika ameliitaka jeshi hilo kuwakamata wanaokwepa kwenda kuuza madini yao kwenye masoko ya madini.

Naibu Waziri Nyongo alitoa kauli hiyo jana, wakati akijibu malalamiko ya wabunge wa mkoani Geita wakati wa hafla ya kufunga maonyesho ya pili ya teknolojia ya uwekezaji sekta ya madini.

Nyongo alisema askari wa jeshi hilo waache kutumia fursa hiyo kuwakamata wachimbaji wadogo wanaopeleka kuuza madini yao kwenye masoko, badala yake wawakamate wanaokwepa kwenda kuuza madini yao kwenye masoko.

Kuhusu maeneo ya uchimbaji wa madini, alisema serikali ikikamilisha utaratibu maeneo hayo yataainishwa.

Acheni kuwakamata wachimbaji wadogo wanaopeleka kuuza madini yao kwenye masoko, wakamateni wanaokwepa kuuza madini," alisema Waziri Nyongo. Awali Mbunge wa Busanda, Lorensia Bukwimba, alilalamikia kitendo cha baadhi ya askari polisi mkoani Geita kuwakamata wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu wanapokuwa wanapeleka dhahabu kwenye masoko ya kuuzia kisha kuwatuhumu kwa uhujumu uchumi.

Bukwimba alitoa kilio hicho kwa Waziri wa Madini, Dotto Biteko, wakati wa kufunga maonyesho ya pili ya teknolojia bora ya uwekezaji sekta ya madini. Biteko alimwakilisha Makamu wa Rais, Samia Hassan Suluhu.

Alisema kuwa baadhi ya askari polisi wamekuwa wakiwakamata wachimbaji wadogo wakiwa katika harakati za kusafirisha madini yao kupeleka kwenye masoko ya kuuza kisha kuwatuhumu kwa kesi za uhujumu uchumi na kusema kuwa hali hiyo ni sawa na kuwanyanyasa wachimbaji.

# Kongamano kujadili mafuta na gesi Dar

**Na Enock Charles**

KATIKA kutekeleza Sera ya Serikali ya Tanzania ya Viwanda, wataalamu wa kimataifa wa mafuta na gesi (CWC), wameandaa kongamano la kimkakati la ushirikiano wa kibiashara katika sekta ya nishati ya mafuta na gesi.

Kongamano hilo litawaleta pamoja wawekezaji na wadau wengine muhimu katika sekta hiyo.

Kongamano hilo linalotarajiwa kushirikisha nchi 67 duniani, litachambua umuhimu wa kimkakati na nafasi ya Tanzania kama kitovu cha Afrika Mashariki katika uendelezaji wa miradi mikubwa katika sekta ya nishati pamoja na kujifunza namna ya kufanya makubaliano ya kibiashara baina ya kampuni za kimataifa na zilizopo nchini. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watoa huduma katika sekta ya mafuta na gesi Tanzania, Abdulsamad Abdulrahim, alisema lengo la kongamano hilo ni kuimarisha ushirikiano wa kibiashara baina ya wenyeji na wageni na kukuza sekta ya mafuta na gesi nchini.

"Washiriki na wadau wa kongamano watatumia nafasi hiyo kutengeneza fursa mbalimbali za kibiashara na mazingira ya ushirikiano yatakayowezesha sekta ya nishati kusonga mbele," Abdulrahim alisema.

Viongozi wanaotarajiwa kushiriki katika kongamano hilo ni Rais mstaafu, Ali Hassan Mwinyi, Makamu wa Rais mstaafu, Dk. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais Biashara Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Ulaya, Maarten Garvelink, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki na Waziri wa Uchumi, Uwekezaji, Nishati, Uunganishaji wa Uchumi, Utalii na Msemaji wa Serikali ya Komoro.

Baadhi ya nchi zinazotarajiwa kushiriki kongamano hilo zikiongozwa na mtoa mada kutoka Ausrtralia ni Uganda, Uholanzi, Comoro,

Kenya, Msumbiji, Norway, Ufaransa, Uingereza, Tunisia, Afrika Kusini, Canada, Marekani, India, Dubai, Uturuki na Nigeria.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

TANGAZO MAALUM KWA WASTAAFU WOTE

NDUGU WATANZANIA SIKU ZA HIVI KARIBUNI KUMEKUWA NA MATUKIO YA UTAPELI YAKIHUSISHA BAADHI YA WASTAAFU KUPIGIWA SIMU NA WATU WANAOJITAMBULISHA KUWA NI WATUMISHI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO WAKIOMBA TAARIFA ZAO ZA KUSTAAFU NA WAKATI MWINGINE KUOMBA FEDHA KWA AJILI YA KUSHUGHULIKIA MAFAO YA KUSTAAFU.

TUNAUARIFU UMMA KUWA HUDUMA HIZI ZINATOLEWA BURE IKUMBUKWE KUWA TAARIFA ZA MSTAAFU HUWASILISHWA WIZARANI NA ALIYEKUWA MWAJIRI WA MSTAAFU NA SIYO MSTAAFU MWENYEWE.

MWANANCHI USIKUBALI KUDANGANYWA NA MATAPELI HAWA AU KUTOA RUSHWA KWA AJILI YA HAKI YAKO.

*ASANTENI*

TANGAZO LIMETOLEWA NA:

KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

215439401

## HABARI KITAIFA



Ofisa Mtendaji Mkuu wa ALAF Ltd, Dipti Mohanty (wa tatu kushoto) na Wakala wa Usambazaji wa Bidhaa za kampuni hiyo, Abdalaah Scabascuba, wakikata utepe kuzindua duka la vifaa vya ujenzi la ALAF, katika eneo la Feri Kigamboni, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Rasilimali Watu wa kampuni hiyo, Petro Kapembwa na Mkuu wa Masoko na Mauzo, Anurag Mishra. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto 20 wapatiwa msaada wa matibabu

**Na Mary Geofrey**

WATOTO 20 wenye matatizo ya moyo ambao wanahitaji kufanyiwa upasuaji katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), wamepatiwa msaada wa matibabu.

Msaada wa Sh. milioni 40, umetolewa na Kampuni ya Mafuta ya Puma Energy kwa ajili ya kuwezesha upasuaji kwa watoto hao kati ya 500 wanaohitaji msaada huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo, Dominic Dhanah, alisema jana kuwa wametoa fedha hizo kuunga mkono jitihada za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, katika kuwasaidia watoto hao.

Alisema kampuni yake siku zote iko tayari kushirikiana na serikali katika masuala ya kijamii ndiyo maana imeona kuna haja ya kushiriki kuwasaidia ili kupata matibabu yanayohitajika. "Sisi tunafanya biashara, lakini jamii inayotuzunguka tunaipa kipaumbele ndiyo maana siku zote tuko tayari kushiriki na kusaidia shughuli mbalimbali na hawa watoto tumeona tuna wajibu wa kushiriki kuokoa maisha yao," Dhanah alisema.

Makonda kwa upande wake mbali na kuishukuru Puma kwa msaada huo, alisema mwanzoni mwa mwezi huu ataunda kamati ya kutafuta Sh. bilioni moja ambazo zitafanikisha upasuaji wa watoto wote 500.

"Nataka kufikia Desemba watoto hawa wawe wamefanyiwa upasuaji na kupata matumaini ya kuuona mwaka mpya wakiwa na matumaini ya kuishi," Makonda alisema.

Sambamba na hilo, Makonda aliipongeza kampuni hiyo kwa kuratibu mafunzo ya usalama barabarani kwa wanafunzi wa shule za msingi na kueleza kuwa imesaidia kupunguza vifo vinavyotokana na ajali kwa kundi hilo.

"Kwa miaka sita ambayo Puma imetoa mafunzo haya kwa watoto tunaona vifo vinapungua. Mwaka huu amefariki dunia mtoto mmoja tu na wengine wanne kujeruhiwa. Takwimu hizi zinaonyesha ni kiasi gani watoto wanaelewa matumizi sahihi ya barabara na niwaombe watu wazima hasa waendesha bodaboda mwendelee kuwasaidia ili wawe salama," Makonda alisema.

DI & PC
TANZANIA

SALES AND MARKETING

We are currently looking for a talented individual with the relevant skills and experience for a position in **Field Sales,** which is based in Dodoma. The successful candidate will report directly to the Regional Sales Manager.

The key purpose of the role is to manage route to market and KPLs.

The duties and responsibility support regional distribution strategy.

- Link up with Distribution Manager to ensure distribution strategy and plans are understood for execution.
- Schedule calls approved by the RTM Manager.
- Manage retail recommended prices in different territories.
- Ensure compliance to qualified standards and manage trade replacements.
- Attend frequent trade visits to customers' stores.
- Understand pack margin and pack role per customer in order to optimize revenue growth.

**Qualifications.**
The candidates should have a bachelor's degree.
Experience of 2 years in Sales **(Preferably with FMCG)**
The candidate should have excellent commercial/industrial awareness, interpersonal and motivational skills.
Application deadline **14.10.2019**

**Dodoma Innovation and Production Company Ltd.**
**HR Manager**
**P.O. Box 1888**
**Dodoma**
**info@asante-dipc.com**
**+255 737 707 522**

215439802

# Mbowe abadili mada kuwakwepa polisi

INATOKA UK 2

watu wengine. Lakini pili wanapaswa kupata taarifa ya kile kinachoendelea katika mkutano ambao ina mashaka nao, hasa kutokana na desturi yao waliyojiwekea wenyewe.

"Kwa hiyo tumepeleka polisi na wako ndani ya hiki kikao kwa kuwa ni mkutano wa chama cha siasa na si 'send off' (sherehe ya kumuaga binti kabla ya kuolewa) wala harusi na kama mijadala yao haina shida yoyote, basi polisi watasikia."

Alisema hata katika mkutano mingine ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), polisi wanakuwa ndani kwa hiyo hawana haja ya kuhofia kwa kuwa polisi wapo kwa ajili ya usalama.

Kwa mujibu wa Sabaya, lengo la polisi ni kuhakikisha wale watu walioko pale wako salama, lakini hawawasababishii wengine uvunjifu wa amani ndiyo maana wamewaagiza wakae pale kuhakikisha usalama wao.

Baadaye, Katibu wa Chadema Mkoa wa Kilimanjaro, Basil Lema, akizungumzia tukio hilo, alisema haelewi ni kwa nini polisi wanavamia mkutano wao wakati ni wa ndani.

Awali, kulikuwa na taarifa kwamba katika mkutano huo, Chadema walipanga kujadili pamoja na mambo mengine, uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu.

# Mabilioni uhujumu uchumi

INATOKA UK 2

mtu mwenye mamlaka ya kufuta kesi yoyote ni DPP wala siyo mtu yeyote, pamoja na mahakama inayotoa hukumu."

**DPP AMWAGIWA SIFA**

Rais Magufuli alisema wamekuwa wakishuhudia na kusikia jinsi ofisi hiyo ikifanya kazi vizuri hasa katika kesi na mashauri mbalimbali na mara nyingi serikali imekuwa ikishinda kwa sababu ya uwakilishi mzuri kwa niaba ya Watanzania.

"Tumeshuhudia madini yakitaifishwa, na hii inadhihirisha ni namna gani ofisi yako inafanya kazi kubwa katika kutetea serikali na rasilimali za Watanzania."

"Ninawaomba mwendelee hivyo, ninawapongeza PCCB (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ambao nao wamekuwa wakishiriki kwenye kesi, Jeshi la Polisi kupitia kitengo cha upelelezi, endeleeni kushikamana kwa pamoja."

Pia Rais Magufuli aliwashukuru watendaji wa mahakama katika kutoa uamuzi kulingana na sheria zinazowaongoza.

Awali Mganga akiwasilisha mbele ya Rais Magufuli taarifa za watuhumiwa hao, alimweleza kuwa katika kipindi cha siku saba alichokitoa kilichoishia Jumamosi, ofisi yake imepokea barua za washtakiwa 467 wakiomba kukiri makosa yao na kurejesha fedha walizowaibia Watanzania.

"Barua hizi zimeendelea kuja, mpaka jana (juzi) bado zilikuwa zinakuja kwa sababu nyingine zimechelewa kutoka mikoani kuja ofisi yangu. Kati ya washtakiwa hao, Sh. bilioni 7.9 zinatarajiwa kurudishwa wakati wowote kuanzia sasa."

Mganga alisema kwa washtakiwa wengine fedha zinazotarajiwa kurudishwa ni Sh. bilioni 5.7.

"Katika kundi hilo, wako ambao tayari wanataka kurudisha moja kwa moja bila kulipa kwa awamu, ambazo ni Sh. bilioni 13.6. Kundi la pili ni la watu ambao wanataka kulipa kwa awamu jumla yake ni Sh. bilioni 94.2.

"Ukijumlisha washtakiwa wote 467, jumla ya fedha ambazo washtakiwa wapo tayari kurudisha ni Sh. 107.8."

Alisema Ijumaa iliyopita mtu aliyekuwa akidaiwa Dola za Marekani 450,000 aliitikia wito huo wa Rais Magufuli na kuamua kukiri kosa lake mahakamani na kuzilipa fedha hizo moja kwa moja kwa aliyekuwa akimdai na faini ya Sh. bilioni tano.

"Ijumaa hiyo hiyo kuna mtu alikuwa na gramu 2123.64 za madini vito vyenye thamani Dola za Marekani 15876.66 ambaye naye alikiri makosa na kulipa fedha hizo na madini hayo kutaifishwa.

"Katika zoezi hili kati ya wanaokubali kulipa na kurejesha mali kuna gramu 33.2 za dhahabu na kilo 18 za madini aina ya Tanzanite zilizokamatwa Arusha na tukijumlisha na kilo 35 za madini vito, watuhumiwa wapo tayari kuzirudisha."

"Tunalazimika kuyasoma majalada, kuyachambua vizuri na kuyapitia kwa kina ili kuona ni maeneo yapi ambayo tunaweza kukubaliana nayo na yapi hatukubaliani nayo na kurekebisha aina ya mashtaka na kwenda nayo mahakamani kwa mujibu wa sheria ili kesho na kesho kutwa wasije wakatumia mbinu nyingine kuishtaki serikali," alisema.

# Wasiojulikana wachoma nguzo 60 za umeme

**Na Said Hamdani, LINDI**

SERIKALI imeendelea kukemea vitendo vya uharibifu wa mazingira, ukiwamo uchomaji moto misitu unaofanywa na baadhi ya jamii kwa kuwa wamekuwa wakisababisha kuharibu miundombinu inayotekelezwa na serikali.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, wakati wa mkutano wa mashauriano kati ya wawekezaji, serikali na wafanyabiashara, uliofanyika Manispaa ya Lindi.

Mgalu alionyesha masikitiko hayo kufuatia watu wasiofahamika kuunguza nguzo 60 za umeme eneo la Kata na Tarafa ya Pandeilaya, Kilwa mkoani Lindi.

Hata hivyo, Mgalu hakubainisha hasara iliyopatikana kufuatia uharibifu huo.

Mgalu alisema: "Hivi sasa nipo hapa mkutanoni napokea ujumbe kwamba kuna nguzo 60 za umeme zimechomwa moto huko Pande."

Mgalu amesema kutokana na uharibifu huo, zinahitajika zaidi ya Sh. milioni 30 kuirejesha hali hiyo, na kuwa hali hiyo inarudisha nyuma jitihada za serikali katika kuwaondolea wananchi changamoto zinazowakabili za kukosa huduma ya umeme.

Pia aliwaomba viongozi wa Mkoa wa Lindi, wakishirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kufanya upelelezi kwa lengo la kuwabaini wahusika ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) Mkoa wa Lindi, Felician Makotta, alipoombwa kutoa ufafanuzi juu ya tukio hilo, alisema nguzo zilizoungua bado zipo chini ya mkandarasi anayemiliki Kampuni ya State Grid iliyopewa kazi ya kusambaza umeme maeneo ya vijijini.

"Ni kweli taarifa aliyoitoa Naibu Waziri wetu, lakini bado nguzo hizo zipo chini ya mkandarasi aliyepewa kazi ya kusambaza huduma hiyo maeneo ya vijijini," alisema Makotta.

Mwandishi wa Habari hizi alipowasiliana na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Charles Mlawa, alikiri kuwapo kwa tukio hilo, lakini hakutaka kutoa maelezo zaidi, badala yake alimtaka kuwasiliana na meneja wake, Bahati Manyangali aliyeko eneo la mradi.

Hata hivyo, Bahati alipotafutwa kupitia simu ya mkononi, sinu iliita muda mrefu bila kupokelewa.



Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (wa pili kulia), akiwa na Mkurugenzi wa Benki ya TADB, Japhet Justine (kushoto kwake) katika ziara ya kutembelea kiwanda cha Manawa Misungwi mkoani Mwanza. **MPIGAPICHA WETU**

# Kiwanda cha pamba Manawa kufunguliwa

**Na Mwandishi Wetu, MISUNGWI**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Bodi ya Pamba Tanzania, zimetakiwa kuangalia mahitaji ya kiwanda cha pamba cha Manawa ili kiweze kufufuliwa kutokana na kuwa na uwezo wa kuchakata takribani kilo milioni 30 za pamba.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, katika ziara yake na benki hiyo Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza iliyolenga kukutana na viongozi wa AMCOS, waataalamu wa kilimo, wanunuzi wa pamba na viongozi mbalimbali wa wilaya kwa ajili ya kujifunza juu ya uzalishaji wa pamba.

Bashe alisema TADB, Bodi ya Pamba na Nyanza Ununio wanatakiwa kutamthini hali ya kiwanda hicho ili kujua nini kinahitajika kukifufua.

"Kiwanda cha Manawa kilikuwa na uwezo wa kuchakata takribani kilo milioni 30 za pamba kutoka AMCOS za Kwimba, Misungwi na Magu, hivyo basi ufufuaji wa kiwanda kutazipa uwezo AMCOS, kuongeza uzalishaji wa pamba na kufungua milango ya masoko kwa wakulima mmoja mmoja wa zao la pamba," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema amepokea agizo hilo la Naibu Waziri huyo na kwamba TADB ingependa pia kuwekeza katika maghala ya pamba kutokana na kuwapo kwa changamoto kubwa hali inayolazimu pamba kulazwa nje ya ghala.

"Baadhi ya AMCOS wilayani Misungwi hulazimika kulaza nje pamba, huku wakisubiri wanunuzi na mwaka jana TADB iliwekeza takribani Sh. bilioni sita katika zao hili na kufanikiwa kupata matokeo mazuri," alisema.

Alifafanua kuwa Sh. bilioni nne ziliwekezwa katika viuadudu na Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya matrekta ya kilimo.

Alieleza kuwa benki hiyo inaendelea kutoa huduma mbalimbali kwa wakulima kwa lengo la kuchagiza maendeleo katika sekta ya kilimo nchini.

"Katika kufanikisha hili, Benki ya Kilimo inawahudumia wakulima wote nchini kwa kupitia matawi yake yaliyomo katika kanda tofauti ikiwamo mkoa wa Dodoma, Mwanza, Kigoma, Dar Es Salaam na hivi karibuni ofisi za kongani ya Nyanda za Juu Kusini zinafunguliwa rasmi mwezi Oktoba mwaka huu," alisema.

# Sera, sheria uwekezaji kuboreshwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki, amesema wanafanya maboresho katika sera na sheria ya uwekezaji ili kuwa na mazingira mazuri kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

Kairuki aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa kusikiliza changamoto za wafanyabiashara na wawekezaji mkoa wa Ruvuma na kuongeza kuwa mapendekezo ya mabadiliko hayo ya sheria ya uwekezaji yanatarajia kuwasilishwa bungeni mwezi Novemba, mwaka huu.

Alisema mabadiliko hayo yatasaidia kupunguza kiwango kinachotakiwa ili kujisajili Kituo cha Uwekezaji (TIC).

"Mabadiliko haya yatasaidia kuvutia uwekezaji zaidi na pia kuwezesha wawekezaji wa kada ya chini na kati kusajiliwa na TIC, utawasaidia kunufaika na vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi," alisema.

Kuhusu matamko mabaya ya viongozi na vitisho kwa wawekezaji na wafanyabiashara, alisema kwa sasa yamepungua.

"Tunaomba viongozi wenye tabia hii wakome na iwapo mfanyabiashara ama mwekezaji atapewa lugha ya vitisho na vidhibiti atoe taarifa haraka," alisema.

Naibu Waziri wa Ardhi, Angeline Mabula, alitoa wito kwa halmashauri zote kuhimiza wawekezaji wote hasa wa kigeni wanaohitaji ardhi ya uwekezaji waanzie TIC.

"Mnapopata ardhi kwa ajili ya uwekezaji msimpe mwekezaji moja kwa moja bali fuateni taratibu na sheria za kupitia TIC ili kujiepusha na migogoro inayoweza kujitokeza," alisema na kuongeza:

"Kuanzia Novemba 19, mwaka huu, wizara itafungua ofisi kila mkoa ili kurahisisha upatikanaji wa ardhi ikiwamo ya uwekezaji, upimaji na upatikanaji wa hati ngazi ya kila mkoa."

Mabula alisema hiyo itapunguza usumbufu kwa wawekezaji na wafanyabiashara kutokana na hati kupatikana mikoa jirani (Kanda) ama Dar es Salaam.

Naye Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema katika kuboresha na kuweka mazingira mazuri kwa wafanyabiashara na mwekezaji, inashauriwa wapewe miezi sita kabla ya kuanza kulipa kodi pale wanapoanza utekelezaji wa miradi yao.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mussa Sima, alitoa wito kwa wawekezaji wote kuwasiliana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc) ili kupata miongozo ya mazingira wanapotaka kutekeleza miradi yao.

# Faida za unywaji maziwa zatajwa

**Na Boniface Gideon, TANGA**

UTAFITI unaonyesha unywaji wa maziwa ni njia pekee inayoweza kusaidia mtu asizeeke na kuzuia ngozi zilizo kunjamana kwa binadamu pamoja na kuzuia tatizo la meno kuuma hadi kufikia hatua ya kung'olewa.

Akizungumza na watafiti kutoka taasisi mbalimbali zilizo chini ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na waandishi wa habari kutoka mikoa ya Tanga, Morogoro na Pwani, Nadomana Nyanga, Meneja, ndiye aliyebainisha hayo.

Alikuwa akizungumzia vyanzo vya maziwa kutoka kiwanda cha Tanga kilichopo jijini Tanga baada ya wanahabari hao, kutembelea kiwandani hapo kwa lengo la kujionea mafanikio yaliyofikiwa katika kuboresha ubora wa maziwa.

Nyanga alisema njia kuu ya kuondoa uzee na ngozi zilizokunjama kwa binadamu na kuzuia tatizo la meno kuuma hadi kufikia hatua ya kung'olewa ni pamoja na kunywa maziwa bora ambayo hayajachanganywa na maji na ng'ombe kula chakula bora chenye lishe inayotakiwa.

Nyanga alisema endapo Watanzania watajiwekea utamaduni wa kunywa maziwa, matatizo yote hayo wataepukana nayo kwa kuwa maziwa yana virutubisho vingi ambavyo huufanya mwili uongeze kinga muda wote.

Aliongeza kuwa wao kama wataalamu wa maziwa, wanajitahidi kuwahamasisha wananchi watumie maziwa kama kinywaji cha kawaida ili waweze kuongeza kinga ya mwili na hatimaye kuwa na afya njema.

"Labda niwaambie tu Watanzania wajiwekee utamaduni wa kunywa maziwa ili kuboresha afya zao pia tukinywa maziwa tutapunguza uzee na mikunjo ya ngozi na utapiamlo utaisha," alisisitiza Nyanga.

Mtaalamu wa mbuzi wa maziwa kutoka Kituo cha Utafiti wa Malisho ya Mifugo (Taliri) kilichopo mkoani Tanga, Ayubu kambadu, alisema asilimia kubwa ya watu wamekuwa wakifika kituoni hapo wasema kuwa unywaji wa maziwa ya mbuzi umekuwa ukiwasaidia kwa kiwango kikubwa kutibu matatizo ya vidonda vya tumbo hali inayosababisha kufanya utafiti kwa kina.

Alisema mbuzi wanaopata malisho mazuri na chakula bora wana uwezo wa kutoa maziwa lita mbili kwa siku na maziwa yake yana virutubisho vingi vinavyoweza kumsaidia binadamu aweze kuongeza kinga ya mwili na kuepukana na magonjwa yasiyo ya kuambukizwa.

# Shule msingi 141 zakabiliwa uhaba matundu vyoo 2,235

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, inakabiliwa na upungufu wa matundu ya vyoo 2,236 katika shule za msingi 141 zilizoko katika halmashauri hiyo.

Akizungumza wakati wa kupokea matundu 19 ya vyoo yaliyojengwa na Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kagera katika shule za msingi za Nsheshe na Misenye kupitia mradi wa Ibwera na Rukoma, Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Murshid Ngeze, alisema kuwa wanahitaji matundu ya vyoo 3,603 na kuwa yaliyopo ni 1,367.

Alisema pia wana upungufu wa vyumba vya madarasa 1,337 kati ya vyumba 2,361 vinavyohitajika katika shule za msingi za halmashauri ya wilaya hiyo.

"Mkakati tulio nao kwanza tumeona tuboreshe vyanzo vya mapato, ili tupate mapato yaelekezwe kwenye miradi ambayo haikupata hela kutoka Serikali Kuu, kwa hiyo kipaumbele chetu kikubwa ni vyoo, madarasa, nyumba za walimu na maabara" alisema.

Ngeze alisema mbali na mkakati huo wamekwishatuma maombi kwa wahisani mbalimbali, kwa lengo la kupata fedha ambazo zitasaidia kupunguza changamoto hizo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Bukoba, Kadole Kilugara, akizungumza kwa niaba ya mkuu wa wilaya hiyo, aliwataka wanafunzi kuvitunza vyoo hivyo ili vidumu.

"Tunashukuru kwa kupata huduma ambayo ni ya msingi, ambayo angalau inajali afya zetu na furaha zetu wakati tunaingia katika faragha hii, kwa hiyo ni jukumu letu kama watoto, kutunza mlichopewa," alisema katibu tawala huyo.

Naye mratibu wa mradi wa Ibwera na Rukoma, Lugembe Ng'oga, alidai wametumia zaidi ya Sh. milioni 148 kutekeleza miradi hiyo.

"Kwa ujumla tumekabidhi matundu 19 ya vyoo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 62, lakini tumekabidhi wodi ya mama na mtoto katika kituo cha afya cha Rubale yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 85.1," alisema Ng'oga.



Mtaalamu wa macho wa Hospitali ya Shree Hindu Mandal, Dk. Kishan Mistry, akitoa huduma ya kupima macho katika Hospitali ya Mbagala Rangi Tatu jijini Dar es Salaam jana, walipotoa huduma ya kupima macho, kisukari, saratani kwa watoto, kwa kushirikiana na Klabu ya Lions ya Uhuru. Kushoto ni Mwenyekiti wa klabu hiyo, Zainab Parpia. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri Mkuu kufanya ziara siku nne Singida

**Na Elisante John, SINGIDA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kufanya ziara ya siku nne ya kikazi katika Mkoa wa Singida, kwa ajili ya kukagua na kutembelea miradi ya maendeleo, ikiwamo mikubwa ya kitaifa, pamoja na kufungua maonyesho ya SIDO kitaifa mjini Singida.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alisema jana kuwa ziara ya Majaliwa itaanza Ijumaa katika Wilaya ya Manyoni, akitokea mkoani Dodoma na kuhitimisha Oktoba saba.

Alisema siku ya kwanza Waziri Mkuu atatembelea pia Halmashauri ya Itigi, Oktoba tano atafanya ziara kwenye Halmashauri za Wilaya ya Ikungi na Manispaa ya Singida, na kuwa Jumapili ataendelea na ziara wilaya za Mkalama na Iramba.

Dk. Nchimbi alisema Waziri Mkuu atahitimisha ziara hiyo Jumatatu kwa kufungua maonyesho yaliyoandaliwa na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) katika viwanja vya Bombadia mjini Singida, yatakayomalizika Oktoba 9.

"Katika ziara hii, Waziri Mkuu atakagua na kutembelea miradi ya kimkoa, kukagua na kuona nini kinachofanyika kwenye miradi ya kitaifa, ukiwamo ule wa umeme wa kilovolti 400 unaopokea na kupoza umeme, ambao utasambazwa kwenda hadi nchi jirani kwa ajili ya kuuza," alisema.

Mkuu huyo wa Mkoa alifafanua kuwa pia kwenye ziara hiyo Waziri Mkuu atakagua daraja la mto Sibiti linalounganisha mikoa ya Singida na Simiyu, ambalo limeshakamilika, huku likiunganisha barabara inayokwenda nchi jirani.

Alifafanua kuwa, kazi kubwa iliyobakia ni kuweka lami kipande cha barabara kilomita 20 za maingilio kwenye daraja hilo, hivyo kuzidi kuchochea uchumi wa wananchi wa mikoa hiyo na taifa kwa ujumla.

Aidha, Dk. Nchimbi alisema kwenye ziara hiyo, Majaliwa atatembelea kiwanda cha kampuni ya Biosssitine kinachochambua pamba katika Manispaa ya Singida, ambacho pia kinanunua na kutengeneza mbegu za zao hilo na kusambazwa kwa wakulima nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Sido, Prof. Sylvester Mpanduji, alisema maonyesho ya mwaka huu yatakuwa na mvuto mkubwa, kutokana na ushiriki wa mataifa makubwa ikiwamo China, India na Afrika Kusini, ambazo zimepiga hatua kubwa, kwa teknolojia ya viwanda.

# Shule binafsi zalia uchache wanafunzi

**Na Daniel Sabuni, ARUSHA**

WADAU wa elimu mkoani Arusha wameshuhudia jinsi idadi ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita katika shule za binafsi ikiwamo Sekondari ya De Foucauld inavyoporomoka licha ya juhudi mbalimbali kufanyika ili wanafunzi wafaulu kwa viwango vya juu.

Akizungumza katika mahafali ya 10 ya kidato cha sita Mkuu wa Shule hiyo, Vicent Mattowo, alisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto ya kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi licha ya kujitahidi kufundisha na kuwa na viwango vya juu vya kitaaluma.

Alisema shule hiyo, ilianzishwa miaka minne iliyopita ilikuwa na wanafunzi wanane na mwaka 2017 walihitimu kwa kupata daraja la pili.

Aidha, alisema shule hiyo katika ufaulu ilishika nafasi za juu kitaifa na ndani ya mkoa wa Arusha na mara nyingi wamekuwa wakijitahidi kufanyakazi kwa bidii.

Kwa kipindi cha mwaka 2018, shule hiyo ilikuwa na wanafunzi wawili na walifaulu kwa daraja la pili na kushika nafasi ya 25, katika ya shule 127.

Kwa mwaka 2019, wamehitimu wanafunzi kumi ambao walifaulu kwa kiwango cha kuridhisha na walishika nafasi ya juu kitaifa na pia katika kanda na kimkoa.

Alisema pamoja na jitihada hizo walimu wa shule hiyo na wanafunzi bado kuna idadi ndogo ya wanafunzi, lakini alisema wataendelea kuimarisha kiwango cha elimu shuleni hapo ili kuwa na mafanikio zaidi.

"Licha ya kuwa na mafanikio makubwa bado tunakabiliwa na changamoto ya uchache wa wanafunzi na uhaba wa nyumba za walimu kitendo kinachopelekea kuchelewa kufika shuleni," Mattowo.

Mdhibiti wa Ubora wa Shule Kanda ya Kaskazini Magharibi, Emmanuel Bilikiye, aliipongeza shule hiyo, kwa kuwaandaa wataalamu ambao wataisaidia nchi kufikia uchumi wa kati na wa viwanda.

Aliwataka wahitimu hao kuwa mabalozi wa zuri wa shule hiyo popote watakapokwenda na kutoa ushuhuda wa kweli wa ufaulu walioupata shule hapo.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Monica Gaudence, aliwataka wazazi kuwapeleka wanafunzi shuleni hapo kwani watakuwa na uhakika wa kufaulu.

Kaimu Ofisa Elimu Jiji la Arusha, Prosper Kessy, aliwaomba wazazi na walezi kupeleka watoto wao kwani imejenga miundombinu bora na rafiki kwa wanafunzi kusoma.

# Vijana waomba mipira ya kiume

**Na Allan Isack, ARUSHA**

KATIKA harakati za kujikinga na maradhi ya ngono pamoja VVU na Ukimwi, vijana wameiomba serikali kuongeza kasi ya kusambaza mipira ya kiume ili imfikie kila mhitaji na iwe kwenye vituo vya afya na pia kuweka utaratibu bora wa upatikanaji wake kwenye maduka ya wazi ili kuendana na ongezeko la wateja.

Ombi hilo lilitolewa na baadhi ya vijana katika mafunzo ya kujiepusha na maambukizi ya VVU na Ukimwi katika mashindano ya kusaka vipaji vya Bongo Star Search (BSS), 2019 jijini Arusha.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), yalilenga kuangazia maambukizi ya VVU na Ukimwi, ngono, matumizi ya dawa za kulevya na kutumia kwa usahihi mipira ya kondomu.

Akizungumza kwa niaba ya vijana wengine, Elibariki Simon na Maiko Joseph Shonga, walisema vijana kufanya ngono na wanawake zaidi ya mmoja na baadhi ya wanawake wamekuwa wakitumia ushawishi wa fedha kuwarubuni vijana wadogo kingono.

Maiko Joseph Shonga (22) kutoka mkoa wa Ruvuma alisema vijana wa kiume wenye umri mdogo wamekuwa wakishawishiwa na wanawake wenye umri mkubwa kushirikiana nao kingono na hivyo wakataka kuwapo na mipira zaidi ya kiume ili kuwaepusha na magonjwa ya ngono.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Tume ya Kudhibiti Ukimwi TACAIDS, Nadhifa Omari, alisema mafunzo hayo, kwa vijana yamelenga kuwakumbusha namna ya kujikinga na maambukizi mapya ya Ukimwi na VVU.

Alisema takwimu za kitafiti za viashiria vya Ukimwi zilizofanyika mwaka 2016 /17 zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya vijana inaambukizwa kwa wastani wa asilimia 80.

Aidha, alisema vijana hao ni wale wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24 wakifuatiwa na wenye umri wa miaka 24 mpaka 49 na wote wana maambukizo ya asilimia 4.7 ya VVU hapa nchini.

Alisema mafunzo hayo, yamelenga kutoa elimu ya kujikinga na Ukimwi, matumizi sahihi ya mipira ya kiume, kujikinga na VVU na Ukimwi, kunyanyapaa na kujinyanyapaa miongoni mwa waathirika.

Aidha, aliwahimiza vijana kupima ili kujua afya zao na kuanza kutumia tiba mara moja.

Aliongeza kuwa mafunzo hayo wamekuwa wakiyatoa kwenye matamasha ya vijana na yataendelea kwenye mikoa mbalimbali hapa nchini katika mashindano ya kusaka vipaji ya BSS.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Star High ya Mbuguni wilayani Arumeru, mkoani Arusha, Sister Monica Massawe, akiwapongeza baadhi ya wanafunzi waliohitimu kidato cha nne kwenye mahafali ya 10 ya shule hiyo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Gambo apania kuinua elimu

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MKOA wa Arusha unaandaa mkakati wa kielimu wa kuongeza ufaulu kwa shule za msingi kwa kuanzisha utaratibu wa kuwa na mtihani jumuishi wa shule binafsi zenye mchepuo wa Kiingereza ili kutambua shule zilizoko nyuma dhidi ya zile zinazofanya vizuri.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, katika mahafali ya wanafunzi wa darasa la saba na la awali yaliyofanyika katika shule ya mchepuo wa Kiingereza ya Green Valley ya jijini Arusha.

Katika mahafali hayo, jumla ya wanafanzi 120 wa darasa la saba walihitimu na kutunukiwa vyeti.

Gambo alisema utaratibu huo, utafanyika kila mara kwa wanafunzi kupewa majaribio ya mtihani ambao utatungwa na kuchapishwa mkoani hapa, na wanafunzi hawatalipa wala kugharamia kuchapisha mitihani hiyo.

Alisema lengo la kutungwa kwa mitihani hiyo ni kuleta mwamko wa kielimu mkoa wa Arusha na kubaini uwezo wa shule za msingi zinazofanya vizuri na zile ambazo zinasuasua.

Awaambia wadau kuwa kamati maalumu imeundwa kwa ajili ya kufuatilia na kubaini chanzo cha kutofanya vizuri kwa shule hizo na hatua zitachukuliwa.

"Tumeanzisha mpango mpya wa mtihani wa pamoja na utafanywa na shule zote za msingi za serikali na binafsi lengo ni kushindanisha uwezo wa shule zetu ili kubaini shule ambazo zinafanya vizuri na zinazosuasua, tumeunda kamati itakayochunguza sababu za kutokufanya vizuri kwa shule hizo," alisema Gambo.

Aidha, Mkuu wa Mkoa alisema anakerwa na taarifa za wanafunzi wa kike kubebeshwa mimba huku wahusika wa mimba hizo na wazazi wakiyamaliza kinyumbani jambo ambalo amewataka wazazi kutokukubali watoto wao kukatishwa ndoto zao za elimu na watu.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Yahaya Ndarita, alisema shule binafsi zenye mchepuo wa Kiingereza zimechangia kuboresha elimu nchini na wanafunzi wanapomaliza elimu ya msingi wanakwenda kuchangamshwa kwenye masomo ya sekondari za kata na kuleta ushindani wenye tija kwa taifa.

Aliwataka wazazi kutokuhofia kuwapatia watoto elimu bora kwa kuogopa gharama kwani kile wanacholipia kinachagiza ubora wa elimu na kusaidia kulikomboa taifa kielimu.

## Kibano wazazi wanaoruhusu watoto biashara

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

SERIKALI imeonya kuwa haitasita kumfikisha mahakamani, mzazi au mlezi atakayemshauri au kumlazimisha mtoto wake kujiingiza katika biashara ya ujasiriamali, kazi za nyumbani na kuchunga mifugo baada ya kuhitimu darasa la saba.

Ofisa Tarafa ya Moshi Magharibi, Senzia Lushino, alisema kumlazimisha mtoto aliyehitimu darasa la saba kujiingiza katika kutafuta kipato, badala ya kuendelea na masomo ya sekondari ni ukatili ambao unapaswa kukemewa.

Lushino alikuwa akizungumza jana, wakati wa mahafali ya Shule ya Mchepuo wa Kiingereza ya GoodShepherd, kwa niaba ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana na Ajira, Athony Mavunde.

"Kila mmoja anazo ndoto zake, hivyo wanapomaliza ni lazima kuhakikisha wanaendelea na masomo yao maana wapo baadhi ya wazazi ambao watoto wao wakimaliza darasa la saba wanafikiria kuwaozesha, kuwafanya kuwa wadada wa kazi na kwa wavulana kuwafanya kuwa wachungaji wa mifugo, machinga.

Hapana, jambo hilo ni hatari kwa ustawi wa taifa letu," alisema Lushino.

Alisema kama serikali itabaini kuna wazazi au walezi wanaendelea kuwasukuma watoto wao kujiingiza katika mambo hayo, wajiandae kwenda mahakamani, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009.

Kuhusu ukatili wa kijinsia, ofisa huyo alisema katika Wilaya ya Moshi bado kuna wimbi kubwa la baadhi ya watu ambao wamekuwa wakiwafanyia vitendo vya ukatili watoto wao kwa kutowapatia elimu.

Alidai yako mambo mawili yanayowakwaza watoto hivi sasa katika jamii ambayo ni kunyimwa haki ya elimu, ukatili wa kingono na unyanyasaji wa kijinsia.

Mkurugenzi wa Shule ya Good Shepherd iliyopo Himo, nje kidogo ya Mji wa Moshi, Jairous Chilewa, alisema malengo makubwa ya kuanzisha shule hiyo ni kuipa nguvu sera ya elimu ya mwaka 2014 kutekelezwa kwa tija.

Hata hivyo, alisema zipo changamoto mbalimbali kama vile kukosekana kwa vyumba viwili vya madarasa, gari moja ya kubebea wanafunzi ikiwa ni pamoja na baadhi ya wazazi kutolipa karo kwa wakati, hivyo kusababisha shule kushindwa kuwa na mpangilio mzuri wa bajeti.

**"Kila mmoja anazo ndoto zake, hivyo wanapomaliza ni lazima kuhakikisha wanaendelea na masomo yao maana wapo baadhi ya wazazi ambao watoto wao wakimaliza darasa la saba wanafikiria kuwaozesha, kuwafanya kuwa wadada wa kazi na kwa wavulana kuwafanya kuwa wachungaji wa mifugo, machinga.**

# RC aibua upya matumizi ya kiberenge Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MJADALA kuhusu matumizi ya 'kiberenge' au magari maalum ya kutumia nyaya katika Mlima Kilimanjaro, umeibuliwa tena na Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Anna Mghwira, anayetaka Waziri wa Maliasili na Utalii kuhitimisha ndoto hiyo au kuruhusu mjadala wa kitaifa.

Tanzania inataka kuongeza idadi ya watalii kupitia magari ya kutumia nyaya katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro ambao ndio mlima mrefu zaidi barani Afrika uliosimama.

Akizungumza juzi, wakati wa akizindua kampeni maalum ya kuupigia kura Mlima Kilimanjaro ili ushinde na kutangazwa kuwa kivutio bora cha utalii duniani, Mghwira alisema:

"Ninaamini pia kwamba, baada ya tukio hili la Kili Challenge 2019, Twenzetu Kileleleni, Mheshimiwa Waziri (Kigwangalla) utatusaidia kuhitimisha na kuongoza mjadala wa matumizi ya kiberenge katika Mlima Kilimanjaro, kama unakuja ama hauji ama unafaa au haufai."

Awali kulikuwa na taarifa kwamba, serikali ilikuwa imeanza mazungumzo na kampuni moja ya China na nyingine ya Magharibi.

Njia iliyokuwa inapendekezwa kutumika kwa kiberenge hicho cha utalii ni ile ya Machame ambayo kwa mujibu wa watoa huduma, ndio njia inayotumika na wageni zaidi kuliko njia nyingine zote kuelekea mlimani.

Kiberenge hicho kinatajwa kwamba kinaweza kuongeza idadi ya watalii kwa asilimia 50, kwa sababu kina uwezo wa kuwawezesha wale wasioweza kupanda mlima huo kwa miguu kufika kilele cha Uhuru chenye urefu wa mita 5, 895.

Aina hiyo ya kuchochea utalii haitakuwa ya mara ya kwanza duniani, kwa vile magari ya kutumia nyaya au viberenge yapo nchini Sweden, Italia na Himalayas.

Kwa sasa Mlima Kilimanjaro unawania tuzo ya dunia ya kivutio bora cha utalii kinachoongoza kwa mwaka 2019.

Mlima Kilimanjaro pamoja na nchi nyingine duniani zinazosifika kwa utalii, zimeorodheshwa na Taasisi ya Kimataifa ya World Travel Awards 2019 na kuingizwa katika shindano hilo.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati), akipiga makofi baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Nyisanze wilayani Chato, mkoani Geita jana. **PICHA: WN**

# Wodi wagonjwa wa nje kwa maradhi mlipuko kujengwa

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

WODI mpya ya wagonjwa wa nje wanaokabiliwa na maradhi ya mlipuko, inatarajiwa kujengwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi) ili kutoa huduma zinazohitaji madaktari bingwa.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema serikali imejiandaa kujenga wodi maalum ya kuwalaza na kuwahudumia wagonjwa wa maradhi ya mlipuko, kwa kuwa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa iliyopo mpakani mwa nchi.

Kwa mujibu wa Mghwira, ofisi yake imepokea maelekezo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ikitaka kuanza mchakato wa ujenzi huo wa wodi maalum ya kuhudumia wanaopata maradhi ya mlipuko.

Alisema maelekezo hayo ya wizara, yanataka kila mkoa wenye Hospitali ya Rufani kujenga wodi hiyo.

"Hiyo wodi itakuwa na jukumu la kuwalaza wagonjwa wa maradhi ya mlipuko kama ebola, kipindupindu na ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Lengo la serikali ni kuwakinga wagonjwa wengine wasiambukizwe lakini pia wahudumu wa afya nao wasiambukizwe," alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Alisema kipindi hakuna magonjwa ya mlipuko, wodi hiyo itatumika kwa kazi nyingine na kwamba mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imejipanga kutoa chanjo ya ugonjwa wa homa ya ini.

Alisema pamoja na Mkoa wa Kilimanjaro kutoa chanjo ya magonjwa mbalimbali, pia umejikita kutoa elimu na kuwahamasisha wananchi kupata chanjo ya ugonjwa wa homa wa ini.

Ugonjwa huo unasababishwa na vitu mbalimbali ikiwamo virusi vya Hepatitis B na C na maambukizi ya bakteria, fangasi (kuvu) na matumizi ya pombe kali ambayo yanachangia kuleta shida hiyo.

Duniani kote watu wanaoishi na virusi vya Hepatitis B, wako milioni 257, kulinganisha na watu milioni 37 ambao wanaoishi na virusi vya Ukimwi. Kwa Tanzania ukubwa wa maambukizi ni asilimia 4.5 licha ya Tanzania imejitahidi kutoa chanjo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 1, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 19



## Gambling Addiction (Uraibu wa michezo ya bahati nasibu)

Ukurasa 15



## Kuvuja mitihani kielelezo cha maadili potofu katika jamii



Ukurasa 18

## Vita bado chanzo kikubwa ukiukwaji haki za mtoto



# Ajali ilivyogeuza michango ya harusi kuwa rambirambi

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# Tanzania bila ya dawa za kulevya inawezekana



Kijana akitumia dawa za kulevya. **PICHA: MTANDAO**

TATIZO la dawa za kulevya hapa nchini bado linaendelea kuathiri taifa na jamii kiujumla.

Kosa la dawa za kulevya ni miongoni mwa makosa ya jinai ambalo kisheria limekuwa likipewa mtazamo wa kipekee kulingana na athari zake kijamii na kitaifa.

Kosa hili limekuwa ni tishio kwa usalama wa wananchi na taifa kwani limekuwa likizalisha makosa mengine ambayo ni makubwa na yanaathiri jamii, kama vile usafirishaji haramu wa binadamu (human trafficking), utakatishaji wa pesa (Money laundering) na makosa mengine yanayovuka mipaka ya nchi (trans-national organized crime).

Serikali ikishirikiana na wadau wengine ndani na nje ya nchi imekuwa ikifanya jitihada katika kuzuia na kupambana na tatizo hili.

Inatumia vyombo vyake vya Dola vinavyohusika katika udhibiti na upambanaji wa dawa za kulevya- Polisi chini ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, ikisaidiana na wadau wengine wanaohusika kwenye ukamataji na upelelezaji wa makosa haya kuhakikisha tatizo hili linadhibitiwa katika nyanja zote za kijamii na kitaifa.

**MIKAKATI YA JESHI LA POLISI**

Jeshi la Polisi limeanzisha madawati maalum yanayoshughulika na ukamataji, upelelezi na ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia kwa makosa ya dawa za kulevya, ikisaidiana na kitengo cha Polisi Jamii katika mikoa yote pamoja na kanda zake.

Uelimishaji wa jamii katika athari za matumizi ya dawa za kulevya, uuzaji na usafirishaji wa dawa hizo, kwa kutumia fursa hizo katika makongamano mbalimbali, warsha, sherehe za kitaifa ili kupunguza tatizo hilo kwa haraka kuliko kupambana na raia mmoja mmoja au vikundi vidogo vidogo.

Uimarishaji wa doria, misako na operesheni katika vijiwe na mitaa yote ambayo wahalifu hao wamekuwa wakikaa na kufanya biashara hiyo ya dawa za kulevya, hivyo kupunguza tatizo hilo kwa baadhi ya mitaa na vijiwe vingine kusambaratishwa kabisa.

Kuimarisha doria za majini na ulinzi mipakani mfano viwanja vya ndege (Airport) na mipaka ya nchi kavu kwa kushirikiana na taasisi nyingine za kiserikali na zile za binafsi.

Hiyo ni katika kupambana na wahalifu ambao wamekuwa wakitumia maboti na majahazi ya kisasa katika kuingiza dawa za kulevya, pia usafiri wa ndege katika kuingiza na kutoka nje ya nchi.

Mafunzo ya kuwajenga wapelelezi na watafutaji wa taarifa (intelligence) yamekuwa yakitolewa ndani na nje ya nchi kwa udhamini wa wadau mbalimbali toka nchi wahisani ambayo yamekuwa yakidhaminiwa kwa kiasi kikubwa na taasisi hizo, hivyo kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na kusaidia kupunguza tatizo la dawa za kulevya.

**MIKAKATI KIJAMII**

Kuimarika kwa mfumo wa utoaji taarifa kutoka kwa jamii husika kutokana na uhamasishaji na uelimishaji kuhusu athari za dawa za kulevya, unaotolewa na Jeshi la Polisi pamoja na wadau wake.

Vilevile kutokana na mzigo ambao familia, jamii husika na taifa imekuwa ikipata kutokana na kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya, hivyo jamii yenyewe wamehamasika katika kushiriki moja kwa moja katika utoaji wa taarifa za uhalifu na wahalifu wa dawa za kulevya bila shuruti.

Taasisi binafsi, baadhi ya wananchi wazawa, taasisi za kidini na wadau wengine wameshiriki katika vita hii ya kupambana na dawa za kulevya kwa kujenga na kuanzisha vituo vya kulelea waathirika wa dawa za kulevya (sober houses) katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Aidha, serikali imekuwa ikiwapa ushirikiano wa ushauri na kuwashirikisha katika hafla mbalimbali za kitaifa ili kuleta hamasa kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yanashiriki katika udhibiti na upambanaji wa janga la dawa za kulevya kwa watoto na vijana kwa kuunda vikundi vya michezo mbalimbali inayohusisha makundi ya vijana wa mitaani.

Lakini pia watoto walio katika makambi ya kulelea watoto/wanaoishi katika mazingira magumu, na wanafunzi waliopo kwenye vyuo mbalimbali.

***ITAENDELEA WIKI IJAYO***

***Imetolewa na:***

***Ofisi ya Uhusiano***

***Makao Makuu ya Polisi.***



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**

marobarnabas@yahoo.com

# Bakita timizeni wajibu wenu

'WAJIBU' ni faradhi*, yaani jambo linalomlazimu mtu kulitekeleza. *Faradhi pia ni kima cha chakula kinachomtosheleza mtu kushiba. Vilevile mauti. Imenilazimu kueleza maana ya maneno haya ili nieleweke vizuri.

Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) ni kama 'linakubaliana' na magazeti yetu ya michezo yanayobadili maana ya baadhi ya maneno ya Kiswahili na kutumia tofauti na maudhui yake. Ni kama petroli kuitwa 'dizeli' au grisi/girisi kuitwa 'oili!'

Aidha, baadhi ya maneno halisi ya Kiswahili hayatumiwi na badala yake maneno ya Kiingereza ndio hutumiwa kwa kubadili lahaja ingawa yapo ya Kiswahili fasaha (-enye usahihi wa matumizi ya maneno)!

Wahenga walisema "Chako ni chako, cha mwenzako si chako." Kitu unachokiita chako ni kizuri na huweza kukufaa. Una uhuru nacho kuliko cha mtu mwingine. Twafunzwa tuvitegemee vitu vyetu kuliko vya watu wengine.

"Tunatesti mitambo Zahera aja na sapraizi, jezi mpya balaa." Ni kichwa kwenye gazeti maarufu la michezo nchini. Maneno yaliyotumiwa vibaya ni: 'Tunatesti', 'mitambo', 'sapraizi' na 'balaa.'

'Tunatesti.' Neno hili limetoholewa (kitendo cha mtu kubadilisha matamshi au tahajia ya neno la lugha moja ili lilingane na matamshi au tahajia ya lugha nyingine) kutoka Kiingereza, yaani 'test.' Maana ya neno hili kwa Kiswahili ni jaribu, tahini, pima; pia jaribio, mtihani, kipimo; upimaji. Kwa nini mwandishi hakutumia moja ya maneno hayo?

'Mtambo' ii) ni kifaa chenye kutoa nguvu za kuendesha vitu vinavyofanya kazi mbalimbali; iii) Kitanda kinachotumiwa kufumia nguo; iv) Kamba inayotengenezwa kwa chane za miyaa na hutumiwa kuvutia mtego wa samaki; na v) ni mashine. Kwa nini wachezaji walinganishwe na mitambo, vitanda vya kufumia nguo au kamba zinazotengenezwa kwa chane za miyaa?

'Sapraizi' ndivyo linavyotamkwa kwa Kiingereza na maana yake kwa Kiswahili ni mshangao, mastaajabu, mzumbao. 'Cause surprise' yaani shangaza. Take 'somebody by surprise' yaani fumania, shtukiza, tokea mtu kwa ghafla (pasi na yeye kutarajia).

'Balaa' au 'baa' ni janga lililoenea katika jamii au kwa mtu binafsi; ii) jambo, kitu au mtu anayedhaniwa kuleta maafa, mkosi au hasara; iii) kisirani, nuksi. Kwa maana hiyo jezi mpya za Yanga zitawaletea maafa, mkosi au hasara? Ni kweli zina kisirani au nuksi!?

Kama ndivyo kwa nini Yanga wamekubali kutengenezewa au kununua jezi zitakazowaletea balaa? Watakaopata balaa ni wachezaji au klabu kwa ujumla wake wakiwemo viongozi, wanachama na mashabiki?

Kichwa kingine kiliandikwa: "Simba Arusha wakatwa stimu." Neno 'kata' lina maana takribani saba zisizoendana na maana iliyokusudiwa na mwandishi wa habari husika. Waaidha (kiunganishi cha kuonesha vilevile; pia, isitoshe, aidha) 'stimu' au 'stima' ni jiko litumialo umeme, spaki.

"Ule mzuka waliokuwa nao wanachama na mashabiki wa Simba jijini Arusha wa kuchangia damu kama sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Simba umekatwa baada ya kushindwa kutoa damu kwa kukosekana kwa maabara yenye vifaa maalum kwa ajili ya huduma hiyo."

Nimeeleza mara nyingi kuwa 'mzuka' ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na huweza kumtokea mtu. Maana ya sentensi ya mwandishi ni kwamba wanachama na mashabiki wa Simba jijini Arusha walikumbwa na pepo/mapepo! Bakita hawaoni upotoshwaji huu wa Kiswahili?

"Wakiwa kwa wingi wao katika kituo hicho baada ya kufanya usafi, waliunga foleni kwa ajili ya kutoa mchango wa damu, lakini viongozi wa hospitali ukawajulisha zoezi limekwama kwa kukosekana kwa huduma hiyo."

Kama ilivyoandikwa ovyo kwenye paragrafu (fungu la maneno katika matini linalofafanua wazo moja) ya kwanza, ndivyo ilivyo kwenye paragrafu ya tatu ya habari ninayoiandikia.

Imeandikwa: "Wakiwa kwa wingi wao katika kituo hicho baada ya kufanya usafi, waliunga foleni kwa ajili ya kutoa mchango wa damu lakini viongozi wa hospitali ukawajulisha zoezi limekwama kwa kukosekana kwa huduma hiyo." (Sentensi ya maneno 32 iliyoandikwa shelabela, yaani hali ya kukosa mpango maalumu).

Ingeandikwa: "Baada ya kufanya usafi walijipanga kwenye foleni ili kuchangia damu, lakini ilishindikana kwani hospitali husika haikuwa na vifaa vya kutolea damu."

"Mwenyekiti wa Simba wa tawi hilo la Kwa Mrombo, Zuberi Daffa alisema wamesikitika kuandaa kwa gharama wanachama wao kwa ajili ya zoezi hilo lakini wamekwamishwa na ukosefu wa vifaa."

**METHALI: WEREVU MWINGI MBELE KIZA.**

**MAROBARNABAS@YAHOO.COM**

**0784 334 096**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Kuvuja mitihani kielelezo cha maadili potofu katika jamii

TAARIFA chache za kuvuja kwa mitihani ya darasa la saba zimejitokeza mkoani Singida katika shule mbili za msingi, hali inayoonyesha kuwa uvujaji wa mitihani hiyo mwaka huu ulikuwa mdogo.

Kimantiki ni wazi kuwa kuwapo kwa matukio mawili ya kuvuja kwa mitihani katika shule ambazo ziko jirani ni sawa na tukio moja la kuvuja mitihani lililofanyika katika shule mbili kwa wahusika kushirikiana.

Na ndivyo madai dhidi ya watuhumiwa kuhusiana na suala hilo yalivyoelezwa mahakamani, kuwa ni njama za pamoja kuvujisha mitihani na kutokufanya kazi ipasavyo wakati wa kusimamia mitihani, kukagua.

Licha ya kuwa tukio la kuvuja mitihani limefahamika kwa uwazi kutokana na watuhumiwa kufikishwa mahakamani, haielekei kuwa hapakuwa na matukio mengine ya kuvuja mitihani, kwani si lazima hali hiyo igundulike wakati wa tukio.

Mara nyingine ni pale usahihishaji wa mitihani unafanyika, au tayari umekamilika halafu matokeo yanaangaliwa kwa shule na orodha ya wanafunzi, halafu inaonekana zaidi ya asilimia 80 wana alama za juu kabisa za kufaulu, hali ambayo siyo ya kawaida.

Ni hali ambayo msingi wake ni kutokea kwa majibu ya mitihani au matokeo ya awali yanayokinzana kabisa na mazingira halisi ya matokeo, yenye msingi wake katika kile kinachoitwa 'normal curve,' 'mgongo takwimu wa kawaida.'

Katika dhana hiyo, sehemu kubwa ya watahiniwa wataangukia katikati ya upana wa 'mgongo takwimu' husika, kupata matokeo ya wastani yanayoendana na uwezo wao au vipaji katika masomo hayo.

Eneo hilo la kati siyo la alama au matokeo yanayofanana bali yanapishana kiasi, kwa mfano kuanzia asilimia 50 hadi asilimia 70 ya kupata alama za vema, na pia kiwango hicho cha kufaulu vizuri.

Ila kuna upande mwingine wa ufaulu dhaifu na hata kushindwa kabisa ambao ni kipenyo hasi (na ncha) upande wa kushoto wa 'mgongo takwimu' au mchoro wa kihesabu kudhihirisha matokeo, na upande mwingine wa ufaulu wa zaida, yaani wachache wanaoweza kuvuka asilimia 70 hadi 80, kwa mfano.

Ziada si kawaida, ila kuna aina ya mitihani ambako mwanafunzi anaweza kupata asilimia 90, kwa vyuo vikuu si mojawapo.

Inapotokea kuwa wanafunzi takriban wote wamevuka asilimia 70 ya ufaulu, hakuna haja ya upelelezi kujua kuwa mtihani umevuja, kwani endapo wanaumudu mtihani kiasi hicho, ina maana kuwa siyo mtihani wa darasa lao ila ni wa chini kabisa.



Wanafunzi wakiwa katika Mtihani wa Taifa wa kidato cha nne. **PICHA: MTANDAO**

> Hisia hiyo ambayo kiitikadi inaitwa 'uzalendo' kimsingi ni hisia ya kutenda haki, lakini ni suala gumu kuwafundisha watu kwani tunajipendelea kifamilia, si kutenda haki.

Upeo wao umevuka mbali kiwango cha kufikiri na utata wa maswali kinacholengwa au kuainishwa katika mtihani, jambo ambalo haliwezi kutokana na kile mwalimu alichofundisha, kwani hawawezi kukumbuka kila kitu na kukieleza kama kilivyo katika mtihani.

Ni wazi kuwa ili mtihani uvuje na isijulikane, inabidi wengi waboronge pamoja na kuwa na nakala ya mtihani, lakini majibu yanapokuwa ni ya kuchagua na kuweka alama jibu lipi ni sahihi, hawawezi kuboronga. Ndiyo maana tatizo la mtihani kuvuja linazidishwa na aina ya mtihani unaofanywa, kuwa ni wa kuchagua kati ya majibu manne na kuweka alama.

Ingekuwa ni kutafakari na kuandika ingebidi matayarisho yawe magumu zaidi, yaani kuvujisha mtihani, kufanya insha zinazotakiwa halafu kutoa nakala wanafunzi wapenye nazo chumba cha mtihani au wanakili kwenye simu.

Mbinu ya simu ilitumiwa katika uvujishaji na kujibu maswali huko Singida, na miaka ya nyuma hata uvujishaji wa maswali kamili ya kuandika insha fupi ulikuwa unatokea, halafu wanafunzi watayarishe makaratasi ya majibu, hasa katika mitihani ya kumalizia shule ya sekondari.

Mtahiniwa anatoka nje kujisaidia halafu rafiki yake anamngoja huko na karatasi ya 'pointi' zote muhimu za kuandika katika swali lile; akirudi na kikaratasi hicho 'anatiririka' tu.

Hata hivyo ujanja huo uligunduliwa na mtahiniwa huyo alifutiwa matokeo, ingawa alikuwa yeye peke yake na hapakuwa na tatizo la kituo cha mtihani kufutiwa matokeo.

Hali hii inatokea mara kwa mara kuwa licha ya kutogunduliwa kuvuja kwa mtihani wakati mtihani huo unafanyika, inatokea mtahiniwa apate majibu takriban yote sawasawa, wakati uwezo wake ni wa wastani tu katika darasa, hivyo kuleta hofu imekuwaje aweze 'kucharuka' kiasi hicho wakati wa mtihani.

Kimsingi uvujaji wa mtihani una sura mbili, ya mtu mmoja na ya kitaasisi, ambako tatizo la kimfumo linaingia endapo taasisi imeruhusu au imezidiwa nguvu na mtihani ukavuja kwa wanafunzi takribani wote, tofauti na akivujishiwa mtu mmoja. Wakati ambapo kisaikolojia hakuna mtu asiyefahamu ujuha wa kuvujisha mtihani na kuwasaidia wanafunzi kushinda kifedhuli, au kujidhania wameshinda wakati mfumo au mpangilio wa matokeo utatoa siri kuwa mtihani ulivuja, bado jitihada hiyo imekuwa ikifanyika mara nyingi.

Unaweza kusema kuwa sababu yake ni mshikamano katika ngazi ya familia na urafiki wa kawaida, kuwa ni vyema kijana akipata alama nzuri apate kuingia sekondari au 'high school,' na hata vyuoni mitihani inavujishwa ili kuwasaidia wanafunzi kupata alama za juu. Inajenga uwezo wa kuajiriwa mahali pazuri baadaye, madhara pembeni.

Kuvujisha mitihani ni kielelezo cha ubinafsi wa kawaida miongoni mwa watu, iwe ni kwa kutaka shule ionekane imefanya vizuri kuliko uwezo wake halisi, au mtoto ambaye ni mwanafamilia atengenezewe mazingira ya kuvushwa hadi sekondari kwa kupewa mtihani.

Ni wazi hakuna hisia ya kuangalia mtihani kama jaribio ambako kila mwanafunzi anatakiwa apate alama sahihi kulingana na uwezo wake ambao utaonekana katika kile alichojibu.

Hisia hiyo ambayo kiitikadi inaitwa 'uzalendo' kimsingi ni hisia ya kutenda haki, lakini ni suala gumu kuwafundisha watu kwani tunajipendelea kifamilia, si kutenda haki. Kuvujisha mitihani ni hisia ya kudhania unaweza kumdanganya mtahini kwa kumsaidia mtahiniwa kujua mtihani ulivyo na kutayarisha majibu, lakini anayesaidiwa anaishia kujitia kitanzi kwa kujifanya anajua kila kitu.

Ni wazi kuwa wavujisha mitihanii wataendelea kukamatwa, iwe ni darasani wakati mtihani unafanyika au ni baada ya kusahihisha na kuona kuwa matokeo yana dalili za upotofu wa mazingira ya kufanyika mtihani huo.

Hakuna darasa lenye wanafunzi wenye alama za A tu siku zote, hivyo inapotokea kufaulu ni kwa ngazi hiyo, hapatakuwa na afueni kwa mtihani huo utafutwa, wahusika watagunduliwa na siyo ajabu ikawaathiri wanafunzi hao (kama mtihani ulivuja kitaasisi) wakaketi tena mtihani huo mwaka unaofuata, katika kituo kingine. Na muda huo uliobaki wanasota nyumbani, hawana vyeti na hawako sekondari.

SIMULIZI

**NA WILLIAM CHARLES**

# Ajali ilivyogeuza michango ya harusi kuwa rambirambi

KABLA ya Mei 19, 2019, Nicholaus Jackson Mwandunga hakuwahi kuhudhuria msiba wala mazishi ya ndugu yake yeyote wa damu aliyefariki kwa ajali ya barabarani. Alikuwa akisikia tu misiba ya aina hii ikiwakumba watu wengine.

Nicholaus (38), hakujua kuwa tarehe hiyo ingebadili kabisa historia yake, kutoka kuwa kaka mwenye wadogo zake watatu mpaka kuwa mtoto mdogo zaidi aliye hai wa Faith Rahabu Kifwange.

Faraja Mwandunga (35), James Mwandunga (32) na Diana Mwandunga (28) wote walikua wadogo zake, lakini ajali ya gari iliyotokea Jumatano, alfajiri ya Mei 19, 2019 ilikatiza uhai wa wadogo zake wote, akiwamo Diana ambaye alikuwa mbioni kufunga ndoa siku saba baadaye.

Ndugu hawa wote walikuwa wakiishi na kuendesha shughuli zao jijini Dar es Salaam na walipata ajali wakirejea kutoka katika sherehe ya kumuaga Diana, mkoani Mbeya ambapo familia yao ilipanga kufanya sherehe mbili; moja Mbeya alipo mama yao mzazi na nyingine jijini Dar es Salaam walipo ndugu wengine.

Sherehe ya kumuaga mwanamke anayekaribia kuolewa (Send Off), ni utamaduni maarufu nchini na duniani, ambapo familia ya bibi harusi mtarajiwa ndiyo huiandaa siku chache kabla ya harusi, mara nyingi ikiwa ni ndani ya wiki itakayofanyika harusi.

Nicholaus Jackson Mwandunga anaeleza kuwa, sherehe ya kumuaga Diana, bibi harusi mtarajiwa ilishafanyika nyumbani kwao Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Mei 16, 2019 na yeye na ndugu zake walijipanga kurejea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya sherehe ya harusi kwa usafiri wa gari ndogo, mali ya kaka yao mkubwa Stephano Mwandunga.

"Bibi harusi mtarajiwa (Diana), hakutakiwa kupanda gari letu, yeye alitakiwa aondoke mapema Mei 17 kwa ndege na mumewe mtarajiwa lakini alikataa...akataka kuondoka na sisi, huku mumewe mtarajiwa Elisante Edward akiamua tu kupanda basi la abiria ili kurejea Dar es Salaam," anasema Nicholaus na kuongeza:

"Siku ya tukio tulisafiri kama kilometa 40, tukiwa ndani ya mkoa wa Mbeya, tulipofika Igawa, njia panda ya Mbeya - kuelekea Rujewa, upande wetu tuliokuwa tunatembelea, palikuwa wazi."

Anabainisha kuwa mbele yao katika upande wa gari walizokuwa wakipishana nazo waliona malori mawili yalimesimama barabarani, huku yakiwa yameachiana umbali wa mita takribani 20 kutoka lori moja na jingine.

"Nadhani moja lilikuwa limeharibika na lingine lilisimama kutoa msaada... na kwa sababu ya wembamba wa barabara, hayakusimama pembeni bali yalikuwa barabarani," anasema na kuongeza:

"Dereva wetu alikuwa kwenye mwendo mkali wa kilomita kama 90 au 100 hivi tukiteremsha eneo hilo la mlima, lakini ghafla tukaona Fuso likiwa mwendo mkali likija katika njia yetu, baada ya kuhama upande wake uliokuwa na malori mawili yaliyosimama bila kuweka alama za tahadhari...wote tulihamaki."

Nicholaus anasema gari walilokuwamo lilikuwa na abiria sita, watu wazima watano, akiwamo Nicholaus na nduguze wanne, mmoja akiwa ni dereva wao pamoja na mtoto wa miaka miwili, aliyekuwa mtoto wa mmoja wa wadogo zake.

Nicholaus aliyekuwa amekaa kiti cha mbele pamoja na dereva anasema:

"Niliona tukielekea kugongana uso kwa uso na lori kwa kuwa barabara ile ni nyembamba na pembeni ina makorongo ndipo ghafla ili kuepuka kugongana uso kwa uso na Fuso, dereva wetu alijaribu kuhama upande wetu ili akajichomeke katika nafasi ndogo iliyokuwapo upande wa pili (kulia) wa barabara yalipokuwa yamesimama malori mawili na kuacha nafasi kati," anasema na kuongeza:

"Kwa kuwa dereva alikuwa amekata kona kidogo, lile Fuso lilikuja kutugonga ubavuni, katika mlango wa abiria wa nyuma ambako ndipo walikuwapo abiria watatu na mtoto."

Anabainisha kwamba walipogongwa, gari yao ilisukumwa na kwenda kujibamiza katika malori yaliyokuwa yamesimama... hivyo mlango mmoja wa viti vya abiria wa nyuma uligongwa na Fuso na mwingine ukaenda kujigonga katika moja ya lori lililokuwa pembeni.

Anasema alipoteza fahamu kwa dakika takribani 30 kabla ya kuzinduka, na kukuta watu wakiwa wamejaa eneo la tukio na kuwakimbiza hospitali, huku wakielezwa kwamba abiria wa nyuma (wadogo zake na mpwa wake), wamekimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mbeya.

"Hatukuelezwa kuwa ndugu zetu wote wanne wamefariki dunia palepale, mpaka baadaye jioni ndipo tulipofahamishwa," anasema Nicholaus.



Moja ya ajali mbaya iliyowahi kutokea nchini kutokana na kutofuata sheria za usalama barabarani.

> Tuliwazika ndugu zetu na baadaye familia ya bwana harusi na sisi tulikutana kama ndugu, tukazungumza kuhusu suala hili zito lililotutokea.



Magari yakipishana bila kufuata sheria za usalama barabani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### UMUHIMU WA MIKANDA

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), kufunga mkanda wa usalama katika gari humsaidia abiria aliyekaa mbele kujikinga na madhara ya ajali kwa asilimia 40 mpaka 50 na asilimia 50 mpaka 75 kwa abiria aliyekaa viti vya nyuma.

WHO pia inapendekeza watoto wadogo wawekwe katika vizuizi vya watoto, vinavyowafanya wasitupwe au kuhamishwa kitini iwapo ajali itatokea.

Nilimuuliza Nicholaus kama abiria wote walifunga mikanda wakati wa safari, alisema; yeye na dereva walifunga mikanda, na abiria waliokaa kushoto na kulia katika viti vya nyuma walifunga mikanda, lakini bibi harusi aliyekuwa amekaa katikati ya wenzake hakufunga mkanda.

Anabainisha mtoto wa miaka miwili alikuwa amepakatwa tu mikononi na mama yake (Faraja Mwandunga).

"Tuliokuwa mbele tulipona kwa sababu tulifunga mikanda, na gari haikugongwa kwa mbele bali ubavuni kwenye mlango wa viti vya nyuma. Waliokaa mlango wa kushoto na wa kulia nyuma walipata madhara makubwa kwa sababu gari iligongwa mlangoni upande mmoja na upande wa pili wa mlango ukaenda kujibamiza kwenye gari lingine," anasema na kuongeza:

"Ila bibi harusi huenda alipoteza maisha kwa kurushwa na kujigonga kwa kuwa hakufunga mkanda."

Wakati ajali hiyo ikiondoka na uhai wa watu wanne, wawili walionusurika kifo walibaki majeruhi, Nicholaus akiwa ameumia shingo na kuwekewa kishikiza shingo huku dereva Ibrana akiumia mbavu.

Hata hivyo, wote waliruhusiwa kutoka hospitali na kushiriki mazishi ya ndugu zao Mei 20, mwaka huu. Mpaka sasa Nicholaus bado analalamika maumivu ya shingo, hawezi kugeuza shingo nyuma kwa haraka, na hata kwa taratibu hawezi kugeuka sana.

Anasema kifo cha ndugu zake kimewaacha wapweke sana lakini wanamshukuru Mungu kwa wao kulinusurika ili walau waeleze kilichotokea.

Ingawa ana maumivu ya shingo lakini anaweza kumudu kufanya shughuli zake za kila siku za kujiingizia kipato.

Anasema sherehe ya 'send off' ya mdogo wake iliyofanyika Mbeya iligharimu Sh. milioni 7.5, lakini sherehe ya pili waliyopanga kufanya jijini Dar es Salaam, Juni 26, 2019, bajeti yake ilikuwa ya Sh. milioni 32 na tayari Sh. milioni 18 za michango zilishapokelewa.

Nilipomuuliza Nicholaus iwapo michango hiyo ya sherehe ilirejeshwa kwa wachangiaji baada ya kifo cha Diana, alisema wachangiaji waliamua michango ya 'Send off' iwe michango ya rambirambi, na itumike kugharamia msiba na mambo mengine.

"Baadhi ya fedha tulishalipa kwa watoa huduma za chakula, ukumbi, MC na muziki... ni jambo lililowaduwaza hata wao lakini hapakuwa na namna," anasema na kuongeza:

"Tuliwazika ndugu zetu na baadaye familia ya bwana harusi na sisi tulikutana kama ndugu, tukazungumza kuhusu suala hili zito lililotutokea."

Diana, anaelezwa kwamba alikuwa binti mpiganaji kimaisha na mbunifu.

"Baada ya kumaliza kusoma stashahada yake na kutopata ajira, aliamua kuanza biashara akitumia mitandao ya kijamii (Online shopping)," anasema na kuongeza:

"Alikuwa akiuza bidhaa mbalimbali mtandaoni, ikiwamo mchele aliokuwa akiutoa Mbeya na maisha yakamwendea vizuri."

Kwa mujibu wa Ripoti ya WHO ya mwaka 2018, vijana wa miaka 15 mpaka 29 ndio waathirika wakubwa zaidi wa ajali za barabarani, huku ikielezwa kuwa ajali za barabarani zimekuwa zikisababisha vifo vya watu milioni 1.3 kila mwaka na asilimia 30 ya vifo na ajali hizo hutokea katika nchi za dunia ya tatu.

### POLISI

Taarifa za Jeshi la Polisi nchini zinaonyesha kuwa magari binafsi, ndio yanayoongoza kwa kusababisha vifo kutokana na ajali za barabarani kulinganisha na mabasi ya abiria, daladala, malori na pikipiki.

Kwamba kati ya Januari na Juni mwaka 2019, magari binafsi yalipata ajali 528 zilizosababisha vifo 222 na majeruhi 453.

### WADAU

Irene Msellem, mdau wa usalama barabarani ambaye anatoa mtazamo wake kuhusu ajali hizi, akisema magari binafsi yenye uzito chini ya tani 3.5 hayajawekewa ukomo wa mwendo kisheria.

Kwamba yanatakiwa kukimbia kilometa 50 kwa saa katika maeneo ya makazi, lakini maeneo yasiyo na makazi wala vibao vya kuelekeza mwendo, yanaweza kwenda mwendo wowote ambao dereva ataona unafaa.

"Wadau tunapendekeza kuwa kama ilivyo kwa mabasi na magari mengine makubwa yanavyoadhibiwa kwa kuzidisha kilometa 80 kwa saa, uwekwe pia ukomo katika magari binafsi ambao unaweza kuwa kilometa 100 kwa saa," anasisitiza.

Mabadiliko mengine yanayopendekezwa na wadau wa usalama barabarani nchini, ni sheria kuweka ulazima kwa abiria wote wa gari kufunga mikanda ya usalama, tofauti na ilivyo sasa ambapo dereva na abiria wa mbele pekee ndio wanaolazimika kuvaa mkanda katika gari binafsi.

Kama ilivyobainishwa hapo juu, utafiti wa WHO unasema kufunga mkanda humsaidia abiria wa mbele kujikinga na madhara ya ajali kwa asilimia 40 mpaka 50, na asilimia 50 hadi 75 kwa abiria waliokaa viti vya nyuma.

---

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Ijue maana ya uwajibikaji



Watendaji wa wilaya mbalimbali wa Takukuru na viongozi wa asasi za kiraia waliohudhuria kongamano jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

**Na Nickolaus Kasera**

SERIKALI nchini chini ya uongozi wa Rais John Magufuli, imejiwekea lengo kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Lengo hilo zuri linafikwaje?

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, anasema mafanikio hayo ni sharti yabebe mambo makuu mawili; Watanzania tujenge mazoea ya kulipa kodi, pili tuwajibike kila mmoja kwa nafasi yake.

Ni matamshi yake hivi karibuni jijini Dodoma, kwenye kongamano la mafunzo kwa kamati mbalimbali za wabunge, lililoratibiwa na asasi ya kijamii - Wajibu Institute of Public Accountability.

Anatumia mfano wa eneo la Sinza jijini Dar es Salaam, kurejea maendeleo ya nchi na mbinu za ulipaji kodi uwe wa hiari, ukishikwa dhana ni sharti wahusika waone huduma kama barabara zinatengenezwa, pia waridhike na upatikanaji wa huduma nyinginezo za umma.

Rais Magufuli, amekuwa akizungumzia uwajibikaji. Hapana shaka, jitihada za kipekee zinaonekana, akichukua hatua mbalimbali zinazolenga kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za walipa kodi.

Inashuhudiwa kwa kiwango kikubwa sana, ofisi yake imepunguza safari za nje ya nchi. Ni dhihirisho la haja ya umakini mkubwa katika mtazamo wa jumla kupunguza ya kiserikali gharama.

Kurudi kwenye misingi ya utoaji huduma na uwajibikaji, kuna dhamira na jitihada kubwa zenye mifano mingi. Ni kipindi kumeshuhudiwa idadi kubwa ya mawaziri na viongozi waandamizi serikalini, uteuzi wao unatenguliwa kutokana na tuhuma za kutowajibika ipasavyo, hususani kwa wananchi.

Hapo inakuja tafsiri ya kiutawala au kimenejimenti hakuna aliye salama na dhana ya kinachoitwa kitaalamu 'Permanent and Pensionable employment' ikimaanisha ajira za kudumu. Sasa zimeingia katika tafakuri mpya, watu wakibanwa na uwajibikaji.

Ilishawahi kujengeka tabia watu walitumia fursa za uteuzi wa kikazi kinyume, katika nafasi mbalimbali ya sura ambayo wateule walipewa msamiati wa mzaha 'wameula' na sio fursa ya kuwajibika.

Mkurugenzi Mkuu wa Asasi ya Wajibu Institute of Public Accountability, ambaye pia ni CAG mstaafu, Ludovick Utouh, kwa nyakati tofauti ameshazungumzia kwa kina maana halisi ya uwajibikaji kwa Watanzania.

"Katika kipindi changu nilivumbua suala la wafanyakazi hewa kwa zaidi ya miaka minne mfululizo:" Utouh na anahoji kitendawili alichokigundua kwamba: "Fikiria kiasi gani cha pesa kimeokolewa kwa wapokeaji mishahara hewa 19,000 kwenye utumishi?"

Utouh baada ya kustaafu utumishi wa umma, sasa amechukua jukumu tofauti kupitia asasi ya uwajibikaji iitwayo Wajibu Institute of Public Accountability, yenye jukumu analolitafsiri "kujenga ushirikiano mkubwa wa maendeleo endelevu".

Akitoa mafunzo ya dhana ya uwajibikaji, mkufunzi na mwezeshaji wa asasi hiyo, Lawrence Chuma, anasema utawala bora kuwa ni mfumo wa kiungozi na kimchakato, unaofuata utawala wa sheria kwa kuzingatia kanuni bora za haki, usawa na ushiriki wa makundi ya jamii, kuleta maendeleo endelevu.

Anaendelea kwamba utawala bora ni nyenzo muhimu iliyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, akitaja msingi na kanuni zake ni pamoja na utawala wa sheria, demokrasia, ushirikishwaji, maridhiano, uwazi na uwajibikaji.

Anaendelea: "Hata hivyo, uwazi na uwajibikaji, pamoja na ushiriki mpana wa wananchi kwenye shughuli za serikali umekuwa changamoto kubwa."

Serikali kwa kutambua changamoto hiyo, ilikuja na dhana za kitaalamu ziitwazo 'SAM' na 'PETS' ili kuhakikisha uwajibikaji unarejeshwa kwenye mfumo mzima wa utawala bora.

PETS ni kifupi cha 'Public Expenditure Tracking System' kwa maana ya mfumo wa ufuatiliaji matumizi ya rasilimali za umma kwa ngazi mbalimbali, kuanzia zinakotoka serikalini, mashirika binafsi, michango ya wananchi na misaada, hadi kwa mwananchi mtumiaji wa mwisho.

SAM inaanzia ujumbe wa maneno ya lugha ya Kiingereza 'Social Accountability Monitoring.' Ni tafsiri rahisi ya ufuatiliaji uwajibikaji jamii, ikisisitiza misingi na kanuni za haki katika utoaji huduma za kijamii.

Hiyo ni misingi inayohitaji watendaji kutoa taarifa za maamuzi na hatua zilizofanywa na serikali yao na wanawajibika kupokea mrejesho kutoka kwa wananchi.

Zote mbili zinahamasisha ushiriki wa wananchi kumlinda na kutumia vyema rasilimali za umma, kukuza hamasa ya umiliki wa rasilimali za wananchi.

Anataja aina zake ni; kuboresha utoaji huduma stahili; uandaaji mipango shirikishi ya maendeleo; kuboresha uwajibikaji wa viongozi na wananchi kwa ngazi mbalimbali; na kutambua railimali inayovuja.

RIPOTI

# Vita bado chanzo kikubwa ukiukwaji haki za mtoto



Watoto wakiwa darasani Sakassou, Côte d'Ivoire. **PICHA: MTANDAO.**

TANGU kupitishwa kwa Mkataba wa Haki za Mtoto (CRC) miaka 30 iliyopita, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kote duniani, bado vita imesalia kuwa chanzo kikubwa cha ukiukwaji wa haki za mtoto.

Aidha, bado kuna nchi ambazo hazijaridhia mkataba huo, anasema Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres.

Akizungumza kwenye mjadala mkuu wa Baraza Kuu la UN, jijini New York nchini Marekani, Guterres anasema: "Mkataba huo (CRC) unatambua kwamba mtoto ana haki ya kulindwa na kuwa na uhakika wa usalama wake nyumbani, anakoishi na kijijini kwake...ana haki ya kutoa maoni yake na kusikilizwa...mkataba huu ni moja ya mikataba ya UN iliyoridhiwa na nchi nyingi zaidi katika historia," anasema.

Hata hivyo, anasema kuwa kwa nchi ambazo hazijaridhia mkataba huo, zitafanya hivyo mapema.

"Kuchukua au kutochukua hatua kwa serikali kuna athari kubwa kwa watoto kuliko kundi lingine lolote katika jamii... watoto wako katika hatari ya umaskini, njaa, afya duni na maisha wasiyostahili," anasema na kuongeza:

"Lakini kwa juhudi zilizofanyika, haki sasa imedhihirika kwa mamilioni ya watoto, ingawaje hatuwezi kubweteka...tunahitaji kuimarisha juhudi zetu kuhakikisha kwamba watoto wote wako salama, wana afya na wanaweza kutimiza ndoto zao."

Anaongeza, uwezo wa mtoto unaweza kudumazwa kutokana na lishe duni kabla ya umri wa miaka miwili ambalo ndilo tatizo kubwa kwa mamilioni ya watoto, hususan walio katika umri wa kwenda shule, kwani maisha ya mtoto huanza kuandaliwa wakati anaanza shule.

**MAFANIKIO YA MIAKA 30 YA MKATABA WA CRC**

Guterres anasema, kwa kiasi kikubwa mkataba wa haki za mtoto unachagiza hatua kwa sasa, kwani watoto wengi zaidi kuliko wakati mwingine wowote wanapata ulinzi na msaada wanaouhitaji.

Katika kipindi cha miaka 30 iliyopita, vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano vimepungua kwa nusu na pia idadi ya watoto wenye utapiamlo. Katika maeneo mengi, serikali na asasi za kiraia wanashirikiana kutoa msaada kwa watoto walio katika maeneo ya vita, kukomesha ndoa za utotoni na kuwapa watoto hao na vijana sauti katika maamuzi ambayo yanawahusu.

"Miaka 30 iliyopita, mataifa yaliungana pamoja kutoa ahadi kwa watoto wa dunia hii...yaliahidi si tu kutekeleza haki zao, pia kuzidumisha na kuwajibika nazo," anasema.

**YALIYOMO KATIKA CRC**

Mkataba wa CRC unatambua haki za mtoto za afya, dawa na lishe. Haki ya kupata majisafi na usafi, haki ya watoto kupata elimu, kukaa darasani wakiwamo watoto wenye ulemavu na walio katika maeneo ya vita.

**HATUA ZAIDI ZAHITAJIKA**

Guterres anasema pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana, bado juhudi zaidi zinahitajika, kwani mamilioni ya watoto kote duniani wanakabiliwa na njaa, maradhi au hatari, na wengine wanateseka kwa sababu ya dini zao, kabila na au ulemavu wao.

Anafafanua zaidi kuwa watoto walio katika vita wako kwenye hatari ya ukatili wa hali ya juu wa kingono, ambao huwasababishia majeraha ya muda mrefu ya kisaikolojia.

Aidha, anabainisha kwamba watoto ambao ni waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu, wameongezeka kwa zaidi ya mara mbili kutoka mwaka 2004 hadi 2016.

Kwamba wengi wanasafirishwa kwa ajili ya utumwa wa ngono, wanashinikizwa kufanya kazi na kuingizwa vitani kama askari watoto.

"Ni lazima tubadili mwenendo huu, kwani haukubaliki... wasichana ndio wako katika hatari zaidi kuingizwa kwenye ndoa za utotoni, ukatili wa ngono na ukatili mwingine," anasema.

**CHANGAMOTO**

Umoja wa Mataifa unasema changamoto mpya ni pamoja na ongezeko la pengo la usawa na teknolojia ya digitali, ambavyo vinawaweka watoto katika hatari kubwa.

Aidha, unasema watoto wa leo watakabiliwa pia na mtihani mkubwa wa athari za mabadiliko ya tabianchi endapo kizazi hiki kitashindwa kuchukua hatua sasa kuzuia hilo.

"Familia nyingi zinahama sasa kuliko wakati mwingine wowote na watoto wa wahamiaji, ndio walio hatarini zaidi duniani kote," inasema UN.

Naye binti mdogo kutoka Ghana aliyeiwakilisha nchi yake na watoto wote wa Afrika katika mjadala huo anasisitiza:

**VITA**

Guterres asisitiza kwamba vita ni moja ya tishio kubwa kwa utimizaji wa haki za mtoto na vinaongeza ukubwa na vitisho vingine na kwamba amani ndio njia bora zaidi ya kuwalinda watoto.

Hivyo, anazitaka nchi zote wanachama wakati zikiadhimisha miaka 30 ya mkataba huo wa kihistoria, kurejea ahadi zao za kuwapa kipaumbele cha kwanza watoto.

"Nawataka wote kutia saini ombi la kimataifa la kuimarisha ahadi zenu kuhusu mkataba wa haki za mtoto. Kwa pamoja hebu twende kwa kasi ya kufikia yaliyofikiwa kwa miaka 30 iliyopita na zaidi kwa ahadi mpya, kwa kila mtoto, kwa kila haki," anasisitiza. **HABARI UN**

JE, WAJUA?

## Wanasayansi wamegundua sayari 'isiyopaswa' kuwapo

WATAALAMU wa anga wamegundua sayari kubwa ambayo wanasema haipaswi kuwapo, kulingana na nadharia za sasa.

Ulimwengu huo unaofanana na sayari ya Jupita ni mkubwa sana ikilinganishwa na nyota yake mwenyeji, hatua inayokinzana na wazo kuhusu jinsi sayari zinavyoundwa.

Nyota hiyo iliyo umbali wa kilomita trilioni 284, ni nyekundu na ndogo ambayo ni aina ya kawaida katika ulimwengu wetu.

Kundi la kimataifa la wataalamu wa angani, limeripoti matokeo hayo katika jarida la sayansi duniani.

"Inafurahisha kwa sababu tumejiuliza kwa muda mrefu iwapo sayari kubwa kama Jupita na Saturn zinaweza kuunda nyota ndogo kama hizo," anasema Profesa Peter Wheatley wa Chuo Kikuu cha Warwick, Uingereza na kuongeza.

"Nadhani maoni ya jumla yalikuwa kwamba sayari hizi hazikuwapo, lakini hatungeweza kuwa na uhakika kwa sababu nyota ndogo ni dhaifu, suala ambalo linafanya kuwa vigumu kuzifanyia utafiti, ingawa zipo kawaida sana kuliko nyota kama vile jua."

Watafiti walitumia darubini zilizoko Hispania na Marekani kufuatilia kasi ya mvuto wa nyota ambayo inaweza kusababishwa na sayari zinazoizunguka.

Nyota hiyo nyekundu iliyo fupi, ina uzani mzito kuliko sayari yake inayoizunguka kwa jina GJ 3512b, lakini tofauti yao ya ukubwa ni ndogo mno zaidi ya ilivyo kati ya jua na Jupita.

Nyota iliyo mbali ina ukubwa ambao ni mara 270 zaidi ya sayari. Kwa kulinganisha, jua lina ukubwa wa takribani mara 1,050 kuliko Jupita. Wanaanga hutumia kompyuta kuelezea nadharia zao za jinsi sayari huundwa kutoka kwa mawingu, au "diski" za gesi na vumbi zinavyozunguka nyota ndogo.

Kompyuta hizi zinatabiri kwamba sayari nyingi ndogo zinapaswa kukusanyika karibu na nyota ndogo aina ya M.

"Karibu na nyota kama hizo, kunapaswa kuwa na sayari zenye ukubwa wa dunia au ulimwengu mwingine mkubwa zaidi," anasema mwandishi mwenza Christopher Mordasini, Profesa katika Chuo Kikuu cha Bern, Uswizi.

Mfano mmoja halisi wa mfumo wa sayari ambao unaambatana na nadharia ni ule unaozunguka nyota inayojulikana kama Trappist-1. Nyota hii, ambayo iko umbali wa kilomita trilioni 369 kutoka kwa jua, inasimamia mfumo wa sayari saba, zote zilizo na ukubwa sawa na au kidogo kuliko ule wa Dunia.

"Hata hivyo, GJ 3512b ni sayari kubwa ikiwa na ukubwa kama nusu ya Jupiter, na kwa hivyo angalau agizo moja kubwa zaidi kuliko sayari zilizotabiriwa na mifano ya nadharia ya nyota ndogo kama hiyo," anasema Prof. Mordasini.

Matokeo hayo yanatoa changamoto kwa wazo la utengenezaji wa sayari linalojulikana kama kiboreshaji cha msingi.

"Mara kwa mara sisi hufikiria kuhusu sayari kubwa zinazoanza maisha katika barafu, inayozunguka nje kwenye diski ya gesi inayozunguka nyota hiyo ndogo, na kisha hukua kwa kasi kwa kuvutia gesi," anasema Prof .Wheatley.

Lakini waandishi wanasema kwamba diski zinazozunguka nyota ndogo, hazitoi vifaa vya kutosha kwa hili kufanyika.

Badala yake, wanazingatia uwezekano kwamba sayari iliundwa ghafla wakati sehemu ya diski ilipoanguka kwa sababu ya nguvu yake yenyewe. Waandishi wa jarida la Sayansi wanapendekeza kwamba kuanguka huko kunaweza kutokea wakati diski ya gesi na vumbi ina zaidi ya theluthi moja ya ukubwa ya nyota kubwa chini ya hali hizi, athari ya mvuto wa nyota inakuwa haitoshi kuweka diski kuwa thabiti.

Prof. Wheatley aliandika utafiti mwaka 2017 ulioelezea jitu kubwa la gesi liitwalo NGTS-1b, ambalo lilinaswa na darubini zinazoongozwa na Uingereza nchini Chile.

NGTS-1b pia ni kubwa sana ikilinganishwa na ukubwa wa nyota nyingine nyekundu ya M- ambayo iko umbali wa miaka 600 kutoka kwenye mwanga. **BBC**



Sayari kubwa iliyogunduliwa na wataalamu wa anga ambayo wanasema haipaswi kuwapo kulingana na nadharia za sasa. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA DK. RAYMOND MGENI

UCHAMBUZI WA KITABU:

# Gambling Addiction (Uraibu wa michezo ya bahati nasibu)



Michezo ya bahati nasibu mara nyingi inawafanya vijana kuwaza saa zote kuibuka na umilionea. **PICHA: MTANDAO**

URAIBU ni hali ya akili kushindwa kujidhibiti katika ufanyaji wa kitu. Hali hii humfanya mtu akose udhibiti wa mawazo na hisia katika kufanya kitu ambacho kwa uhalisia havutiwi kukifanya.

Eneo athirika zaidi katika udhibiti huu ni eneo la ubongo. Michezo ya bahati nasibu imetengenezwa kwa namna ya kumfanya mtu asipokuwa makini, huishia kuwa katika ngazi ya uraibu.

Kinachotengenezwa ndani ya mtu ni kuwekewa hali ya kujisikia vizuri pindi anaposhinda katika kubahatisha na ile kumbukumbu kumrudisha ajaribu tena na tena.

Kadri anavyojaribu ndivyo anavyojiwekea nafasi ya kuwa mtumwa asiyeweza kujitoa kirahisi.

Michezo ya bahati nasibu imekuwa inachezwa na watu wengi wakiwa na matumaini ya kutengeneza fedha kwa njia ya kubashiri.

Kubashiri kwa kushiriki kucheza katika mashine, michezo mbalimbali kama mpira kunafanya watu waone ni njia ya kuishi kujitengenezea kipato.

Ukiangalia mifumo ya michezo hii, imetengenezwa kuunda matumaini ya kuweza kushinda kunakofanya watu washindwe kuacha kujaribu.

Kuna wakati ambao watu huishiwa fedha kabisa ndipo hupata ufahamu wa namna michezo hii ilivyowamalizia fedha na muda wao.

Ila kwa kuwa ni tabia sugu, wapatapo fedha huirudia tena na tena. Mwandishi atoa mifano ya watu wengi ambao wameingia katika madeni sababu ya kumaliza fedha zote kupitia michezo hii.

Mwandishi anasema watu wengi wameingia kushiriki michezo hii ya kubashiri kwa kukosekana marufuku kutoka kwa tawala za nchi zao.

Hivyo watu wamekuwa wakiona ni njia ambayo imehalalishwa kuwapo na wao wakaweka nguvu kujiingizia kipato.

Kwa kuwa watu hupata usalama huu wa kuonekana ni michezo iliyoruhusiwa, basi hucheza na kushiriki kutwa nzima katika maeneo ambapo watu wanaweza kucheza.

Kwa mfumo huu, kundi kubwa la vijana limejikuta likiwa katika uraibu huu.

Kitendo cha mchezaji wa michezo ya bahati nasibu kuendelea kucheza michezo hii, ndivyo anavyokuwa anasababisha kemikali iitwayo dopamini kumfanya aendelee zaidi.

Kemikali hii kazi yake kubwa ni kumpa mtu hali ya kujisikia raha akifanya kitu. Kwa kuwa kumbukumbu hii hubakia iwe kwa kubashiri na kushinda, humsukuma mtu ajaribu tena na tena kuitafuta ile hali ya kujisikia vizuri.

Na hii haitokei kwa michezo ya bahati nasibu tu inatokea hata kwa aina zingine za uraibu kama kutoacha kuvuta sigara huku mhusika akijua ina madhara, kuangalia picha za utupu akijua zinapelekea kujichua na kuharibika kufikiri.

Au kushinda muda wote mtandaoni akijua ni kupoteza muda au kushiriki mapenzi, mhusika akijua kuna hatari ya magonjwa na kuvunjika mahusiano.

Kampuni kubwa ya uendeshaji michezo ya bahati nasibu kila siku huingiza fedha kupitia wachezaji ambao hawaachi kubashiri kila siku.

Na mifumo ya michezo hii imetengenezwa katika mfumo wa zawadi kuwa ukibashiri mchezo fulani basi utapata zawadi ya kitu fulani.

Kwa kuwa wanajua jinsi akili huvutika na matarajio ya zawadi, basi watu kwa kujua au pasipo kujua hupukutisha fedha katika kucheza huku wakiwa na matumaini ya majaribio ya kushinda.

Na kuna maeneo mengine ya mashine za bahati nasibu, hutoa zawadi kuwa atakayeshinda basi anaweza kupata fedha pamoja na kinywaji fulani.

Hivyo hili huwahamasisha wengi kushiriki kucheza bahati zao. Mwandishi anaelezea namna watu wengine walivyokomba fedha zote katika mashine za kutoa fedha (ATM) ili wajaribu kubashiri.

Mwandishi anaeleza namna michezo ya bahati nasibu inavyoweza kupelekea mtu kuwa na madeni, mahusiano kuvunjika, ulevi na kuharibu maisha.

Mwandishi anaeleza jinsi ambavyo watu waliozoea kucheza sana michezo hii walivyo tayari kukopa ili wakabashiri. Kwa kuwa ni michezo ya bahati nasibu, kuna kukosa na kupata. Inapotokea wengi wanakosa na huku wamepoteza fedha nyingi, hii hupelekea kuwa na msongo wa mawazo.

Matatizo ya madeni na kuwa na msongo wa mawazo kunazaa matatizo mengine ya ulevi. Michezo hii ni matatizo makubwa kwa watu wanapokosa udhibiti kama anavyoshirikisha mwandishi kitabuni.

Watu wengi wanapofikia kuwa na uraibu wa michezo hii, wakiwa na madeni, familia zikiingia katika migogoro, huwa wanashindwa kujieleza vizuri.

Wengi wanaona aibu kueleza kuwa madeni walionayo ni sababu ya kupoteza fedha kupitia michezo hii. Wachache huwa tayari kujieleza kwa wengine ili wapatiwe msaada katika hali za uraibu wao.

Mambo yanapokuwa magumu, msongo wa mawazo ukiwa mkubwa ndipo huwa hawana njia mbadala ya kufanya, isipokuwa kujieleza kuwa wamepoteza fedha zote kwa michezo ya kubahatisha.

> Mtu huendelea kufanya hivyo hadi fedha zote zinapomwishia. Kwa kuwa mtu hubakiwa na kumbukumbu, anaweza kwenda kukopa akiamini kuwa wakati huu akibashiri atapata fedha.

Mwisho mwandishi anaeleza kuwa katika michezo yoyote ile inayohusisha kitendo cha ubahatishaji ni kuwa mwangalifu unapoanza kucheza.

Maana imefanywa kuanza rahisi ila kutoka au kuacha ni ngumu. Kinachokuwa kigumu kuacha ni kuwa mfumo wa akili huwa unajitengenezea au kuchochea hali ya kukuzawadia kemikali ya dopamini pale unaposhinda.

Hali hii inamfanya mtu asukumwe kusema "ngoja nijaribu tena labda nitashinda".

Mtu huendelea kufanya hivyo hadi fedha zote zinapomwishia. Kwa kuwa mtu hubakiwa na kumbukumbu, anaweza kwenda kukopa akiamini kuwa wakati huu akibashiri atapata fedha.

Mzunguko huu huendelea kumfanya mtu kuwa mtumwa wa michezo hii. Njia bora ya kuepuka kitu chochote kile kinachokufanya usijikie vizuri katika majaribio yake kina hatari ya kukufanya uwe mteja.

Hii ndio ishara ambayo unapaswa kuangalia kila unapokuwa unajaribu vitu ambavyo baadaye vinakufanya uwe mtumwa na usiwe huru.

*Mchambuzi ni Dk. Raymond Nusura Mgeni anapatikana kupitia*
*raymondpoet@yahoo.com*
*+255 676 559 211.*
*Dar-es-Salaam.*



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

ZAIDI ya wanafunzi 600 mkoani Dar es Salaam, hawakufanya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi mwaka huu, kutokana na sababu mbalimbali, lakini kubwa ikiwa ni utoro. Wadau wanasemaje?



### MAGANGA JUMA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

UTORO shuleni ni moja ya tishio kubwa la kutotimiza lengo namba nne la Maendeleo Endelevu (SDG) lihusulo elimu, kama halitadhibitiwa nchini. Serikali ilishaamua kulivalia njuga kwa kampeni ya mkoa kwa mkoa na mkono wa sheria.

Kampeni hizo ni za kuihamasisha jamii kuelewa umuhimu wa elimu, kuwafikisha mahakamani wazazi wasiohimiza watoto kwenda shule au wanaowafanyisha watoto wao kazi badala ya kuwapeleka shule na pia maandamano ya amani kama yaliyowahi kufanyika mkoani Tabora yakihusisha viongozi wa serikali, walimu, wazazi na wahusika wakuu ambao ni wanafunzi.

Kimsingi wazazi wana wajibu mkubwa kuhakikisha watoto wao wanahudhuria shule, hivyo wazazi wasiowajibika katika hili wanakumbana na mkono wa sheria. Kukomesha utoro kunaweza kusaidia lengo la elimu kitaifa linatimia kufikia mwaka 2030.

Pamoja na hayo yote, bado kuna haja ya kuboresha mazingira ya kufundishia, kuacha uonevu dhidi ya wanafunzi, walimu kuacha ukali, adhabu zisizo na maana, wafundishe vizuri na wazazi nao wafuatilie na kuwaeleza watoto wao umuhimu wa elimu ili wajue ni nini wanatakiwa kufanya.

Yaani hapa ni kwamba kila upande ukitimiza wajibu vizuri, nina uhakika suala la utoro linaweza kuwa historia nchini.

Inashangaza na inasikitisha kusikia mwanafunzi amehudhuria masomo kwa muda wa miaka saba halafu siku ya mtihani anashindwa kwenda shule kwa sababu ya utoro! Ikiwezekana, kuanzia sasa iwe ni lazima wanafunzi wote kuwekwa kwenye kambi za taaluma mara mtihani wa taifa unapokaribia ili kumaliza tatizo hilo.



### JUDITH MREMI (MWALIMU SEKONDARI YA MNAZI MMOJA DAR ES SALAAM)

KUMEKUWA na sababu nyingi zinazotajwa kuwa chanzo cha utoro wa wanafunzi shuleni, ikiwamo walimu kutokuwa na upendo kwao, kwamba baadhi yao wanakwepa shule kwa kuwa wanakosa matumaini ya upendo kutoka kwa walimu wao.

Sababu inayotajwa ni wazazi kutofuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni na hivyo kutojua kile ambacho watoto hao wanakifanya wanapokuwa shule. Sipingani na sababu hizo, lakini wapo wanafunzi ambao wameshindikana, hata wakisaidiwa kiasi gani hawabadiliki na mwisho wa siku wanakataa shule au kuendelea kuwa watoro hadi wanahitimu elimu ya msingi na hata sekondari.

Unakuta wengine wamefundishwa malezi na maadili mema nyumbani kwao, lakini wanapokutana na makundi ya kihuni wanabadilika na kuwa wabaya.

Hapa sasa ndipo sasa inapokuja dhana ya mzazi kufuatilia maendeleo ya mtoto wake shuleni hata kama amemfundisha mtoto maadili mema kiasi gani, lazima ajue kuwa kuna walimu wengine wa mitaani wanaoweza kumfanya mtoto akaacha kile alichofundishwa nyumbani na kupokea kingine kabisa.

Lakini kwa sababu tatizo la utoro limekuwa likiendelea kuwapo katika shule mbalimbali nchini, basi kuna haja kuwapa semina wazazi, walezi, na viongozi wa shule ili isaidie kuwafanya kila mmoja kujua majukumu yake kuepusha hayo yaliyotokea mkoani Dar es Salaam, kufuatia baadhi ya wanafunzi wa darasa la saba kutofanya mtihani wa taifa wa mwaka huu eti kwa sababu ya utoro, kitu ambacho ni adui wa maendeleo ya elimu nchini.



### SALUM KALI (MWALIMU MSTAAFU, MKAZI WA JIJINI MWANZA)

HAKUNA mwalimu anayefurahia utoro wa wanafunzi ingawa kuna baadhi ya watu huwa wanadai na kulaumu walimu kwamba wanachangia hali hiyo, lakini ukweli ni kwamba mtindo huu unasababishwa na mambo mengi, ikiwamo wazazi kuwaacha watoto wao wawe huru kupita kiasi na mwisho wa siku kujiingiza kwenye makundi yanayowaharibu kwa kuona shule haina maana.

Utoro wa wanafunzi ni moja ya tatizo kubwa linaloikabili sekta ya elimu na hasa katika shule za umma, na chanzo kikubwa nimekitaja kuwa ni baadhi ya wazazi kutofuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni.

Walimu peke yao wakiachiwa kazi ya malezi ni vigumu kumudu wanafunzi, hasa kwa kuzingatia kwamba kila mwanafunzi anakuwa na tabia aliyofundishwa kwao au malezi aliyolelewa. Wapo baadhi ya wanafunzi hawataki kuguswa hata wakifanya kosa kiasi gani na pia wapo baadhi ya wazazi hawataki kusikia watoto wao wameadhibiwa.

Sasa katika mazingira hayo, usitegemee kwamba matatizo yakiwamo ya utoro yanaweza kwisha shuleni. Elimu kwa sasa ni bure, sasa kuna sababu gani ya mwanafunzi kutohudhuria masomo shuleni?

Wazazi wanakuwa wapi hadi watoto wao wanashindwa kufanya mtihani? Niwakumbushe wazazi kwamba shule ya kwanza ya mtoto inaanzia nyumbani, watambue hilo ili kuwasaidia watoto wao, na kikubwa zaidi ni kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni.



### JOHN MASURULI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

DALILI za utoro huwa zinajulikana kwa mzazi kwa kukagua daftari za mtoto wake kila mara, ingawa wapo baadhi wanafunzi hufanya ujanja wa kujisahihishia kwa lengo la kuzuga ili ionekane wanahudhuria shule, kumbe sivyo.

Hata hivyo, nina uhakika kwa mzazi makini anayefuatilia maendeleo ya mtoto wake anajua tiki za mwalimu na hata za kufoji. Kwa hiyo kama mtoto anafanya utundu wa kukwepa shule na kuandika masomo kwa kukopi kutoka katika daftari za wenzake na kujisahihishia, utamgundua tu.

Sisi sote kama wazazi tuna wajibu wa kuhakikisha watoto wetu wanapata elimu kwa kufuatilia maendeleo yao shuleni. Bila kufanya hivyo itakuwa ni sawa na kuruhusu wasisome kwa kushawishiwa na wenzao wakorofi na hatimaye kuhudhurua shule kwa kusuasua au kuacha kabisa.

Kwa mzazi makini ni lazima pia ajue marafiki wa mtoto wake ni wa aina gani anaokuja nao nyumbani kama ni wema au wabaya. Njia hiyo inaweza kumsaidia mzazi kutambua kama mtoto wake amebadilika kitabia au bado anazingatia maadili mema.

Katika kufanikisha hilo, kuna haja ya kutenga muda wa dakika 45 za kukaa na mtoto na kumuuliza amejifunza nini shuleni na kujua matatizo alionayo katika elimu ili kumsaidia kusonga mbele.

Bila kufanya hivyo utoro utaendelea kuwapo na kukwamisha maendeleo ya elimu.



### KULWA JACKSON (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

UKIONA hali kama hiyo ujue tatizo linaanzia nyumbani, hasa kwa wazazi kutofuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni.

Unaweza kukuta mtoto anaishia njiani na kwenda katika vibanda vya kuonyesha video za ngono, ngumi na nyingine nyingi bila mzazi kujua na matokeo yake ni utoro shuleni na hatimaye kukacha mitihani kama ilivyotokea kwa baadhi ya wanafunzi wa Dar es Salaam.

Ikumbukwe kwamba shule nyingi za Dar es Salaam zina wanafunzi wengi, unaweza kukuta mkondo mmoja una wanafunzi hata 300, sasa katika mazingira kama hayo siyo rahisi walimu kufuatilia kila mwanafunzi.

Wanabaki kukazania wenye uwezo mzuri darasani tu na hao wengine wasiojituma wanabaki hawana kitu.

Hivyo ni wajibu wa mzazi au mlezi kufuatilia maendeleo ya mtoto wake shuleni, walimu wasiachiwe kila kitu na inawezekana wapo baadhi ya wanafunzi wanaofukuzwa shule au kupewa barua za wito kupeleka kwa wazazi wao, lakini hawafikishi, badala yake wanaamka asubuhi na kuchukua daftari kana kwamba wanakwenda shule, kumbe wanaishia vijiweni.

Ushauri wangu ni kwamba wazazi watimize wajibu wao na wafanye urafiki na walimu ili kupata taarifa za watoto wao kila siku, kwani mahusiano mazuri miongoni mwao ni jambo la muhimu kwa maendeleo ya kielimu ya wanafunzi.





# 'Wahamiaji' CCM ruksa kugombea serikali mitaa

**Na Nebart Msokwa, BUSOKELO**

CHAMA Cha Mapinduzi wilayani Rungwe kimeonywa kuwanyanyapaa wanachama wapya wanaohamia ndani ya CCM wakitokea vyama vya upinzani wakati wa mchakato wa uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji uliopangwa kufanyika mwezi ujio.

Katibu wa CCM Wilaya ya Rungwe, Clemence Mponzi, alitoa ushauri huo jana wakati akimpokea aliyekuwa Mwenyekiti wa Kijiji Kandete kwa tiketi ya Chadema, Danfor Mwambapa aliyehamia CCM.

Alisema kuwa endapo wanachama hao wapya watakuwa na sifa, kulingana na miongozo ya CCM wateuliwe kugombea kwenye nafasi yoyote ya uongozi waliyoiomba ili wagombee kwa tiketi ya chama tawala.

"Kila mwanachama ana haki na hadhi sawa ndani ya CCM, hawa wenzetu tukishawakabidhi kadi za CCM wanakuwa ni wanachama wenye hadhi sawa na wengine, hivyo wakiamua kuchukua fomu za kugombea uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa wapeni na wakiwa na sifa wapitisheni bila masharti," alisema Mponzi.

Alisema kuwa anaamini kuwa wanachama wanaorejea ndani ya CCM ni wana-CCM wa zamani ambao walihamia vyama vya upinzani kwa sababu mbalimbali kutokana na mazingira ya wakati huo.

Akimkabidhi kadi ya CCM, Mbunge wa Busokelo, Atupele Mwakibete, alisema kuwa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na vijiji wana-CCM wanahitaji zaidi umoja ili waweze kupata ushindi wa kishindo.

Aliwaonya wanasiasa wanaoanza siasa za kuwagawa wananchi wa Busokelo kwa madai kuwa madhara yake yanaathiri hata maendeleo makubwa ambayo yameshafanyika ndani ya jimbo hilo.

Mwenyekiti wa Chadema Kijiji cha Kandete aliyerudi CCM, Darnford Mwambapa, alisema ameamua kurejea CCM baada ya kuona chama chini ya uongozi wa Rais John Magufuli sasa kimejijengea misingi imara ya haki inayopinga rushwa na inayozingatia uadilifu.



Wananchi wa Kijiji cha Ntokela katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wakiendelea na biashara ya viazi pembezoni mwa barabara kuu ya Tanzania na Malawi jana, eneo ambalo ni hatari kwa maisha yao kutokana na kuwa na mteremko mkali. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kampeni ya kusafisha Bonde la Rukwa yaanza

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BODI ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa, imeanzisha kampeni mahsusi ya kufanya usafi kwenye vyanzo vya Mto Nzovwe kwa kuwashirikisha wananchi pamoja na shule mbalimbali za msingi na sekondari za jiji la Mbeya, kukabili changamoto za uchafunzi wa mazingira na upotevu wa maji.

Kampeni hiyo ilizinduliwa juzi katika kiwanja cha Shule ya Msingi Mumvwa kilichopo kata ya Mshewe wilayani Mbeya na bodi hiyo kwa kushirikiana na viongozi mbalimbali wa serikali.

Kampeni hiyo ilitanguliwa na watu wote kushiriki kufanya usafi kwenye Mto Nzovwe kwa kuondoa taka za mifuko ya plastiki na chupa ambazo zinaelezwa kuwa hatari kwa viumbe hai.

Mkurugenzi wa Bodi, Grace Chitanda, alisema waliamua kuanzisha kampeni hiyo ili kuwaelimisha wananchi waache tabia za kutupa taka ngumu kwenye mto huo ambao ni muhimu kwa maisha ya viumbe hai na matumizi ya wananchi.

Alisema katika kampeni hiyo wanashirikiana na shule za msingi na sekondari 13 za Jiji la Mbeya ambazo zipo pembezoni mwa Mto Nzovwe pamoja na wananchi wa vijiji na mitaa yote ambayo ipo pembezoni mwa mto huo.

Vilevile alisema kampeni hiyo itawaelimisha wananchi kuwa na matumizi sahihi ya maji ili kuwe na mtiririko endelevu wa maji mtoni humo ambao unamwaga maji yake ndani ya Ziwa Rukwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Salum Manyata, ambaye alihudhuria hafla hiyo alisema uchafuzi wa maji ni hatari kutokana na kusababisha milipuko ya magonjwa ambayo ni hatari kwa maisha.

Alisema asilimia 60 ya magonjwa ya binadamu yanatokana na matumizi ya maji yasiyokuwa salama na kwamba kampeni hiyo ni muhimu katika kuiamsha jamii kulinda afya yake.

"Kuna changamoto kubwa sana ya uchafuzi wa vyanzo vya maji, hali hii inasababisha ongezeko la magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na kuhara matumbo. Ni wakati sahihi kwa wananchi kupatiwa elimu ili wajue chanzo cha magonjwa hayo," alisema Dk. Manyata.

Baadhi ya wanafunzi walioshiriki kwenye kampeni hiyo, waliiomba serikali kuzisaidia shule kuwa na vikundi imara vya mazingira ili kukabiliana na uchafuzi wa mazingira na kusambaza elimu ya mazingira kwa wananchi.


CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz


# Kampuni tumbaku yaacha majonzi

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

BAADHI ya wakulima wa tumbaku wilayani Chunya katika mkoa wa Mbeya, wapo hatirini kukosa masoko kutokana na moja ya kampuni wanunuzi kujitoa.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Jimbo la Lupa (CCM), Victor Mwambalaswa, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani cha kupitia mapato na matumizi ya halmashauri hiyo na kupitisha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mwambalaswa alisema kampuni iliyojitoa ni TLTC na kwamba kitendo cha kujiondoa kutafanya biashara na kusababisha baadhi ya wakulima walioko kwenye vyama vya ushirika vilivyokuwa vinaiuzia kukosa soko.

Alisema hali hiyo inaweza ikahatarisha uchumi wa wananchi hao kwa kuwa madai kuwa asilimia kubwa ya maisha yao hutegemea tumbaku.

"Chunya tuna kampuni mbili zinazonunua tumbaku, na sasa kampuni ya TLTC imejitoa kununua zao hilo, tumebakiwa na Premium, hivyo wakulima waliokuwa wakilima na kuliuzia kampuni iliyojiondoa hawatalima mwaka huu hali ambayo itateteresha uchumi wao," alisema Mwambalaswa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, alisema kutokana na taarifa za kampuni kujitoa, wakulima wanatakiwa kulima mazao mbadala yatakayoweza kuwasaidia katika kuinua uchumi wao.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, TLTC imejitoa kwa kununua tumbaku nchi nzima na sio kwa Wilaya ya Chunya pekee hivyo kuwataka wakulima wawe wavumilivu kwa kipindi hiki wakati serikali ikilitafutia ufumbuzi suala hilo.





## 'Wizi wa mitihani unakwaza elimu'

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema wizi wa mitihani ni jambo linalo poromosha elimu ya Tanzania na kuwaonya walimu kutojihusisha na vitendo hivyo.

Jafo alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa kwanza wa wenyeviti wa walimu wakuu wa shule za msingi Tanzania Bara.

Alisema wizi wa mitihani sio sifa njema kwa Taifa, hivyo wahakikishe wanasimamia kanuni na weledi kwenye masuala ya mitihani.

"Nidhamu katika usimamizi wa mitihani kwa sasa imerudi nikupongeze sana Msonde kwa hili, ukifanya wizi wa mitihani jambo hili lina gharama kubwa kwa Taifa," alisema.

Aliongeza: "Niwasihi nyinyi mliopewa dhamana katika hili, nendeni mkafanye compliers (utekelezaji) suala zima kwa kuzingatia kanuni na kusimamia weledi."

Alibainisha kuwa mwaka huu ofisi yake itatoa tuzo ya ufanyaji vizuri wa mitihani ili kuleta motisha kwa walimu.

Aidha, alisema uimarishaji wa miundombinu umekuwa ni mkubwa ambapo lengo la Rais ni kuhakikisha watoto wote wanapata fursa ya elimu na kusoma katika mazingira mazuri.

Alisema pamoja na fedha zinazotolewa kwa ajili ya elimu bila malipo, pia serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 305.1 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ikiwamo ujenzi wa nyumba za walimu, madarasa, matundu ya vyoo, maabara na maboma.

Waziri Jafo alisema mwaka huu serikali imetenga Sh. bilioni 288.247 kwa ajili ya elimu bila ya malipo.

"Ajenda ya elimu kwa sasa inaenda kwa kasi sana, bajeti ya mwaka huu tumetenga Sh. bilioni 288.247, katika programu ya elimu bila malipo na kutoa zaidi ya Sh. bilioni 24 kila mwezi, ikiwamo Sh. bilioni 3.2 ambazo ni kwa ajili ya posho za walimu.

Hata hivyo, alisema kutokana na wanafunzi kusoma kwenye shule za kata za serikali, baadhi ya shule zimeanza kusaka wateja wa kununua shule zao kutokana na kukosa wanafunzi.

"Shule ambazo zinafanya biashara badala ya kutoa elimu zimeanza kujitoa zenyewe, ndio maana kuna mtu anakuja nataka kuuza shule yangu, amekosa wanafunzi kwa kuwa wengine walikuwa hata hawana walimu wazuri," alisema.

Kuhusu maboresho ya shule kongwe, Jafo alisema walibainisha shule kongwe 89 ambazo zilikuwa katika hali mbaya na kuwa mpaka sasa shule 43 tayari zimekabilika kufanyiwa maboresho huku zilizobaki zikiwa katika hatua mbalimbali ya kuboreshwa.

Aidha, Jafo amewataka wakuu wao kuhakikisha wanasimamia fedha zinazopelekwa katika maeneo yao na kusisitiza kuwa Tamisemi haina masihara na usimamizi wa fedha za umma.

Pia amewasihi walimu wakuu hao kujiepusha na rushwa ya aina yoyote ili kuwezesha elimu kupiga hatua zaidi.

# Kiwanda mvinyo Chamwino sasa kuzalisha ajira 572

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

KUFUATIA Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Chamwino kuridhia kuuza ekari 400 kwa ajili ya uwekezaji wa kiwanda cha kusindika mvinyo, inatarajiwa kutoa ajira 572.

Kampuni ya Mega Beverages Co.LTD ya jijini Arusha ndiyo itafanya uwekezaji huo, ambapo ujenzi wake unatarajiwa kuanza hivi karibuni na utakamilika mwaka 2020.

Akitoa taarifa kwa madiwani katika kikao maalum, Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Athuman Masasi, alisema ekari hizo zipo katika Kijiji cha Chinangali ambapo mwekezaji huyo ameuziwa kwa kiasi cha Sh. milioni 200.

Aidha, alisema kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kutoa ajira rasmi 52 na zisizo rasmi zaidi 520, hivyo kuweza kutimiza azma ya halmashauri ya kuelekea uchumi wa viwanda.

"Kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuchakata zabibu tani 2,750 ambazo zitakuwa na uwezo wa kuzalisha mvinyo wa zabibu zaidi ya lita milioni mbili kwa mwaka," alisema.

Alisema kuwapo kwa kiwanda hicho kutaweza kufungua soko la zabibu na kuchochea kilimo kutoka kwa wakulima wadogo wadogo ambao kwa muda mrefu wamekosa soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

"Napenda kuliweka wazi jambo hili kwenu nyinyi madiwani pamoja na mwekezaji kujenga kiwanda hicho pia ameahidi kujenga miundombinu ya sekta mbalimbali kama vile ya afya, elimu, maji, kilimo, mifugo na uvuvi endapo kitakuwa na uhitaji katika maeneo ya jirani na uwekezaji utakapofanyika," alisema.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Samweli Kawea, alisema kuwa kupatikana kwa mwekezaji huyo kutaongeza ajira kwa wananchi na wakulima waliopo jirani kwa kuwa watapata soko la kuuza zabibu katika kiwanda hicho.



Mchungaji Hamprey Sam (kulia), wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Mtaa wa Kisasa Dayosisi ya Dodoma akiwagawia zawadi ya vifaa vya shule watoto katika sherehe iliyofanyika kanisani hapo juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wafugaji Mpwapwa watakiwa kumiliki mashamba ya malisho

**Na Renatha Msungu, MPWAPWA**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imewaagiza wafugaji kumiliki ardhi ya kutosha kupitia halmashauri zao kwa ajili ya mashamba ya malisho ili kuepusha migogoro baina yao na wakulima.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani wa wizara hiyo, Dk. Angello Mwillawa, katika mafunzo ya wataalamu wa malisho yaliyofanyika katika Chuo cha mifugo LITA kilichopo Mpwapwa.

Dk. Mwillawa alisema wafugaji wanapaswa kumiliki ardhi ya kutosha kupitia halmashauri za vijiji vyao ili kupunguza migogoro ya kugombea maeneo ya malisho.

Alisema wanakila sababu ya kuwa na maeneo hayo kwa ajili ya kupanda malisho ili ufugaji uwe wenye tija na utakaowasaidia kuongeza kipato katika kaya husika.

"Tunahimiza wafugaji kumiliki ardhi ya kutosha kihalali katika vijiji vyao lengo ni kuona migogoro ya ardhi dhidi yao inakwisha, lakini ufugaji uwe wa tija wa kisasa," alisema Dk. Mwillawa.

Alisema faida za kumiliki ardhi ya kutosha itawasaidia kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa malisho ya mifugo katika kipindi cha mwaka mzima, kuboresha ubora wa chakula cha mifugo, kutunza ubora wa udongo, ikiwamo kuzuia mmomonyoko na upotevu wa udongo wenye rutuba. Alieleza wizara imeweka mkazo mkubwa katika utoaji elimu ya upandaji, utunzaji, uvunaji, hifadhi za malisho, ulishaji na uvunaji wa mbegu za malisho ni kutaka kuboresha sekta hiyo kutokana na umuhimu wake.

Alisema kwa kuzingatia umuhimu wa malisho kwa mifugo, wizara imeamua kuweka mkazo wa uzalishaji malisho kwa kutoa mafunzo ambayo yanazingatia sekta hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema wafugaji na wadau wa malisho wanapaswa kuchukua dhana hiyo ya ustawishaji ili kuhakikisha malisho yanapatikana kwa mifugo katika misimu yote ya mwaka.

Naye Mkuu wa Chuo cha Lita Mpwapwa, Moses Mlahagwa, aliipongeza wizara kwa kutoa mafunzo hayo kwa wataalamu wa malisho ambayo yatasaidia kuwajengea zaidi ikiwamo kuwakumbusha jukumu lao katika sekta ya malisho.

Alisema wataalamu wa malisho wanapaswa kujua nini umuhimu wao katika suala zima la elimu ya upandaji wa malisho jambo ambalo litachangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza ugomvi baina ya wakulima na wafugaji.



# Pilipili kichaa kuinua vijana

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, amewataka vijana kujitegemea na kubadili mitizamo ya kufikiria kuajiriwa serikalini pekee.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na vijana wa Wilaya za Kaskazini B Unguja na Kati waliomo katika mradi wa kilimo biashara cha pilipili kichaa katika shamba darasa.

Shamba hilo lipo katika Kijiji cha Panga Tupu Kaskazini Unguja na Bambi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema umefika wakati sasa kwa vijana kubadili fikra na mawazo ambayo wengi wao wanatamani kuwa mabaharia, wanajeshi au polisi.

Aliitaka Wizara ya Vijana kutoa elimu kwa vijana ili kubadili mawazo ya kutegemea ajira kutoka serikalini na badala yake wajielekeze katika kilimo cha kibiashara.

Alisema kilimo biashara cha pilipili kichaa ni kizuri ambapo mahitaji ya soko ni kubwa na kilimo hicho hakina gharama kubwa ikilinganishwa na kilimo kingine.

"Soko la pilipili kichaa lipo tena ni la uhakika, hivyo vijana niwaombe kuchangamkia fursa hiyo ili kuweza kupata maendeleo," alisema Waziri.

Balozi Amina alieleza kuwa miaka ya nyuma Zanzibar ilikuwa ni mzalishaji mkubwa wa pilipili kichaa na ilikuwa ikisafirisha nje ya nchi, lakini baada ya soko la bidhaa hiyo kuanguka wananchi wakaacha kulima kilimo hicho na uzalishaji wake haukuwa mkubwa.

Kwa upande wake Said Seif Mzee, Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC), alisema malengo ya mradi huo wa kilimo cha pilipili kichaa ni kujiweka katika kilimo cha kibiashara kwani kwa muda mrefu wananchi wa Zanzibar wanalima lakini hawalimi kilimo cha biashara.

Aidha, aliwataka vijana wajitahidi kwenda katika kilimo cha biashara hasa kwa kilimo cha viungo ambacho kinasoko zuri na kuweza kujisaidia kiuchumi.

"Lengo la serikali kuanzisha mradi huu ni kuwasaidia vijana kupata ajira kwani vijana wanapokuwa na ajira vitendo vingi vya uhalifu hupungua," alisema.

Mtaalamu wa kilimo cha pilipili kichaa, Josephat Ligondo, kutoka kampuni ya Vegrab Organic Farming ya Dar es Salaam, alisema zao hilo si geni na lilikuwapo miaka mingi lakini lilipotea kwa sababu ya kukosa soko na uzalishaji kupungua.

Alisema hivi sasa soko la zao hilo limerudi na kuwataka vijana hao kufanya bidii katika kilimo hicho ili kuendana na kasi ya soko la zao hilo.

"Kilimo hiki kina faida sana kwanza mmea unahimili magonjwa, unakupa miaka mitatu ya mavuno bila ya wasiwasi na unakupa muda mwingi wa kupata kipato," alisema mtaalamu huyo.

Alieleza kuwa katika shamba la Kijiji cha Panga Tupu wamelima heka 15 na kupanda zao hilo ambapo kila eka moja inatoa wastani wa miche 10,000 na iwapo itakua vizuri vijana wa eneo hilo watakuwa na uhakika wa kuvuna kilo 600 kwa mwezi ambapo bei yake ni Sh. 2,000,000.

Kwa upande wao vijana kutoka mabaraza ya vijana wa mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja ambao ndiyo walengwa wa mradi huo, waliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuwapatia mradi huo wakiita kuwa ni neema kubwa kwao.

"Tuna imani kuwa kile kilio cha vijana wengi cha kutokuwa na ajira sasa kitapungua kwa sababu mradi huu wa kilimo biashara ni mkombozi kwetu sisi vijana," alisema Shein Khamis Mohd.

Mohd ambaye ni Mwenyekiti wa Mabaraza la Vijana Wilaya ya Kaskazini B Unguja.



Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali (wa nne kulia), akipata maelezo kutoka kwa mtaalamu wa kilimo cha pilipili kichaa, Josephat Ligondo (wa pili kulia), wakati alipotembelea mradi wa vijana wa kilimo biashara cha pilipili kichaa huko Kijiji cha Panga Tupu, Kaskazini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wasafirisha miti dawa kinyemela waonywa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKAILI imeeleza umuhimu wa hifadhi ya misitu Zanzibar na kukumbusha kuwa ina hazina kubwa ya miti dawa na kuwaonya wanaouza dawa hizo nje bila vibali.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Dk. Makame Ali Ussi, alieleza hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni, Shehe Hamad Mattar.

Mattar aliuliza suala hilo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi akitaka kujua wizara inafahamu kuwa baadhi ya dawa za asili zinasafirishwa nje ya nchi.

Naibu Waziri huyo alisema wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakitumia dawa hizo kwa karne nyingi na serikali inafahamu kuwa hivi sasa zipo juhudi kubwa zinazofanywa na Wizara ya Afya kwa kufanya utafiti wa dawa zinazotaka na miti ya asili.

Alieleza kuwa katika kutekeleza azma hiyo, serikali ilipokea ombi kutoka Wizara ya Afya kitengo cha dawa asili kutaka kufanya utafiti wa dawa hizo kutoka katika misitu ya hifadhi.

"Wizara yangu tayari imeshatoa ruhusa kwa wataalamu kuchukua sampuli ya majani na mizizi ya miti ya asili wanayohitaji kwa ajili ya utafiti huo," alisema.

Aidha, alieleza kuwa wizara yake haijapokea maombi ya kusafirisha mimea au dawa ya asili kwenda nje ya nchi na wala haijatoa kibali cha usafirishaji.

Aliongeza: "Napenda kuwasihi wananchi ikiwa wanafanya biashara hiyo waache kusafirisha na kuendelea kufanya hivyo ni kinyume na utaratibu wa sheria za nchi."

Alieleza kuwa suala la dawa linasimamiwa kisheria na Wizara ya Afya na hivyo watashirikiana kuhakikisha kwamba maliasili hizo za dawa hazisafirishwi nje ya nchi kinyume na sheria.

# Kodi kujenga bandari Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi kukamilisha miradi mitatu mikubwa ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri na jengo la abiria la uwanja wa ndege wa Zanzibar kwa fedha za makusanyo ya ndani.

Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sirra Ubwa Mamboya, aliyasema hayo akijibu taarifa ya Kamati ya Mawasiliano na Usafiri ya Baraza la Wawakilishi.

Alisema mradi wa ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka 2015-2020.

Alisema mradi huo umezorota kutokana na kukosa fedha za wahisani pamoja na taasisi za fedha za kimataifa.

''Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaahidi kugharamia ujenzi huo wa jengo la abiria la uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume licha ya kukosa fedha kutoka kwa taasisi za fedha na kibenki,'' alisema Mamboya.

Aidha, aliutaja mradi mwingine wa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri huko Maruhubi kwamba utajengwa kwa kutumia fedha za ndani.

Alisema mahitaji ya bandari nyingine yapo kutokana na bandari iliyopo sasa ya Malindi kuzidiwa na msongamano mkubwa wa shehena kama makasha au makontena.

''Tunakusudia kujenga bandari mpya ya Mpigaduri kwa kutumia fedha za ndani ambazo zinatokana na makusanyo ya kodi,'' alisema Mamboya.

Aidha, alisema mradi wa ujenzi wa barabara ya Ole Kengeja, utajengwa kwa kutumia fedha za ndani pia kazi itakayofanyika katika kipindi cha mwaka huu wa fedha 2019-2020.

Alisema hayo kufuatia baadhi ya wawakilishi wengi kutoka Pemba kutaka kupata ufafanuzi kuhusu barabara hiyo ambayo ujenzi wake umekwama kwa zaidi ya miaka miwili sasa licha ya serikali kutoa ahadi.

Mwakilishi wa Jimbo la Chakechake Suleiman Sarhani, pamoja na mwingine kutoka Jimbo la Mgogoni Shekhe Hamad Mattar, aliitaka serikali kujenga barabara hiyo muhimu kiungo cha wakulima wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kutumia fedha za ndani.

# Mwenge kuipa fursa Mtwara

**Na Hamisi Nasiri, NANYUMBU**

JUMLA ya miradi 69 yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 27.8 inatarajiwa kuzinduliwa, kukaguliwa na kuwekwa mawe ya msingi mkoani Mtwara katika mbio za Mwenge wa Uhuru 2019.

Miradi hiyo ni ya sekta mbalimbali ikiwamo ujenzi, biashara, afya na maji na kwamba itatembelewa na mbio hizo katika halmashauri tisa za Mkoa wa Mtwara kuanzia juzi.

Akizungumza katika kijiji cha Lumesule wilayani Nanyumbu wakati akipokea Mwenge huo kutoka Mkoa wa Ruvuma, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, alisema miradi 69 yenye thamani ya Sh. bilioni 27.8 itafunguliwa, kukaguliwa na kuwekwa mawe ya msingi na kwamba katika miradi hiyo wananchi wamechangia asilimia 6.3

Byakanwa alieleza kuwa halmashauri zimechangia asilimia 6.4, Serikali Kuu imechangia asilimia 49, washirika wa maendeleo wamechangia asilimia 38.1, huku elimu ya kujitegemea imechangia asilimia 0.1.

Alisema Mwenge wa Uhuru utaweka mawe ya msingi katika miradi 11, kufungua miradi 12, kuzindua miradi 11, kuona na kukagua miradi 35 inayotekelezwa na wananchi kwa kushirikiana na serikali, washirika wa maendeleo na halmashauri.

"Tunaahidi kushirikiana vema na wakimbiza Mwenge kitaifa kwa kipindi chote watakachokuwa ndani ya mkoa wetu wa Mtwara karibuni sana," alisema Byakanwa.

Byakanwa alisema mbio za Mwenge mkoani humo zitawakumbusha kuwa maji ni hali yao ya msingi, hivyo wananchi wanapaswa kulinda vyanzo vya maji kwenye maeneo yao.

Aidha, Byakanwa alisema Mkoa wa Mtwara hauko mbali katika kutekeleza sera mbalimbali zinazolenga kuboresha huduma mbalimbali za kijamii ikiwamo maji na afya.

Alisema pia mkoa huo unaendelea na mapambano dhidi ya vitendo vya kutoa na kupokea rushwa, hivyo kupitia mbio za Mwenge, elimu itaendelea kutolewa kwa jamii.

Kadhalika Byakanwa alisema mkoa wake utaendelea kupambana na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) pamoja na ugonjwa na malaria ili kupunguza kiwango cha maambukizi ya magonjwa hayo.

# Afungwa maisha jela kwa kubaka, kulawiti mtoto

**Na Said Hamdani, LINDI**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Lindi mkoani hapa, imemuhukumu kifungo cha maisha jela Emmanuel Thomas Msemakweli (29), mkazi wa Kata ya Rasbura, Manispaa ya Lindi, baada ya kukutwa na hatia ya makosa mawili, likiwamo la kulawiti.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Franco Kiswaga, baada ya mshtakiwa kukutwa na makosa mawili likiwamo kubaka na kulawiti mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 10 (jina limehifadhiwa).

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Kiswaga alimuuliza mshtakiwa kwa nini mahakama isimpe adhabu kali kutokana na makosa aliyoyafanya dhidi ya mlalamikaji.

Akijitetea, aliomba mahakama imwonee huruma kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza, na alifanya kosa hilo baada ya kupitiwa na ibilisi.

Baada ya utetezi huo, Mwanasheria wa Serikali, Yahaya Gumbo akisaidiana na Godfrey Mramba, waliiomba mahakama kumpa mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwake na wengine walio na tabia ya aina hiyo.

Hakimu Kiswaga baada ya kusikiliza maombi ya pande zote mbili, alisema anakubaliana na maombi yao, lakini kutokana na Sheria kumfunga mikono, huku akitumia vifungu 130 (1),(2) (a) na 131 (1) kanuni ya adhabu sura ya 16/2002 kutoa adhabu, alimuhukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 kwa kosa la kubaka.

Pia Hakimu Kiswaga akitumia kifungu namba 154 (1) (a) kanuni hiyo ya adhabu sura ya 16/2002 katika kesi hiyo namba 37/2019 kwa kumhukumu kifungo cha maisha na kwa kuwa adhabu zote zinakwenda kwa pamoja, Msemakweli atalazimika kuishi gerezani maisha.

Awali ilidaiwa mahakamani hapo na wanasheria wa serikali, Gumbo na Mramba, kuwa mshtakiwa kwa muda, siku na nyakati tafauti, huku akifahamu anachokifanya ni makosa, alimbaka mtoto huyo (jina likiwamo la shule anayosoma limehifadhiwa).

Wanasheria hao waliiambia mahakama kuwa hali hiyo ilibainika baada ya walimu wake na mama yake kuona mabadiliko, yakiwamo utembeaji wake na kushuka kwa maendeleo yake shuleni.

Aidha, walieleza kufuatia hali hiyo, walimu na mzazi wake walimuhoji na kuelezea kile kinachomsibu, kisha kuchukua hatua ya kumpeleka hospitali kufanyiwa uchunguzi wa kitaalamu na kubainika kuingiliwa kinyume cha maumbile.

Wanasheria hao walieleza kuwa baada ya kubaini hilo, walimu wakishirikiana na mama wa mwanafunzi huyo walitoa taarifa kwa vyombo husika vya serikali, ndipo mshtakiwa alipofuatwa na kukamatwa.



Mchuuzi wa mihogo ya kukaanga, akifanya shughuli zake katika mazingira yasiyo salama kiafya katika eneo la Manzese, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wadau wa TPSF waunga mkono mwongozo kuchochea uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

MWONGOZO wa kufanya maboresho ya kanuni juu ya ufanyaji biashara nchini (Blueprint), umeungwa mkono na wanachama na wadau wa sekta binafsi (TPSF) kwani utachochea zaidi wawekezaji kuja kuwekeza nchini.

Mpango huo ulioasisiwa na wadau wa sekta binafsi na mapendekezo yake kupelekwa serikalini tangu mwaka 2010 sasa upo katika hatua nzuri ya utekelezaji, ambapo serikali imeamua kuutengenezea sheria ambayo imetajwa kuja kuwa mwarobaini kwa ustawi wa sekta binafsi na za umma.

Akizungumza katika Mkutano wa 19 wa mwaka wa TPSF jijini Dar es Salaam, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alisema kuwa katika kutekeleza mpango huo serikali imeshachukua hatua kadhaa ikiwamo kujenga miundombinu ya barabara, reli na kuboresha bandari pamoja na viwanja ya ndege.

"Serikali imeamua mambo yaende na wote ni mashuhuda, tumeanza kuweka mazingira rafiki kwa kujenga miundombinu itakayochochea uwekezaji na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa kutoka maeneo ya uzalishaji na kuunganishwa na masoko ya ndani na nje ya nchi," alisema Kairuki.

Aliongeza kuwa katika kutekeleza mpango huo serikali imefuta tozo na ada takribani 54 sambamba na kuunganisha baadhi ya majukumu ya taasisi za udhibiti kama vile kuhamisha masuala ya chakula kutoka TFDA kwenda TBS.

"Kama serikali tunaendelea kuchambua na kufanya mapitio ya sera na sheria ambazo zimekuwa kikwazo kwa ukuaji wa sekta binafsi lengo likiwa ni kupunguza changamoto zilizopo katika uwekezaji ili kufikia azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPSF, Salum Shamte, alipongeza hatua zinazoendelea kuchukuliwa na serikali katika kuifanya sekta binafsi iwe imara na yenye tija hapa nchini.

"Blueprint ni mpango ulioasisiwa na wadau wa sekta binafsi kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo kwenye sekta hii, leo tunapoona wenzetu serikalini wakifanyia kazi mawazo yetu kwa kweli inatupa faraja na hatuna sababu ya kuacha kupongeza juhudi hizo," alisema Shamte.

Alisema kuwa jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na serikali zikiwa zitatungiwa kanuni na sheria zitazidi kuitoa sekta binafsi kutoka ilipo na kuwa yenye tija zaidi kwa kuvutia uwekezaji na kuongeza ajira.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, aliumwagia sifa mpango huo ambao kikao kijacho cha Bunge utaujadili na kupitisha kuwa sheria hali ambayo itasaidia kuwavuta wawekezaji kuja kuwekeza nchini.

# Al-Shabab yaipiga kambi ya Amerika

**MOGADISHU,** Somalia

WAPIGANAJI wa Jihadi wameshambulia ngome ya kijeshi inayotumiwa na askari wa Marekani kutoa mafunzo kwa makomando nchini Somalia na kujeruhi kadhaa.

Majirani wa eneo hilo waliripoti kusikia milipuko mizito na milio ya risasi katika uwanja wa ndege wa Baledogle Kusini mwa Jimbo la Lower Shabelle kwenye kambi hiyo.

Kikundi cha wanamgambo wa al-Shabab kimesema ndicho kilichofanya shambulio hilo, kikitumia mabomu ya kutegwa ndani ya gari kulipua milango kabla ya kuwatuma wapiganaji wake ndani ya ngome hiyo.

**Baada ya kuvunja uzio wa ngome hiyo yenye ulinzi mkali Mujahideen hao walivamia majengo ya ngome hiyo na kukabiliana na wanajeshi katika mapigano makali.**

Maofisa wa kijeshi walisema wapiganaji hao wamerudishwa nyuma na pia Al-Shabab, imesema katika taarifa yake kwamba ilifanya uvamizi huo na kwamba ulikuwa ukiendelea.

"Baada ya kuvunja uzio wa ngome hiyo yenye ulinzi mkali, Mujahideen hao walivamia majengo ya ngome hiyo na kukabiliana na wanajeshi katika mapigano makali."

Ngome hiyo iko umbali wa takribani kilometa 100 magharibi mwa mji mkuu wa Somalia Mogadishu na inaaminiwa kuwa ni makazi ya kikosi maalum cha Marekani, Somalia na walinda amani wa Uganda.

Aidha, hutumiwa kama kituo cha mashambulizi ya ndege za Marekani zisizo na rubani pamoja na kituo cha mafunzo ya kijeshi yanayotolewa na Marekani nchini Somalia. Kadhalika katika tukio jingine, msafara wa jeshi la Italia ulipigwa na mlipuko mjini Mogadishu, ilisema Wizara ya Ulinzi ya Italia. Hakuna majeruhi walioripotiwa katika shambulio hilo.

Marekani iliongeza kwa kiasi kikubwa mashambulio yake ya anga dhidi ya Al-Shabab, tangu Rais Donald Trump alipochukua mamlaka.

Maofisa nchini Somalia walisema kundi hilo limeongeza mashambulio mjini Mogadishu kama hatua ya kulipiza kisasi dhidi ya mashambulio ya anga ya Marekani.

Katika taarifa yake kuhusiana na shambulio hilo, Marekani imelaani vikali shambulio la Baledogle na Mogadishu na ikiwapongeza maofisa wa usalama waliofanikiwa kuzima shambulio hilo.

Mhariri wa BBC Afrika, Mary Harper, alisema kuwa kutokana na ukweli kwamba al-Shabab waliweza kushambulia maeneo mawili ya kigeni katika siku moja hii inaonyesha kuwa kundi hilo linaratibiwa na ujasusi wa hali ya juu.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilisema kuwa al-Shabab bado wanadhibiti eneo kubwa ya nchi ya Somalia na wana uwezo wa kufanya mashambulio makubwa kwa kutumia mashambulio ya kujitoa mhanga, kwa kutumia vilipuzi na silaha ndogo ndogo. **BBC**

## Mhalifu aishi pangoni miaka 17

**BEIJING,** China

POLISI nchini China wamemkamata mhalifu ambaye amekuwa akijificha kwa miaka 17, baada ya kutumia ndege zisizokuwa na rubani kubaini pango alimokuwa akijificha.

Mwanaume huyo mwenye umri wa miaka 63, Song Jiang, amekuwa akitafutwa na polisi baada ya kutoroka jela ambapo alifungwa kwa kufanya biashara haramu ya kuwasafirisha wanawake na watoto, lakini aliweza 'kuyeyuka' kutoka kwenye kambi ya jela mwaka 2002.

Alidaiwa amekuwa akiishi ndani ya pango dogo na kukata mawasiliano ya aina yoyote na binadamu kwa miaka mingi. Polisi katika mji wa Yongshan, walipokea taarifa kuhusu ni wapi alipo Song kwa mujibu wa maelezo yao waliyoyachapisha katika akaunti ya mtandao wa kijamii wa WeChat. Taarifa hizo ziliwapeleka hadi katika eneo la milima iliyopo nyuma ya mji anakotoka katika jimbo la Yunnan lililopo Kusini Mashariki mwa China. Baada ya kushindwa kumpata katika msako wa kawaida, maofisa walituma ndege zisizokuwa na rubani za ziada ili kuwasaidia polisi katika msako huo.

Hatimaye ndege hizo zilibaini chumba chenye rangi kwenye eneo la mteremko mkali pamoja na taka zilizokuwa kando ya makazi yaliyopo karibu na eneo hilo. Ndipo polisi walipoamua kutembea kwa miguu hadi katika eneo hilo na kumkuta Song ndani ya pango dogo ambako amekuwa akiishi kwa miaka karibu 17.

Kwa mujibu wa polisi, mwanamume huyo amekuwa akiishi kwa kujificha muda mrefu kiasi kwamba ilikuwa ni vigumu kwake kuwasiliana na maofisa usalama, baada ya kukamatwa amerudishwa upya gerezani. **BBC**



Pango alilokuwa anaishi Song Jiang. **PICHA MTANDAO**



Maofisa wakibeba jeneza la Rais Chirac wakati wa misa ya maombolezo iliyofanyika jana. **PICHA MTANDAO**

## Dunia yamuaga Jacques Chirac

**PARIS,** Ufaransa

VIONGOZI wa mataifa mbalimbali dunia na Wafaransa wametoa heshima za mwisho kwa Rais wa zamani wa Ufaransa Jacques Chirac (87) (pichani).

Aidha, baadhi ya viongozi wa dunia, akiwamo Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Frank-Walter Steinmeier, Vladimir Putin wa Urusi na mwenyekiti anayemaliza wadhifa wake wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya, Jean-Claude Juncker, wanampa heshima za mwisho Rais wa zamani wa Ufaransa Jacques Chirac.



Rais Emmanuel Macron na viongozi wengine wa dunia walihudhuria misa katika Kanisa la Saint Sulpice mjini Paris, siku moja baada ya maelfu ya Wafaransa kupiga foleni ili kumuaga Chirac ambaye jeneza lake lilipambwa kwa bendera ya Ufaransa likiwekwa katika kasri la kumbukumbu la Les Invalides.

Jana ilitangazwa kuwa ni siku ya maombolezi nchini Ufaransa. Taasisi zote za serikali na shule pamoja na watu watakaa kimya kwa dakika moja kuomboleza kifo cha rais huyo wa zamani anayetajwa kuwa kipenzi cha Wafaransa.

Uchunguzi wa maoni ya wananchi umedhihirisha kwamba Wafaransa wengi wanamuenzi Jacques Chirac, kuwa kiongozi bora zaidi sawa na Charles de Gaulle na hasa kutokana na uamuzi wake wa kupinga uvamizi wa Marekani nchini Iraq mwaka 2003.

Jacques René Chirac alikuwa Rais wa Ufaransa kuanzia mwaka 1995 hadi 2007, alifariki dunia Alhamisi wiki iliyopita, akiwa na miaka 87. **DW**

# Huduma ya kliniki chini ya mti Dar

**Na Beatrice Moses**

HUDUMA ya kliniki ya watoto na wajawazito inatolewa chini ya mti wa mkwaju uliopo nje ya Ofisi ya Serikali ya Mtaa wa Saranga wilayani Ubungo, jijini Dar es Salaam.

Hali hiyo imesababisha wananchi kadhaa kujiwekea maazimio ya kuchangishana fedha na kujitolea nguvu kazi ili kujenga jengo litakalotumika kutoa huduma hiyo, ambayo hutajwa ni muhimu kwa kuwa husaidia kupunguza idadi ya vifo vya uzazi na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Saranga, Godwin Muro, akizungumza kwenye mkutano wa hadhara uliodhuriwa na baadhi ya wakazi wa eneo hilo, alisema mara kadhaa amejikuta akilazimika kupisha wajawazito kupimwa kwenye ofisi yake.

"Huduma hiyo inatolewa katika hali duni, wananchi wenye hekima na busara tunapaswa kufanya kitu hapa badala ya kuisubiri serikali, nashukuru kuna wadau kadhaa wameanza kuchanga vifaa vya ujenzi na fedha ili kuwezesha ujenzi huu kuanza," alisema Muro.

Alisema anaamini kuwa wakazi wa eneo hilo wakiwa na nia moja na wakiunganisha nguvu za hali na mali itawezesha jengo la zahanati walilokusudia kulijenga lenye vyumba vitatu na maabara litakamilika, hivyo kuwezesha huduma za afya kutolewa kwenye mazingira mazuri.

Mwenyekiti wa Kamati ya uchangiaji, Deogratus Mugizi, alisema awali jengo hilo lilipaswa kujengwa miaka miwili iliyopita, lakini kukajitokeza hali ya kusuasua kwenye michango tofauti na walivyokubaliana.

"Tulifanikiwa kuchanga fedha kama Sh. milioni mbili tukanunua tofali 2,000, hata hivyo, kuna baadhi ya watu wasio waaminifu wamekuwa wakiiba hizo tofali, naamini tunapokwenda kuanza ujenzi huu sasa itasaidia kuamsha mwitikio wa wananchi kufanikisha jambo hilo."

Katika mkutano huo wananchi walikubaliana kila kaya itoe mchango wa Sh. 10,000 kwa utaratibu ambao utahusisha kupewa risiti za serikali, ikiwa ni hatua ya kuhakikisha fedha zinatumika ipasavyo.

Baadhi ya wakazi waliotajwa jana kuchangia vifaa vilivyoko kwenye mabano ni Aloyce Shayo (tofali 200), Billy Mwakatage (mifuko 15 ya saruji) Umoja wa wanawake Saranga (tofali 200).

Wakazi wa eneo hilo wamekuwa wakitibiwa kwenye Kituo cha Afya cha Kimara, ambacho kinahudumia wananchi kutoka kwenye mitaa tisa ya Kata ya Saranga ambayo kwa sasa haina zahanati.



Kaimu Mkurugenzi wa Wateja wa Rejareja wa Benki ya NBC, Benjamin Nkaka (kushoto), pamoja na Meneja wa Benki hiyo Tawi la Chang'ombe wilayani Temeke, Saada Matitu (aliyevaa fulana nyeusi) wakifungua pazia ili kuonyesha zawadi zitakazotolewa kwa washindi mbalimbali wakati wa kampeni maalum inayofahamika kwa jina la 'Ibuka Kidedea na NBC Malengo' iliyozinduliwa jana, jijini Dar es Salaam, ikilenga kuhamasisha wateja wa benki hiyo na jamii kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba kupitia akaunti ya malengo ya benki hiyo. Wengine ni wafanyakazi wa benki hiyo tawi la Chang'ombe. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ireland kuwekeza sekta ya maziwa

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (anayeshughulikia mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, amekutana na wawekezaji kutoka Jamhuri ya Ireland kwa ajili ya kuangalia fursa ya kuwekeza katika sekta ya maziwa nchini.

Wawekezaji hao kutoka Shirika la Sustainable Systems la Ireland (SFSI), wako nchini kuangalia fursa za uwekezaji katika sekta hiyo hususani katika kuyaongezea thamani ili kupanua zaidi soko la maziwa kutoka Tanzania kwenda nje ya nchi.

Prof. Ole Gabriel alisema maziwa yatakapoongezewa thamani yataiwezesha Tanzania kuingia zaidi katika masoko ya nje ya nchi yakiwamo ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Tunataka waongeze zaidi mnyonyoro wa thamani namna ya kuyaongezea thamani ili tuingie katika soko la Afrika Mashariki, nje na ndani ya SADC... kazi inayotakiwa kufanywa ni kuwasisitiza wafugaji kuzalisha maziwa yenye ubora wa kuingia katika soko," alisema Prof. Ole Gabriel.

Alisema wizara yake inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha inatengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji ili soko la maziwa liendelee kuwapo.

Prof. Ole Gabriel alisema kwa sasa Tanzania inazalisha maziwa lita bilioni 2.7 kwa mwaka, huku akisisitiza kwamba juhudi kubwa inayopaswa kufanyika sasa ni kuyaongezea thamani ili kukuza soko ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi wa SFSI ambalo lipo chini ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Bahari ya Jamhuri ya Ireland, David Butler, alisema shirika hilo limekuwa likifanya kazi nchini mbalimbali, na linafanya vizuri katika sekta ya nyama na maziwa kwa zaidi ya miaka 40, ikiwamo kuendesha programu za kilimo na mifugo.

Butler ambaye aliongozana na Dk. Seamus Crosse kutoka Shirika la Kimataifa la Greenfield la Jamhuri ya Ireland, wanatarajia pia kukutana na wataalamu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na taasisi zilizo chini ya wizara hiyo ili kuangalia namna bora ya uwekezaji katika tasnia ya maziwa nchini.

# Mabati ya Alaf yasogezwa Kigamboni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha uchumi wa viwanda unakwenda sambamba na ukuaji wa masoko nchini, huku mlaji wa mwisho ambaye ni mwananchi anapata bidhaa pasipo usumbufu, kampuni ya uzalishaji wa mabati na vifaa vingine vya uwezekaji, Alaf Limited, imesogeza huduma hiyo mtaa wa Feri, Wilaya ya Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Alaf, Dipti Mohanty, alisema lengo la huduma hiyo kufunguliwa Kigamboni ni kuhakikisha ujenzi wa wilaya hiyo unaenda kwa kasi kwa wananchi kutopata tabu ya kupata vifaa vya ujenzi.

Sababu nyingine ni kuongeza ushindani kwa mabati yanayotoka nje ya nchi kwa kuwavutia wateja kupenda bidhaa zinazotengenezwa nchini.

Aidha, alisema duka hilo la maonyesho litawanufaisha wananchi wa Wilaya ya Kigamboni na maeneo ya jirani kupata majibu ya haraka ya mahitaji yao, kujifunza kuhusu bidhaa mbalimbali za Alaf na kuweka oda za mahitaji yao ya mabati.

"Lakini wateja wataweza kununua bidhaa mbalimbali za Alaf, kupata ushauri wa kitaalamu kutoka kwa wataalamu wetu waliobobea kwenye fani ya upauaji," alisema.

# Wananchi 55,000 wapata fursa umeme

**Na Gurian Adolf,** Katavi

ZAIDI ya wakazi 55,000 wa Kata za Majimoto na Mamba Halmashauri ya Mpimbwe mkoani Katavi, wamenufaika na umeme wa REA uliowashwa juzi.

Hatua hiyo imekuja baada ya kampuni ya kichina ya CRCEBG kukamilisha mradi kwa wakati na kuwashwa kwa wakazi wa kata hizo ulifanyika jana kwenye Kata za Majimoto na Mamba na uzinduzi huo ulifanywa na mkuu wa mkoa huo, Juma Homera.

Meneja wa Tanesco Mkoa wa Katavi, Mhandisi Felix Olang, alieleza serikali imehakikisha wananchi wa kata hizo wapatao 55,234 wanafikiwa na nishati ya umeme.

Mradi huo wa umeme wa REA umetekelezwa na kampuni ya kichina ya CRCEBG ambayo imeweza kutekeleza mradi huo kwa wakati.

Alisema mradi huo una jumla ya kilometa 24 zinazoanzia katika kijiji cha Ntimbila hadi Majimoto ukiwa na laini kubwa na transfoma kutokana na ukubwa wa kata hizo kuwa na viwanda vingi vya kukoboa nafaka na wafanyabiashara.

Homera aliwata wakazi wa kata hiyo kutumia vizuri fursa ya kuingiza katika nyumba zao wakati wa mradi huo haujafungwa kwani gharama yake kwa sasa ni Sh. 27,000, lakini mradi utakapofungwa gharama ya kulipia itaongezeka.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA


**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**BENEDICT EMIL NINHO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **T 310/15** kilichotolewa na **KAZIMA SEKONDARI TABORA MWAKA 1971.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polis: **TAB/RB/2402/2019.**

115438002

## KUPOTEA KWA CHETI



**CYLIVIA C. CHOMOLA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **NS 0256/0007** kilichotolewa na HURUMA GIRLS SEKONDARI MWAKA 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polis: **DAR/KIJ/RB/313789/2019.**

115438102

## KUPOTEA KWA CHETI



**FULANO LOZALIA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **PS 1782/084** kilichotolewa na NYABUBINZA SEKONDARI MWAKA 2013.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polis: **DAR/GOG/RB/232376/2019.**

215439002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya Mwanzo ya ………..ARUSHA MJINI**
**Wilaya ya………………… ARUSHA**
**MADAI NAMBARI………………….. 108 YA 2019**
**amdai**
**Mdai………………………… MAGRETH RAPHAEL MUSHI**
**Mdaiwa ……………………..STEPHEN SAMWEL FUPPI**

**Kwa …………………………STEPHEN SAMWEL FUPPI**
**Wa Moshono-Arusha.**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba /eleza habari za Madai:-

**FIKA MAHAKAMANI KUJIBU MADAI YA TALAKA.**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATATU
tarehe 7-10-2019 saa 03:00 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati iliyotolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 27.9.2019

115438602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ADAM SERENGE HAIDARY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 787 DMU TOYOTA KLUGER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/97437/2019.**

115439602

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 65 OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late HEDTJARN NILS RAGNAR**

**And**

**In the matter of the Application for letters of Administration by ESTHER KALUNDE BARROS**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.
Objections (if any) to the grant should be filed on or before day of 9th October, 2019.
The will of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.
Date 12th this day of September 2019

Resident Magistrate
DODOMA

115438702

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MZENA KAMPAN LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 485 AVE BOXER.** Chassis namba **MD2A21BZFWAS1802.** Engine namba **PFZWFA40042.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/179653/2019.**

115438902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CHRISTOPHER PETER MATUTU** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI yenye namba za usajili **T358DNS.** Chasis No. **1215064827.** Engine No **1215064827.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/DOD/RB/250847/2019.**

115438802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**IDARA YA UHAMIAJI**

**OMBI LA URAIA**



**BIBI. MARYAM SAEED SAEED AL-AMOUDI**
**S.L.P 156 MUHEZA**

Tangazo limetolewa kwamba, mtu ambaye picha yake imetolewa hapo juu anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa mambo ya Ndani ya nchi. Mtajwa kwa sasa ni raia wa ***YEMEN na anatokea nchi ya YEMEN ni Mama wa Nyumbani.***

Mtajwa amekuwepo hapa nchini kwa miaka 16. kwamba mtu yeyote mwenye taarifa au sababu kwanini mwombaji asipewe uraia apeleke sababu hizo kwa maandishi yaliyosainiwa kwa Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, S.L.P 512 Dar es salaam.

**Kny.KAMISHNA MKUU WA UHAMIAJI**

115439302


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie
0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MCTOMINAY: SOLSKJAER NI MTU SAHIHI MAN UNITED




**MANCHESTER,** England

SCOTT McTominay anaamini kwamba kocha, Ole Gunnar Solskjaer ambaye anaonekana kukalia kuti kavu kwa sasa ni mtu sahihi kuendelea kuiongoza Manchester United na anaweza kufikia mafanikio ya Alex Ferguson.

United imekuwa na mwanzo mbaya wa msimu huu chini ya Solskjaer ikishinda mechi mbili kati ya sita za ufunguzi wa Ligi Kuu.

Ed Woodward, Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa klabu hiyo, amezungumzia umuhimu wa uvumilivu na kiungo, McTominay na ana matumaini raia huyo wa Norway anatakiwa kupewa muda zaidi ili afanye kazi yake vizuri.

David Moyes, Louis van Gaal na Jose Mourinho wote walishindwa kufikia mafanikio ya gwiji Ferguson aliyestaafu mwaka 2013.

"Inachukua muda kwa kocha mpya kuweza kuweka mambo sawa," alisema McTominay akiliambia Gazeti la The Mirror.

"Si jambo la ghafla tu kuweza kupata mafanikio, inachukua muda na anahitaji kupewa muda zaidi.

"Mara baada ya Sir Alex kuondoka, itachukua muda klabu kupata kocha sahihi, na naamini kwamba, Ole ni mtu sahihi kwa sasa.

"Unaona kuna zama tofauti kwenye soka, kila mmoja anapitia kipindi cha mpito na sisi ndio tunapitia wakati huo kwa sasa."

## Ribery: Najiona kijana dimbani

**MIILAN,** Italia

FRANCK Ribery amesema licha ya umri wake kusonga, lakini akiwa uwanjani anajihisi kama kijana mdogo, baada ya kuonyesha kiwango cha juu wakati Fiorentina ikiifumua AC Milan mabao 3-1, juzi Jumapili.

Mkongwe huyo raia wa Ufaransa aliifungia timu yake bao la tatu kwenye mchezo uliopigwa dimba la San Siro na alishangiliwa na umati wa mashabiki baada ya kufunga na kutolewa nje.

Ribery alionekana kuwa mwiba mkali kwa kikosi cha Milan, ambao walimaliza wakiwa na wachezaji 10.


Kwa sasa Ribery ana umri wa miaka 36, lakini amesisitiza bado ana mapenzi na soka na hivyo ataendelea kucheza.

"Nina furaha, wakati unapocheza kwenye Uwanja wa San Siro, mara zote unakuwa wakati maalumu. Ni uwanja mkubwa na wenye mashabiki wengi," alisema akiiambia Sky Sport Italia.

"Ni wakati mbaya kwa mashabiki wa Milan kwa sasa, lakini tulicheza kwa kiwango cha kuvutia na hilo ni muhimu kwetu.

"Ndio, mimi nina umri mkubwa, lakini najhisi kijana nikiwa uwanjani. Soka ni maisha yangu, naupenda mchezo huu. Nilikuwa na njaa wakati nilipofika Fiorentina na nimefurahia kuona mambo yanakwenda vizuri.

"Nimekuja kuisaidia Fiorentina, wachezaji na mashabiki. Nina furaha, lakini natakiwa kufanya kazi kwa bidii kila siku, kila wiki kucheza vizuri kama nilivyocheza leo."






## *Majaliwa ya Sancho hayajulikani*

**DORTMUND,** Ujerumani

MKURUGENZI wa Soka wa Borussia Dortmund, Michael Zorc, amesema hakuna maamuzi yoyote yaliyofanywa kuhusu majaliwa ya Jadon Sancho anayewaniwa na Manchester United.

Sancho ameendelea kuhusishwa na mpango wa kutakiwa na United, ambao wameripotiwa kwamba, wana muwania nyota huyo wa England kwa udi na uvumba.

'Mashetani Wekundu' hao walijaribu kutaka kumsajili Sancho wakati wa kipindi cha majira ya joto, lakini walishindwa kumrudisha England mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 ambaye aliondoka Manchester City na kutua Dortmund mwaka 2017.

Alipoulizwa kuhusu majaliwa ya Sancho baada ya mwaka 2020, Zorc aliliambia Gazeti la Kicker: "Hakuna maamuzi yaliyofanyika, lakini huwezi kuwa nabii kujua kwamba hatacheza tena hapa kwa miaka mitano mingine."

Sancho amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji wenye vipaji vya juu barani Ulaya baada ya kuondoka Ligi Kuu miaka miwili iliyopita.

Amefunga mabao 12 na kutoa pasi za mwisho 14, wakati Dortmund ilipomaliza nafasi ya pili nyuma ya Bayern Munich kwenye msimamo wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu uliopita. Na tayari Sancho amefunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho nne msimu huu.

"Amekuwa na muda wa kujiimarisha hapa Dortmund. Nina shaka kama angekuwa na klabu za Uingereza," alisema Zorc.

"Tunawaamini wachezaji vizuri, na hatuhofii kuwaacha wao wacheze. Na analijua hilo."

HABARI MICHEZO

# Man United yasaka mshambuliaji mpya

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United chini ya kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer wanajipanga kutafuta mshambuliaji mpya katika kikosi hicho, kwa mujibu wa Gazeti la Daily Mail.

Man United imeanza vibaya msimu huu kwa kushinda mechi mbili tu kati ya sita za Ligi Kuu na imebainisha kwamba, safu yake ya ushambuliaji imekuwa butu na hivyo wanajipanga kutafuta mshambuliaji.

Kwa mujibu wa Daily Mail, Man United itaingia sokoni wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari kwa ajili ya kusaka mshambuliaji huyo.

Solskjaer amewapoteza washambuliaji Romelu Lukaku na Alexis Sanchez waliojiunga na Inter Milan katika usajili wa majira ya kiangazi.

Kocha huyo amewaeleza vigogo wa bodi ya klabu hiyo anataka mshambuliaji mwenye kiwango bora cha kufunga mabao Man United.

"Ndio tumewapoteza Alexis na Romelu, tunahitaji mshambuliaji mbunifu mwenye kiwango bora cha kufunga mabao," alisema Solskjaer.

"Naamini kwamba, dirisha la usajili la Januari utakuwa wakati mzuri kwa upande wetu kutafuta mshambuliaji ambaye ataweza kuongeza nguvu kwenye kikosi chetu.

"Kwa sasa bado tuna tatizo la ufungaji, ingawa nina wachezaji vijana, bado hawana uzoefu wa kutosha, hivyo ni lazima tutafute mshambuliaji mpya kwa ajili ya kuwa na nafasi ya kuweza kufunga.

"Tutaangalia nini kitatokeo wakati wa dirisha dogo la usajili, lakini nina imani kubwa tutaingia sokoni."

Nguli huyo wa zamani wa timu hiyo alisema hakuna namna zaidi ya kumpiga bei Lukaku kwa kuwa hakutaka kubaki Old Trafford.

Kocha huyo alisema safu yake ya ulinzi inafanya vema, lakini hana furaha na namna washambuliaji wanavyocheza.






# EMERY AJIPANGA KUMPIGA BEI OZIL

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imepanga kumtoa kwa mkopo nyota wake, Mesut Ozil katika dirisha dogo la usajili Januari, mwakani.

Kocha wa Arsenal, Unai Emery, amepanga kumtoa Ozil baada ya kukosa namba katika kikosi cha kwanza.

Emery anaamini mpango wake utafanikiwa licha ya kiungo huyo wa Ujerumani kulipwa mshahara mkubwa wa pauni 350,000 kwa wiki.

Kocha huyo amekaririwa akidai mchezaji huyo wa zamani Real Madrid ameshindwa kuelewa mfumo wake wa ufundishaji.

Licha ya kukosa namba kikosi cha kwanza, Ozil ambaye mkataba wake umebakiza miaka miwili anataka kubaki Emirates.

Ozil ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa Arsenal, lakini anapambana kupata namba kikosi cha kwanza.

# *Kocha wa AC Milan hatarini kutimuliwa*

**MILAN,** Italia

BAADA ya timu ya AC Milan kukutana na kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa Fiorentina, kocha wake, Marco Giampaolo yupo kwenye hatari ya kupoteza kibarua chake.

Kibarua cha Giampaolo kipo hatarini baada ya kufungwa mechi nne kati ya sita katika mashindano ya Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu huu.

Kocha huyo alirithi mikoba ya Gennaro Gattuso ambaye aliiongoza kwa misimu miwili kabla ya kutimuliwa.

Hii ni mara ya kwanza baada ya miaka 80 kwa AC Milan kupata matokeo mabaya kama hayo.

Baada ya kichapo hicho, AC Milan kwa sasa inashika nafasi ya 16 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Italia.

Kipigo dhidi ya Fiorentina kinakuwa cha tatu mfululizo kwa timu hiyo inayotumia dimba la San Siro.


Matokeo kama hayo kwa mara ya mwisho waliyapata msimu wa mwaka 1938-1939.

Kocha huyo alidai anawajibika kwa matokeo hayo, lakini bado ana nafasi ya kufanya maajabu katika mechi zinazofuata.

AC Milan ilicheza pungufu baada ya Mateo Musacchio kulimwa kadi nyekundu kwa kumchezea madhambi Franck Ribery.



# DONDO SOK
## MAGAZE A ULAYA



# VAN DIJK: UBINGWA LIVER BADO MAPEMA

**Kila mmoja analitambua hilo kwa sababu msimu uliopita tuliona namna mambo...**

**LIVERPOOL,** England

VIRGIL van Dijk ameweka wazi kuwa ni mapema mno kwa Liverpool kufikiria kuhusu ubingwa wa Ligi Kuu England, huku akisisitiza kwamba kuongoza kwao kwa pointi tano zaidi ya mabingwa watetezi, Manchester City hakumaanishi chochote.

**Liverpool ipo mbele pointi tano zaidi baada ya mechi saba wakati huu ikitazama kutwaa ubingwa wa ligi hiyo kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990.**

Kocha Jurgen Klopp wa Liverpool, ambaye ameibebesha ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19, pia alikuwa na wakati mzuri katika Ligi Kuu msimu uliopita kabla ya uongozi wao wa pointi saba kupinduliwa na Man City katika vita vya mbio za ubingwa huo.

Na baada ya Jumamosi kushinda bao 1-0 ugenini dhidi ya Sheffield United , kumeifanya kushinda mechi saba mfululizo za mwanzo huu wa msimu, na beki kisiki wa Liverpool, Van Dijk alisema: "Haimainishi chochote [kuongoza kwa pointi tano]. Ni mapema sana. Ndiyo kwanza tupo Oktoba na kipindi kigumu kitakuja.

"Bado kuna mechi nyingi zimebaki na kitu pekee tunachoangazia ni mechi zilizopo mbele yetu. Hatutaki kutazama kuhusu wengine kwa sababu hakuna faida yoyote ya kufanya hivyo.

"Kila mmoja analitambua hilo kwa sababu msimu uliopita tuliona namna mambo yalivyogeuka haraka. Tunachotaka ni kutazama mechi ilipo mbele yetu."

Liverpool haijapoteza ugenini mechi ya Ligi Kuu tangu Januari ilipofungwa na City - ikishinda mechi 12 wakati pia 'Wekundu' hao hawajafungwa wakiwa katika uwanja wao wa Anfield tangu Aprili 2017.

"Ni vyombo vya habari ambavyo vinapenda takwimu. Ukweli ni kwamba hatuna chochote kwa sasa. Tunataka kuendelea kufanya vizuri na bado kuna nafasi kubwa ya kujizatiti," aliongeza Van Dijk, ambaye Liverpool yake inaikaribisha Salzburg katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya keshokutwa, Jumatano.

"Tunapaswa kujiamini; unapaswa kufikiri unakwenda kushinda kila mechi vinginevyo lazima pia ubaki nyumbani. Tunao ubora, tunao wachezaji.

"Tutabeba ubora huu na kisha kujiandaa kwa mechi dhidi ya Salzburg na hiyo itakuwa mechi ngumu pia. Tunapaswa kushinda kila mechi, hivyo ndivyo ilivyo."

## ZISIKUPITE

### OZIL KUTOLEWA JANUARI

ARSENAL inataka kumtoa kwa mkopo kiungo wao wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani, Mesut Ozil katika dirisha la Januari, hata kama itahitajika kumchangia sehemu ya mshahara wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. ***(Mirror)***

### CONTE AMGEUKIA MATIC

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte yupo tayari kumwajiri kiungo wa kimataifa wa Serbia na Manchester United, Nemanja Matic, 31. ***(Calciomercato)***

### SOLSKJAER ASAKA STRAIKA

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer amethibitisha kuwa kipaumbele chake sokoni kitakuwa ni kusajili mshambuliaji na kuongeza nguvu ya kuiimarisha timu ya Manchester United ambayo imeshindwa kufunga zaidi ya mara moja katika mechi 17 kati ya 20 zilizopita. ***(Telegraph)***

### HAALAND KUIWAHI LIVER

Red Bull Salzburg inatumai mshambuliaji wao, Erling Haaland, 19, atapona ugonjwa unaomsumbua na kuwa fiti kuivaa Liverpool Jumatano kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

### EMERY APINGA LUGHA SHIDA

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amekana kuwapo kwa tatizo la lugha ambalo linasababisha kushindwa kuwasiliana na wachezaji, lakini akaeleza uwezo wake wa Kiingereza ni sita ya kumi. ***(Mirror)***

### MANDZUKIC WA JANUARI UTD

DIRISHA la januari Manchester United itamfuata mshambuliaji wa Juventus na Croatia, Mario Mandzukic, 33, ambaye alikuwa katika mipango yao majira ya joto. Juve inaweza kuhitaji ada kiasi cha pauni milioni tisa, wakati Mandzukic atakuwa hategemei kupunguza kiasi cha pauni milioni 4.5 anacholipwa kama mshahara wake kwa mwaka. ***(Goal.com)***

### KLOPP KUMFUNGA MILNER

KIUNGO wa Liverpool, James Milner, 33, yupo katika mwaka wa mwisho kwenye mkataba wake na klabu hiyo, lakini Kocha wa 'Wekundu' hao, Jurgen Klopp anaamini ataongeza mkataba mpya. ***(Express)***

### PERISIC AFUNGUKA UNITED

WINGA wa Bayern Munich, Ivan Perisic, 30, ambaye yupo kwa mkopo katika klabu hiyo ya Ujerumani akitokea Inter Milan, amesema "alikaribia sana" kujiunga na Manchester United wakati Jose Mourinho alipokuwa akiinoa miamba hiyo ya Old Trafford. ***(Athletic, via Express)***

### MERTENS KUONDOKA NAPOLI

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ubelgiji na Napoli, Dries Mertens, 32, anaonekana anajiandaa kuondoka akiwa huru katika klabu hiyo majira ya joto yajayo. ***(Calciomercato)***

### PETIT AMWONYA EMERY

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Emmanuel Petit amemwonya kocha Unai Emery dhidi ya tabia yake ya kubadili kikosi mara kwa mara. ***(Sun)***

## Morocco kuendelea kuifundisha Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limemtangaza Hemedi Morocco kuendelea kuwa Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Zanzibar (Zanzibar Heroes) ambayo inatarajia kuanza maandalizi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Mashindano ya Kombe la Chalenji yanayoandaliwa na Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), mwaka huu yamepangwa kufanyika mapema Desemba jijini Kampala, Uganda.

Morocco alikuwa akimsaidia Mnigeria Emmanuel Amunike kuifundisha timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars).

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa ZFF, Mohammed Ali Hilali, alisema kocha huyo atakuwa na jukumu la kuteua kikosi kitakachoshiriki mashindano hayo yanayotarajiwa kushirikisha zaidi ya nchi 10 wanachama wa Cecafa.

Hilali alisema ZFF imeamua kuanza maandalizi mapema ili kumpa muda kocha huyo kuandaa kikosi imara ambacho kitaleta mafanikio katika mashindano hayo ya mwaka huu.

"Tunajua hii ndiyo michuano yetu mikubwa tunayoshiriki, michuano hii ya Kombe la Chalenji ni yenye ushindani, tumempa majukumu mapema, tunataka mara tu Morocco atakapowasili visiwani Zanzibar, yeye mwenyewe atakuwa na jukumu la kuchagua benchi lake la ufundi," alisema Hilali.

## Babu Seya ahamia rasmi Muheza

**Na Steven William,** MUHEZA

MWANAMUZIKI mkongwe Nguza Viking maarufu Babu Seya, amesema kwa sasa amehamia rasmi wilayani Muheza, Tanga huku akifafanua kwamba isingekuwa huruma ya Rais John Magufuli kumtoa jela katika kifungo cha maisha asingeweza kupata mke na kufunga ndoa ambayo imemfanya kuhamia mkoani humo.

Hayo yalisemwa juzi usiku na Babu Seya katika sherehe ya kupongezwa baada ya kufunga ndoa na mchumba wake, Desderia Haule ambaye ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Muheza, iliyofanyika katika ukumbi wa Tate Plus na mamia ya watu.

Babu Seya alisema anamshukuru sana Rais Magufuli kwa kumtoa jela katika kifungo cha maisha kwani bila yeye asingeweza kufunga ndoa na mchumba wake huyo ambaye kwa sasa ni tayari ni mke wake rasmi.

Alisema anaomba sana kupitia sherehe hiyo Magufuli apelekewe salamu kwa kitendo chake cha utu kwa kumtoa jela na sasa amepata mke wa kuishi naye na kwamba amehamia rasmi katika Wilaya ya Muheza.

Kwa upande wake mfanyabiashara katika Wilaya ya Muheza, Teddy Illeti alisema anamtakia maisha mema Babu Seya kwa kupata jiko.

# MAAFANDE POLISI TANZANIA WATAMBA KUIMALIZA YANGA

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Polisi Tanzania kimetua jijini Dar es Salaam salama, huku kikitamba kiko tayari na kamili kuwavaa Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu Bara unaotarajiwa kuchezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Uhuru.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi, alisema wamekuwa imara na wanaamini wataondoka na pointi zote tatu katika mchezo huo.**

Munisi alisema wachezaji wa Polisi Tanzania wamekuwa wakiimarika kila siku na hivyo wamejipanga kupata ushindi dhidi ya wawakilishi hao pekee wa Tanzania waliobaki kwenye mashindano ya kimataifa.

"Tulipoteza mchezo uliopita kwa kukosa bahati, mpira uliochezwa pale haukuwa wa kawaida, sasa hatutarudia makosa tuliyoyabaini tutakapoivaa Yanga, tumejipanga na tuko kamili kuhakikisha tunawafunga, tunashinda na kuendelea kujiweka katika nafasi nzuri," alisema Munisi.

Aliongeza kuwa ligi ya msimu huu ni ngumu, hivyo wanataka kumaliza "kazi" katika mechi za mzunguko wa kwanza.

"Msimu huu zitashuka timu nne, kwa hiyo vita itakavyokuwa huko mwishoni ni kubwa, hatutaki kuwa sehemu ya timu zilizoko katika mstari mwekundu, tumedhamiria kuleta mapinduzi, wachezaji wako tayari kutekeleza kile tulichokiweka katika malengo yetu, naamini tutapata furaha," Munisi alisema.

Aliongeza kuwa kambi ya muda iliyowekwa Kibaha, Pwani kwa muda, imewasaidia kuwaongezea mbinu wachezaji wao na mapumziko ya kupisha kalenda ya kimataifa ilisaidia kuwaondolea uchovu.

"Tumeshafika mjini, hatukua mbali, kambi ndogo ilikuwa Kibaha, na sasa tumeshaingia Dar es Salaam kuendelea kujiimarisha, tumekuja kushindana, tunaijua Yanga vema, naamini hautakuwa mchezo mwepesi," aliongeza kiongozi huyo.

Polisi Tanzania ina pointi tatu baada ya kucheza mechi mbili na katika msimamo wa Ligi Kuu Bara iko kwenye nafasi ya 15, huku wapinzani wao Yanga ambao wamecheza mchezo mmoja wakiburuza mkia kutokana na kutokuwa na pointi hata moja.




Mshindi wa Promosheni ya Faidika na Jero, Frank Kimambo, mkazi wa Kimara Temboni akikabidhiwa simu Janja na mchezaji wa Yanga, Issa Bigirimana (kushoto), baada ya kuibuka mmoja kati ya washindi watano kwenye droo ya wiki iliyopita. SportPesa kwa kushirikiana na tiGO wanatoa simu Janja kila siku huku zawadi ya gari aina ya Renault Kwid ikitarajiwa kutolewa katika droo ya mwisho ya promosheni hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Simba yampa 'ubosi' Kikeke*

**Na Somoe Ng'itu**

UONGOZI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, umemtangaza rasmi Mtangazaji wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Salim Kikeke, kuwa balozi wa klabu hiyo nchini humo, imefahamika.

Kikeke, Mtangazaji wa zamani wa Kituo cha Televisheni cha ITV, kwa sasa yuko nchini kwa mapumziko.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mwekezaji wa Simba, Mohammed "Mo" Dewji, alisema uamuzi wa kumteua Kikeke kuwa balozi wa klabu yao ulifikiwa katika kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kilichokutana mwishoni mwa wiki.

Dewji alisema wanaamini Kikeke atainгaza Simba katika ngazi ya kimataifa na atajenga umoja wa wanachama wa timu hiyo hasa wanaoishi Uingereza.

"Tumemteua Mtangazaji wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Salim Kikeke, kuwa balozi wa Simba Sports Club wa Jiji la London, Uingereza, tunaamini ataitendea haki klabu yake anayoipenda," alisema Dewji.

Kikeke amekuwa akionyesha picha za video mbalimbali akifurahia ushindi wa Simba au kuonyesha kutokata tamaa pale klabu hiyo inapopata matokeo mabaya.

Hata alipokuwa katika mashindano ya Kombe la Mataifa Afrika (Afcon 2019) jijini Cairo nchini Misri, mwaka huu, Kikeke alionekana kuvaa zaidi jezi ya Simba badala ya timu ya Taifa (Taifa Stars).

Pia mara kadhaa anapokuwa katika majukumu yake jijini London, Kikeke amekuwa akiitangaza Klabu ya Simba kwa kugawa jezi na vifaa mbalimbali vyenye nembo ya klabu hiyo iliyoko Mtaa wa Msimbazi, Karikaoo jijini.

# Michezo

Jumanne Oktoba 1, 2019

Nipashe




Van Dijk: Ubingwa Liver bado mapema

UKURASA 30




Washambuliaji wa Simba, Meddie Kagere na Miraji Athumani wakipongezana baada ya kuiongoza timu hiyo kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwa kila mmoja kufunga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Biashara United iliyopigwa katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Aussems: Sasa ni wakati wa samba

## ●●● Akunwa na viwango wachezaji Simba huku uongozi ukimshukia Mkude kwa kutoroka, atakiwa...

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kuvuna pointi sita katika mechi mbili za mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kocha Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Patrick Aussems, amesema anataka kuona kikosi chake kinapata ushindi mnono na kucheza soka la kuvutia 'samba' zaidi kwenye mechi za ligi hiyo zinazofuata.

**Simba iko kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kufikisha pointi 12, ikishinda mechi zote nne ilizocheza dhidi ya JKT Tanzania, Mtibwa Sugar, Kagera Sugar na juzi mjini Musoma, Mara ilipowachapa Biashara United mabao 2-0.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Aussems, alisema bado kikosi chake hakijaonyesha uwezo wake halisi, hivyo anaendelea kuwajenga wachezaji wake waweze kucheza soka la kiwango cha juu na kutumia vizuri nafasi wanazozitengeneza.

Mbelgiji huyo alisema hakuna mechi rahisi katika ligi hiyo, lakini kila mara amewajenga wachezaji wake kujiamini na kuongeza umakini wanapokuwa na mpira.

"Ninahitaji kuona tunacheza soka zuri, utakapocheza vizuri, ni wazi kwamba utapata ushindi mkubwa, utakuwa salama, nina furaha kila mchezaji anaendelea kuimarika, ni jambo zuri kwa timu, kila mchezaji ana morali ya kujituma," alisema Aussems.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema kikosi cha timu hiyo kilirejea jijini jana mchana tayari kuanza kuendelea na maandalizi ya mchezo wake wa raundi ya tano wa ligi hiyo.

"Ndio tumefika muda huu (jana mchana), kuhusu mchezo unaofuata, bado tunasubiri maelekezo kutoka Bodi ya Ligi," alisema kwa kifupi meneja huyo.

Endapo Simba itakosa kupangiwa mchezo mwingine wiki hii, italazimika kusubiri hadi Oktoba 23, mwaka huu kuvaana na Azam FC ambayo nayo imeshatolewa katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

### MKUDE MATATANI

Kiungo wa timu hiyo, Jonas Mkude, ametakiwa kutoa maelezo ni kwa sababu gani aliondoka kambini bila ruhusa na kumfanya ashindwe kusafiri na wenzake kuelekea mikoa ya Kanda ya Ziwa (Kagera na Mara).

Taarifa za ndani kutoka katika klabu hiyo, zinaeleza kwamba, endapo utetezi wake hautapokelewa, kiungo huyo anatarajiwa kusimamishwa au kukatwa sehemu ya mshahara wake.

Kutokana na utoro huo, Mkude amekosa michezo miwili ya Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar na Biashara United, ambayo yote Simba ilifanikiwa kupata ushindi.

# Zahera atangaza vita mpya Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kundi la kwanza la wachezaji wa Yanga lilitarajiwa kurejea nchini jana usiku, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mwinyi Zahera, amesema kuwa wamerudi kwenye mapambano ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kundi la pili la wachezaji wa timu hiyo lilitarajiwa kuwasili nchini leo asubuhi na sasa Yanga inatarajia kuikaribisha Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaochezwa keshokutwa, Alhamisi kwenye Uwanja wa Uhuru, halafu Jumapili itawavaa Coastal Union kutoka jijini Tanga.

Zahera (pichani chini) aliliambia gazeti hili kuwa sasa akili na mipango yao inarejea kwenye Ligi Kuu Bara mpaka pale watakapofahamu mpinzani wao kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

"Soka ni mchezo wa kushindana na kupambana, tumetoka katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, sasa tunarudi kwenye ligi ya nyumbani," alisema kwa kifupi kocha huyo Mkongomani.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia gazeti hili jana kuwa, wachezaji wao watarejea nchini kwa makundi mawili na baada ya kuwasili watajiandaa na mechi zao mbili za ligi zitakazochezwa hapa jijini.

"Timu inarejea leo (jana) usiku, mechi zetu zimesogezwa mbele, mchezo dhidi ya Polisi Tanzania utachezwa Oktoba 3, mwaka huu ile ya Coastal Union itachezwa Oktoba 6," Bumbuli alisema.

Yanga iliyocheza mchezo mmoja tu, na ambayo ilifungwa bao 1-0 na Ruvu Shooting, inaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo inayoongozwa na watani zao, Simba wenye pointi 12 baada ya kushuka dimbani mara nne.



GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002